Kikao cha Kumi – Tarehe 26 Oktoba, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia asubuhi hii kufika tukiwa wazima wenye afya njema. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hati Mezani kuhusu Hoja yangu Binafsi kwa Wanafunzi Waliokosa Kupata Mkopo wa Elimu ya Juu. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma. Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea tunao wageni pale juu ambao wamekuja kwa ajili ya kujumuika nasi katika shughuli zetu za leo. Wageni wetu waliopo leo ni Jumuia ya Wanafunzi wa Vyuo Vikuu na Elimu ya Juu pamoja na Wanafunzi wa Vyuo Vikuu kutoka Zanzibar na idadi yao ni 35.

Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe mutambue kuwepo kwao, ambao wamekuja maalum kwa ajili ya kuhudhuria vikao vyetu na kuona wazee wao wanafanya nini kwa ajili yao. *(Makofi)*

Vijana wetu mnakaribishwa sana katika ukumbi huu, ili muone Baraza hili linafanya nini kwa ajili yenu, karibuni sana. Ahsante Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 72

Usambazaji wa Askari Polisi kwa Kutumia Malori

Mhe. Ali Salum Haji – Aliuliza:-

Jeshi la Polisi kwa muda mrefu limekuwa likitumia magari aina ya lori kusambaza askari wake vituo kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya ulinzi. Jambo la kushangaza na

kusikitisha, magari hayo ni mabovu na yanashusha hadhi ya jeshi hilo na askari wake kwa ujumla.

Je, ni lini jeshi hilo litapatiwa usafiri unaoendana na hadhi ya askari wetu na umuhimu wao kwa taifa?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais) – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 72 kama hivi ifuatavyo:-

Lakini kabla sijamjibu naomba kutoa maelezo ya ziada. Mhe. Spika, ufanisi wa kazi za polisi unategemea vifaa mbali mbali vikiwemo magari, ambayo hununuliwa kutokana na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mara nyingi hutoa michango yake mbali mbali kwa kulipatia jeshi hilo huduma za magari.

Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti yetu imekuwa vigumu kukidhi mahitaji yote ya magari kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Polisi kwa kutegemea mchango wa SMZ. Kutokana na hali hiyo, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na serikali limekuwa likichukua hatua wakati baada ya wakati, ili kuweza kuwa magari kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama hivi ifuatavyo:-

Nia ya serikali ni kununua magari mapya kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Polisi kila wakati fedha zitakapopatikana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Jeshi la Polisi kama alivyosema Mhe. Waziri ni Jeshi la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile kila zinapopita bajeti basi na Wizara ya Mambo ya Ndani nayo huwa inapitishiwa bajeti kwa ajili ya kuhudumia wizara yake.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Muungano ni wakati gani ambapo magari yalinunuliwa haya yaliopo na muda gani kwa sababu bajeti imeshapitishwa watanununuliwa askari hawa magari?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais): Mhe. Spika, ni wakati gani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilishirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kununua magari haya mapya.

Kwa kweli ni muda mrefu sana inafika hata miaka minne tokea bajeti hizo mbili kutumika kwa ajili ya kununua magari haya. Lakini kama nilivyosema mwanzo Jeshi la

Polisi liko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hivyo, jukumu kubwa ni Bajeti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio inayotakiwa kukidhi haja ya kununua vifaa na wala si magari tu, isipokuwa ni vifaa vyote vinavyotumika kwa Jeshi hili la Polisi.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali amekiri kuwa kuwepo kwa vifaa kunasaidia ufanisi wa kazi hasa katika Jeshi la Polisi. Swali langu lipo hapa kwa kuwa hivi sasa hakuna vifaa katika Jeshi la Polisi hususan magari, hivi anataka kutuambia ufanisi wa kazi katika Jeshi hili hivi sasa haupo?

(b) Kwa kuwa Jeshi la Polisi katika Wilaya ya Magharibi wanao gari moja tu, ambayo inatumika na Mkuu wa Kituo. Je, shughuli za jeshi hili katika Wilaya ya Magharibi zitafanikiwa vipi ikiwa kuna gari moja ambayo ndio ya Mkuu wa Kituo?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais): Mhe. Spika, nitaanza kulijibu la (b) na baadaye la (a)

Mhe. Spika, kwa Mjini Magharibi kuwepo gari moja kwa ajili ya matumizi ya mkoa au wilaya nzima nakubaliana na yeye kwamba hapatapatikana mafanikio makubwa ya utekelezaji wa shughuli zote za polisi.

Swali la (a) linaoana na lile la (b). Ufanisi upo lakini sio kwa kiwango kinachostahiki, isipokuwa nakubali kwamba wakati jeshi halina magari pamoja na vifaa vyengine halitaweza kufanikiwa majukumu yake.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Jeshi la Polisi ni la Muungano na tunatawaliwa na Katiba mbili, yaani Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar.

Hivyo, kukikosekana ufanisi katika utekelezaji wa chombo kama hiki cha muungano ni nani mdhamini kikatiba kwa Zanzibar anayepaswa kufuatilia haki za wale wanaolitumikia hapa Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais): Mhe. Spika, ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndio mdhamini wa kufuatilia zile kasoro zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, suala hili linafuatiliwa na waziri anayehusika kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mafanikio ya kuridhisha bado hayajapatikana.

Lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuwasiliana na wahusika wa Tanzania Bara na hasa ilivyokuwa sasa waziri mhusika ni Mzanzibari pengine huenda tukafaidika na manufaa haya ya kupata vyombo hivi ambavyo hivi sasa havipo. *(Makofi)*

Nam. 78

Tatizo la Maji

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:-

Pamoja na serikali kutekeleza mradi mkubwa wa maji kwa Mkoa wa Mjini Magharibi kupitia mkopo wa Serikali ya Japan, bado wananchi wengi wa Mkoa wa Mjini Magharibi wanakabiliwa na tatizo kubwa la maji jambo linaloathiri zaidi wanawake.

Mhe. Waziri hili tatizo kubwa la maji limesababishwa na nini baada ya mradi huo kukamilika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 78 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba kukubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba pamoja na serikali kutekeleza Mradi Mkubwa wa Maji wa Mkoa wa Mjini Magharibi kupitia msaada wa Serikali ya Japan, bado baadhi ya wananchi wa mkoa huo wanakabiliwa na tatizo hilo la maji, kutokana na sababu zifuatazo:-

- Kushuka mno kwa udhalishaji wa vyanzo vilivyokuwepo hapo awali vilivyosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa.
- Kuharibika kwa mfululizo mitambo ya kusukumia maji.
- Uchakavu wa mtandao wa usambazaji maji katika mji wetu.
- Ujenzi holela unaojengwa katika vianzio vya maji.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, tatizo la maji limekithiri katika Wilaya ya Mjini na Mhe. Waziri amekubali, pia amekubali uharibifu wa mabomba katika maeneo mbali mbali ya mjini.

Katika eneo la Makadara kuna bomba kubwa ambalo linasambaza maji kwenye maeneo ya Jimbo la Rahaleo, Kikwajuni pamoja na Mji Mkongwe. Kwa kweli mimi mwenywe binafsi pamoja na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji tumefanya ziara na kumuonesha suala lile, lakini mpaka leo Mhe. Spika bado halijatengezwa.

(a) Je, ni lini bomba lile litatengenezwa?

(b) Mhe. Waziri haoni kwamba hivi sasa kufanya ziara maalum katika majimbo ya Wilaya ya Mji, ili kuona mwenyewe matatizo ya maji yanayowakabili wananchi wetu?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika,

(a) Namhakikishia kwamba avute subira hilo bomba tutakuja kulitengeneza. Kwa hivyo, wizara yangu itajitahidi kulisimamia na kulitengeneza bomba hilo. *(Makofi)*

(b) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ni vizuri kufanya ziara na kutembelea katika sehemu zenye matatizo. Mhe. Spika, katika hili naomba nishirikiane na Mhe. Mjumbe tupite pamoja kwenye maeneo yenye matatizo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii asubuhi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

(a) Mhe. Naibu Waziri atakubaliana nami kuharibika kwa mitambo hiyo ni jukumu la wizara au Mamlaka ya Maji na mamlaka hiyo inashindwa kutekeleza jukumu lake. Kutokana na hali hiyo, wananchi anawaambia nini Mhe. Waziri? *(Makofi)*

(b) Sababu zipi zinazopelekea mitambo hiyo kuharibika kwa haraka?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika,

(a) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba jukumu la kutengeneza mitambo hiyo ni la Wizara ya Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati kupitia Mamlaka ya Maji.

(b) Kinachosababisha mitambo hiyo kuharibika kama nilivyojibu swali ambalo nililojibu kipindi cha nyuma kwamba ni matatizo yanayotokana na kukatika kwa umeme pamoja na shoti zinazotokana na umeme wetu tunaotumia Zanzibar.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba mradi huo wa maji ambao umefadhiliwa na Serikali ya Japan lengo lake ni kuwasaidia Wazanzibari na kwa vyovyote vile fedha hizi ni kwa ajili ya kuwasaidia Wazanzibari.

(a) Hivi ikiwa mradi huu hauna mafanikio je atawaambia Wazanzibari wamekula hasara na fedha hizo za wahisani zimetumika ovyo?

(b) Kwa kuwa Wazanzibari ndio wanaolipa maji na mategemeo ya Wazanzibari baada ya kulipa maji, maana yake watengenezewe miundombinu. Sasa wizara yake inashindwa kutengeneza miundombinu hii je hivi sasa Wazanzibari wasilipie maji? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Serikali haijashindwa kutafuta miundombinu ya maji. Mhe. Spika, mara kadhaa nimekuwa nikizungumza katika Baraza hili kwamba kuna miradi mitatu kwa minne ni hii ifuatayo:-

(a) Mradi wa *ADB*;
(b) China miradi miwili na
(c) Mradi mwengine unakuja kwa ajili ya kusambaza mitandao ya maji.

Mhe. Spika, kazi hiyo inafanywa na serikali kupitia wizara yangu. Kwa hivyo, wananchi nimeahidi katika Baraza hili ifikapo mwaka 2013 suala la matatizo ya maji itakuwa ni hadith au historia. *(Makofi)*

Hivyo, tuchukue msimamo huo na tusubiri ikifika mwaka 2013 Desemba maji nchini hakuna, basi mwenye kutaka kulisema lake aliseme wakati huo. Lakini juhudi za serikali hatulali katika kutafuta mitandao mipya ya maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

Nam. 73

Wizi wa Waya za Umeme Kutokana na Biashara ya Vyuma Chakavu

Mhe. Mjumbe, aliyeuliza swali hili ameliondolea.

Nam. 56

Vyombo vya Usafiri kwa Maafisa wa Habari

Mhe. Kazija Khamis Kona – Aliuliza:-

Kwa kuwa miaka ya zamani Maafisa Habari wa Wilaya na Mikoa na Maafisa Uhusiano wa Mikoa walikuwa wakipatiwa vyombo vya usafiri kama pikipiki na vespa na kwa kuwa miaka mingi sasa suala hilo limesitishwa kabisa wakati mahitaji ya vyombo hivyo yako pale pale kutokana na kazi ngumu walizonazo za kufuatilia habari hususan vijijini.

Ja, wizara ina mikakati gani ya kuwafanya maafisa hao watekeleze majukumu yao kikamilifu kwa kuwapatia vyombo vya usafiri?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 56 kama ifuatavyo:-

Ni kweli miaka ya zamani Maafisa Habari wa Wilaya na Mikoa na Maafisa Uhusiano wa Mikoa walikuwa wakipatiwa vyombo vya usafiri kama vile pikipiki kutoka Wizara ya Habari pale Madaraka Mikoani ilipoanzishwa rasmi, kwa ajili ya kusaidia Madaraka Mikoani, lakini haikuwa ni wajibu wetu.

Mhe. Spika, kusita kutoa msaada wa kuwapatia vyombo hivyo ni kweli kumewafanya waandishi hao kufanyakazi zao ipasavyo, lakini hii ni kutokana na ufinyu wa bajeti.

Hata hivyo, wizara hivi sasa imo mbioni kuandika miradi mbali mbali kwa ajili ya kuwasilisha kwa wahisani, ili wizara ifaidike, waandishi na wakiwemo hao Maafisa wa Uhusiano wa Mikoani nao wafaidike na miradi hiyo.

Aidha wizara yenyewe itaangalia uwezekano wa kusaidia pale bajeti itakaporuhusu kwa mwakani.

Nam. 22

Wananchi wa Kojani Kutopatiwa Msaada

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiwahimiza sana wananchi kujikusanya pamoja, ili waweze kuunganisha nguvu zao katika kujiletea maendeleo, ili iwe rahisi kwa serikali kuwasaidia na kuwawezesha katika kufikia malengo hayo. Wananchi wa Jimbo la Kojani ambao zaidi ya asilimia 70 ni wavuvi tayari wameshatimiza jukumu hilo la kujikusanya kupitia vikundi na *NGO's* mbali mbali.

Lakini licha ya maombi mengi waliyoyatuma Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini na wizara kwa ujumla, hasi sasa hakuna hata ishara ya mafanikio achilia mbali mafanikio yenyewe.

(a) Kuna sababu ipi ya msingi inayofanya hadi leo wananchi hawa hawajasaidiwa kama wanavyosaidiwa wenzao, masharti yaliyotakiwa?

(b) Je, wizara yako ina mpango gani katika kuwawezesha wavuvi kiuchumi?

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Nakushukuru Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Tangu kuanzishwa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi hakuna kikundi kimoja si cha Kojani wala eneo jengine ambacho kimepatiwa vifaa vya uvuvi na wizara yangu.

Mwelekeo mpya wa wizara yangu sio kutoa misaada ya vifaa vya uvuvi, bali ni kutafuta mitaji kupitia wawekezaji ambao wavuvi watakopeshwa vifaa vya uvuvi kwa misingi dhamana madhubuti ya urejeshaji wa mitaji hiyo.

(b) Mara baada ya mazungumzo yetu na Wawekezaji wa Sekta ya Uvuvi yatakapokamilika, basi Wavuvi wa Kojani pamoja na maeneo mengine watakaokuwa tayari kwa kushirikiana na wizara yangu pamoja na wizara inayohusika na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, basi nao watawezeshwa kiuchumi.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Waziri kwa sababu Wavuvi wa Kojani wanavulia boti ambazo zinabeba watu 40 mpaka 50.

Je, katika kuwawezesha wavuvi kuna mpango gani au zana gani katika wizara yako ambazo utawasaidia kupitia boti zao hizo?

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba Wavuvi wa Kojani wanavua kwa pamoja, yaani wavuvi wengi wanaingia kwenye boti moja na sisi tunaelewa kuwa ndio uvuvi wanaovua na kimsingi hatuupingi.

Kwa hivyo, mitaji itakayopatikana itawawezesha Wavuvi wa Kojani kutafuta vyombo vya aina hiyo. Hivyo, si tatizo kwamba wanavua wavuvi wengi katika chombo kimoja.

Jambo la msingi ni kuwa wao wenyewe watakapokuwa tayari na kipindi si kirefu tukijaaliwa, basi watakuwa na uwezo wa kutafuta vyombo vya aina hiyo ambavyo vinaweza kuvua kwa kuingiza wavuvi wengi kwa pamoja.

Nam. 26

Kupatiwa Vifaa vya Kisasa

Mhe. Mjumbe, aliyeuliza swali ameliondoa.

Nam. 93

Wanafunzi wa Zanzibar Wanaopata Mikopo ya Elimu ya Juu wa Tanzania

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

Tunaipongeza serikali kwa kusikia kilio cha wananchi wa Zanzibar kuhusu umuhimu wa serikali kuwasomesha na kuwaendeleza kielimu wananchi wake na miongoni mwa matokeo yake mazuri ni pamoja na kuanzishwa kwa Bodi ya Mkopo wa Elimu ya Juu wa Zanzibar huku Mkopo wa Elimu ya Juu wa Tanzania.

Hata hivyo, kwa kila miaka ikizidi kwenda, idadi ya wanafunzi wa Zanzibar wanaopata mkopo katika Bodi ya Mkopo wa Elimu ya Juu wa Tanzania inapungua kwa kasi kubwa.

Itakumbukwa kwamba kwa mwaka wa 2011/2012, wanafunzi 48 tu wa Chuo Kikuu cha Zanziabr (*Zanzibar University*) wamepatiwa mkopo. Wanafunzi 34 wa *Education* kupitia *Central Admission System* ndio waliopata mkopo kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*), huku wanafunzi 30 tu wa *Education* wamepata mkopo huo katika Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani.

(a) Je, serikali haioni kwamba kupungua kwa idadi ya wanafunzi wanaopata mkopo wa Elimu ya Juu wa Tanzania, kunadhoofisha maendeleo ya Elimu kwa wanafunzi wetu wa Zanzibar.

(b) Je, serikali haioni kwamba kupungua huko kunasababishwa na mawazo ya kuikandamiza Zanzibar kwa kisingizio cha kuwa na Bodi yake ya Elimu ya Juu kwa wanafunzi wa Zanzibar pekee.

(c) Kwa kuwa mkopo unaotolewa na Bodi ya Elimu ya Juu ya Tanzania ni haki ya Watanzania wote. Je, serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha idadi ya Wazanzibari wanaopata mkopo huo inaongezeka kila mwaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 93 lenye vifungu (a), (b) na (c).

Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Napenda kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kuwepo kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania na kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar hivi karibuni, kutasaidia sana serikali zetu mbili kuweza kutoa mikopo mingi zaidi kwa wanafunzi wa Taasisi ya Elimu ya Juu, hatimaye kufanikiwa kuwasomesha na kuwaendeleza kielimu wananchi wetu wengi zaidi.

Vile vile ni kweli kwamba kwa mwaka huu idadi ya wanafunzi wa Zanzibar waliokubaliwa kupatiwa mikopo ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania kusoma katika vyuo vyetu vitatu vilivyoko Zanzibar imepungua sana.

Kwa mfano, katika mwaka 2010/2011 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Chukwani kati ya wanafunzi 337 walioomba mkopo, wanafunzi 283 walipatiwa mkopo huo ikiwa ni sawa na asilimia 84 ya waombaji wote. Kwa mwaka 2011/2012 kati ya wanafunzi 356 walioomba mkopo, waombaji 30 tu, ndio waliokubaliwa kupata mkopo ikiwa ni sawa na asilimia 8.4 ya waombaji wote.

Kwa upande wa Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*) wanafunzi 31 tu, ndio waliopatiwa mkopo katika mwaka 2011/2012 kati ya waombaji 293 sawa na asilimia 10.5 ya waombaji wote. Kwa mwaka 2010/2011 wanafunzi 211 wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar walipatiwa mikopo na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania.

Hivyo, kupungua huko kwa idadi ya wanafunzi wa Zanzibar wanaosoma katika Vyuo Vikuu vilivyopo Zanzibar kunatokana na ongezeko kubwa la waombaji wa mikopo kwa Tanzania nzima na hivyo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania kulazimisha kuweka vigezo vipya katika kuchagua wanafunzi wanaostahiki kupewa mikopo hiyo.

Pia ni kweli kwamba kwa mwaka huu, idadi ya wanafunzi wa Zanzibar waliokubaliwa kupatiwa mikopo na Bodi ya mikopo ya Elimu ya Juu ya Tanzania kusoma katika vyuo vikuu vitatu vilivyopo Zanzibar imepungua sana. Kupungua huko kumetokana na ongezeko kubwa la waombaji wa mikopo kwa Tanzania nzima na hivyo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Tanzania kulazimika kuweka vigezo vipya katika kuchagua wanafunzi wanaostahiki kupatiwa mikopo. Vigezo hivyo vimezingatia kwa kiasi kikubwa fani za kipaumbele kwa maendeleo ya Taifa ni kama vile Ualimu, Sayansi za Tiba, Sayansi za Kilimo na Sayansi za Mifugo.

Pia vigezo vimelenga katika kuwapatia mikopo wanafunzi wenye mahitaji maalumu pamoja na wale waliofaulu vizuri katika masomo yao ya Kidato cha sita na wenye sifa linganifu katika fani za ualimu wa Sayansi na Hesabu. Pamoja na kutumiwa vigezo hivyo, baadhi ya wanafunzi wenye sifa na wanaochukua programu za ualimu wamekosa mikopo. Katika ziara ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi wa Tanzania aliyoifanya hapa Zanzibar tarehe 9 Oktoba hadi tarehe 12 Oktoba 2011, tulifanya mazungumzo yeye pamoja na ujumbe wake akiwemo Ofisa kutoka Bodi ya Mikopo na ametuarifu kuwa idadi ya Wanafunzi wa Zanzibar waliopitishwa kupata mikopo imeongezeka katika uteuzi wa hatua ya pili *(second selection).* Pia, ameahidi kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Tanzania itapitia upya majina ya wanafunzi waliokosa mikopo ili kubaini kasoro zote zilijitokeza. Baada ya maelezo hayo napenda kujibu kama hvi ifuatavyo:

a) Ni kweli kuwa kupungua kwa idadi ya wafanafunzi Zanzibar watakaopatiwa mikopo ya elimu ya juu kupitia bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Tanzania kwa ajili ya kusoma katika vyuo vikuu vilivyopo Zanzibar, kutasababisha wanafunzi wengi kushindwa kujiunga na vyuo hivyo hali hiyo itarejesha nyuma juhudi zetu za kuwasomesha vijana wengi zaidi katika vyuo vikuu vya hapa nyumbani. Hata hivyo mbali na wanafunzi walioomba mkopo kwa ajili ya kusoma vyuo vikuu vilivyopo Zanzibar pia wapo wanafuzi wengi wa Zanzibar walioomba mikopo ya kusoma katika vyuo vikuu vilivyopo Tanzania Bara na baadhi yao wamefanikiwa kupata mikopo hiyo.

   Kupungua kwa idadi ya wanafunzi Zanzibar waliokubaliwa kupatiwa mikopo na elimu ya juu ya mikopo ya Tanzania hakuna mahusiano kabisa na kuanzisha kwa bodi ya mikopo ya elimu ya juu Zanzibar, kwani mfuko wa elimu wa juu Zanzibar ulikuwepo kabla ya kuanzishwa kwa bodi ya mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar, kuwepo kwake hakuathiri upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Zanzibar kupitia bodi ya Mikopo ya Tanzania.

Utaratibu wa utoaji wa mikopo ya elimu ya juu ni kwa njia ya ushindani na kwa kuangalia vigezo vilivyowekwa ninawashauri waombaji wetu kufanya vizuri zaidi katika masomo, ili waweze kuwa na sifa za juu na pika kuomba masomo katika maeneo yaliyopewa kipaumbele. Utaratibu uliopo sasa hautengi nafasi kwa ajili ya eneo la mwanafunzi analotoka, Wizara yangu itaendelea kufanya mazungumzo na viongozi wetu wa Tanzania Bara kuona ni jinsi gani kutapatikana uwiano wa utoaji wa mikopo ya wanafunzi kwa vyuo vikuu mbali mbali vya Tanzania.
Hata hivyo napenda kukiri kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanoomba mikopo ya elimu ya juu kunatoa changamoto kubwa kwetu kwani fedha zinazotengwa ni chache na hazitoshi kuwahudumia wanafunzi wote, hasa kutonana na wanafunzi wengi kupata sifa za kujiunga na taasisi ya Elimu ya Juu. Wizara yangu nakusudia kufanya mazungumza na vyombo vya fedha kama vile mabenki na mfuko wa hifadhi ya Jamii ili kuangalia uwezekano kwa kufanya kazi kuweza kupata mikopo ya kuwasomesha wanafunzi wetu wa elimu ya juu.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu marefu na mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

a) Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kuwa pamoja na kuteua wafanafunzi wenye sifa au fani za kipaumbele, wapo bado waliobaki na wenye sifa kama hizo kuendelea kuwaacha hao ni kuleta yale matabaka yaliyokuweko tokea mwaka 1964 kabla ya Mapinduzi.

a. Serikali ikiunganisha taasisi zake inatarajia kupata mafanikio bora, Je, Wizara yako ina sababu gani za msingi za kuunganisha mfuko wa elimu ya juu na kuwa bodi ya elimu ya juu wakati wananchi wengi mpaka sasa wanaona hauna mafanikio yoyote.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nataka nikubaliane na Mhe. Muhammed Said Mohammed kuwa mbali na vipaumbele ambavyo vimewekwa basi kuna wanafunzi wetu ambao wamekosa na walikuwa na sifa hizo, na hili nilikiri kwenye suala langu mama.

Lakini kama serikali inataka kuweka matabaka sidhani serikali ina nia ya kuweka matabaka lakini nia yake ni kutoa kipaumbele kwa zile nafasi ambazo tunaona tuna wakosefu wa wataalam ndani ya nchi.

Lakini suala lake namba (b) Sheria Nam. 6 ya mwaka 2001 ya mfuko wa Elimu ya Juu ilifutwa na tukaleta sheria mpya Nam. 3 ya mwaka 2011 hazikuunganishwa, lakini ilifutwa ile sheria na nia ya kufuta sheria hii ni kuunda chombo kipya ambacho tumekipa nguvu ndani ya sheria hii. Moja ya nguvu ambayo tumekipa chombo hiki kwa sababu tumeona ni wazi katika bajeti ambayo tunapitisha katika Baraza letu hili haitoshelezi, kwa hivyo tukawapa nguvu ya kutafuta mkopo pesa popote ambapo wanaweza kupata.

Lakini pia tumeipa nguvu bodi hii kuna wanafunzi wengi ambao walikopeshwa na huu mfuko karibu bilioni saba zimetumika na mpaka leo pesa hivi hazijarudi, kwa hivyo

tuliipa nguvu bodi hii ili iandae utaratibu mpya wa kuweza kurudisha hizi pesa ambazo zimekopwa ili kuweza kusaidia wanafunzi wetu.

Mhe. Salim Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu ya Jamuri ya Muungano wa Tanzania inafanya shughuli zake kupitia kodi za wananchi wa nchi hii, kwa kuwa hakuna fomula ya utoaji wa mikopo hii baina ya Bara na Zanzibar jambo ambalo linapelekea Wazanzibari kupewa kwa uchache sana mkopo huu wa elimu.

a) Je, kwa kufanya hivyo Mhe. Waziri si kuwadhulumu Wazanzibari.
b) Atakubaliana nami Mhe. Waziri kwamba kuwanyima Wazanzibari mikopo ya Elimu ya Juu si kwenda kinyume na haki ya msingi ya Wazanzibari aidha hii atakubaliana nami vile vile ni moja katika kero kubwa za muungano jambo ambalo Wazanzibari wengi wanashindwa sasa kuendelea na Muungano huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Utaratibu wa utoaji wa mikopo ya Elimu ya Juu ni wa ushindani kulinganisha na vigezo ambavyo viliwekwa na bodi husika.

Suala la kusema kwamba kuna upendeleo au Zanzibar tunanyimwa haki sioni kama ni suala la msingi, kwa sababu mkopo hatupewi pesa sisi kutia kwenye bodi yetu ya Zanzibar, mkopo huu unaomba kwa mujibu wa waombaji wanavyoomba na sifa za muombaji. Kwa hivyo kama ambavyo nilizungumza ni wanafunzi wetu wa Zanzibar kuzidisha bidii ili waende sambamba na zile sifa na viwango vilivyowekwa kwa kuweza kupata mkopo huu wa Elimu ya Juu Tanzania.

Halafu suala jengine Mhe. Mjumbe kauliza kwamba wanafunzi kunyimwa mkopo huu si kwenda kinyume na haki za binaadam. Nafahamu kwamba elimu ni jambo la lazima kwa mwanadamu kupata lakini kunyimwa mkopo huu si kwenda kinyume na haki za binaadamu kwa sababu waombaji wamewekewa masharti na lazima haya masharti wayafuate.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Tunajua kwamba watoto wetu siku hizi wanavyosoma wanasoma katika mazingira magumu na wengi ambao hawapati kuendelea hujisaidia kwa fedha zao wenyewe, mpaka ikafika pahala ambapo serikali huwa inaweka mpango wa kuwakopesha na kwa mujibu wa maneno ya Mhe. Waziri ni kuwa sasa wanawakopesha watu kwa kutoa vipaumbele, maana yake ni kwa wale wote ambao sifa zao ni za kutosheleza hapa Zanzibar huwa wanakoseshwa mikopo hiyo na hawapewi taarifa kabla kuwa msichukue masomo haya hampati mkopo.

a) Haoni kuwa hivi sasa tayari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeshapotea mwelekeo halisi wa kuendeleza watu wetu kielimu na huu unaofanywa hivi sasa ni ubaguzi wa dhahiri, kuwa masomo haya tutawapa mkopo na masomo haya hatuwapi wakati wote walikwenda kwa gharama mpaka wakafika pale walipofika.

b) Kuna watoto ambao wanasoma hilo wanalolitaka lakini karatasi zao za maombi zilipotea katika mafaili yao mpaka zikaonekana juzi na hawakupata mkopo hawa je, atunawafanya vipi.

Mhe.Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ni kweli nilisema kwamba serikali mara hii tumeweka kipaubele ni ya serikali yetu ya Zanzibar ni kusomesha wanafunzi wote wenye uwezo wa kusoma, lakini tulieka kipaumbele kwa sababu mahitaji ya wanafunzi wetu kutaka kwenda elimu ya juu ni wengi, fedha ambazo tulipitishiwa kwenye bajeti kwa mwaka huu zilikuwa hazitoshi kulingana na mahitaji ambayo yaliwekwa.

Bila ya shaka Mhe. Spika, kwenye wanafunzi (6,103) uwezo watu kwa mwaka huu ni kusomesha wanafunzi (191) sasa hapa ni lazima kuwe na sifa za ziada ambazo utaweza kuchambua ili kuwapata ambao unaweza kuwapa mkopo kwa mujibu wa fedha ambazo tunazo.

Lakini kama nilivyosema kama tunatarajia mwakani kama mambo yatakuwa kinyume na hivi kwa sababu bodi imeanza kazi August, tu mapema, tumeipa mikono na miguu ya kutafuta kwa hivyo bila ya shaka mwakani itakuwa na uwezo mkubwa na atutaweza kuchukua wanafunzi wengi zaidi kuliko hivi sasa, inawezekana hivi vipaumbele vinaweza kubadilika, kwa sababu vipaumbele vinatokana na mahitaji ya nchi. Kwa hivyo mwakani tukawa na mahitaji mengine yaliyokuwa sio haya tuliyoyatoa mwaka huu.

Lakini suala la pili alilouliza Mheshimi Mwakilishi nikiri kwamba sikuwa na taarifa kwamba kuna maombi ambayo wameleta waombaji wetu na yakapotea kwenye bodi yetu, sikuwa na taarifa hiyo Mhe. Spika.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mimi Mheshimiwa nimesema yapo maombi hayo na Mhe. Waziri anasema hana taarifa, kutokuwa na taarifa ni kwamba haina maana kuwa hayapo ikiwa yapo sijapata jibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Sikumkatalia Mheshimiwa Mjumbe nilisema sikuwa na taarifa kwamba kuna suala hilo, madhali kanipa taarifa yeye ni kiongozi na mimi kiongozi nitahakikisha ninafuatilia katika Wizara yangu na kuona ni namna gani tunaweza kuwasaaidi hao wanafunzi, bado Mheshimiwa hatujamaliza mchakato tuko katika kuchagua wanafunzi, kwa hivyo kama wana sifa wanaweza kupita kwenye hii ngwe ya pili.

UCHAGUZI WA MJUMBE MMOJA WA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR KUINGIA KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Mhe. Spika: tumsikilize *returning officer* wetu ambae ni Katiba wa Baraza la Wawakilishi.

Katibu Baraza la Wawakilishi: Ahsante sana Mhe. Spika, katika ajenda hii ya uchaguzi naomba nitoe taarifa mbili kwanza.

Taarifa ya Kwanza :

Jana tarehe 25 Oktobar, 2011 nilipokea barua kutoka kwa mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi katika Baraza la Wawakilishi Mhe. Salmin Awadh Salmin Muwakilishi wa Jimbo la Magomeni, inayoniarifu kwamba Chama cha Mapinduzi kinaleta mbele ya Baraza la Wawakilishi majina matatu ya Wagombea kwa ajili ya nafasi hii. Na hayo yamefanyika kwa mujibu wa kanuni ya 143 kanuni 1 ya kwanza ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi ya toleo la mwaka 2011.

Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba wagombea ambao wameletwa na Chama cha mapinduzi kwa ajili ya nafasi hii ni Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando), Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) na Mhe. Mussa Ali Hassan.

Pia naomba nitoe taarifa kwamba tumeorodhesha majina haya kwa kufuata *Alphabet* isionekane labda pengine hivi au hivi utaratibu uliofuata ni kufuata *alphabet*, kwa hivyo *alphabet* ya kwanza ndio waliokuja kwanza huo ndio utaratibu tuliofuata katika kura zetu.

Taarifa ya Pili: Taarifa ya pili ni kwamba utaratibu tutakaotumia katika uchaguzi utakuwa kama ifutavyo:-

Hatua ya kwanza: Mhe. Spika, atamwita kila mgombea atoe maelezo yake mafupi na aombe kura kwa wajumbe aulizwe masuali yasiyozidi matatu kama yapo.

Hatua ya pili : Itakuwa ya upigaji kura.

Hatua ya Tatu: Uteuzi wa Mawakala kwa kila mgombe kwa ajili ya kuhesabu kura.

Hatua ya Nne: Ziezi lenyewe la kuhesabu kura ambalo zoezi hili litasimamiwa na Katibu wa Baraza pamoja na wasaidizi wake wawili, Ndugu Mdungi Makeme Mdungu na Ndugu Saleh Ali Saleh. Kwa hivyo timu ya watu watatu kwa kushirikiana na mawakala watakaoteuliwa na wagombea ndio watashughulikia katika zoezi la kuhesabu kura.

Hatua ya Mwisho: Kuja kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa heshima na taazima naomba kutoa taarifa hizo mbili na huo ndio utaratibu tutakaotumia katika uchaguzi, karibu sana ili tuanze hatua ya kwanza ya kuwaita wagombea kwa utaraibu huo ili watoe maelezo mafupi na kuomba kura kwa wajumbe na ikiwezekana kama yapo masuali waulizwe masuali yasiyozidi matatu. Karibu sana Mhe. Spika.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, baraza letu linaongozwa na kanuni lakini pia linaongozwa na mwenendo jinsi tunavyoendesha shughuli zetu, nafasi tunayokusudia kuijaza ni nafasi ambayo tayari ilishapigiwa kura katika baraza hili katika kikao chake cha mkutano wa mwanzo kabisa baada ya uchaguzi. Nakumbuka wakati ule tulipochagua hakukuwa na kujieleza wala kuuliza masuala tuliambiwa majina yamewasilishwa hapa sote tunaelewana tukapiga kura mimi nilikuwa mmoja katika wagombea wa chama changu.

Sasa naona utaratibu unaoelezwa leo unaanzisha urataibu mpya nilikuwa naomba muongozo wako tunafuata taratibu gani katika chaguzi kama hizi Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Hebu tupe utaratibu wa kanuni halafu nitaelezea kilichotokea kipindi kile.

Katibu Bazara la Wawakilishi: Mhe. Spika, ni kwamba Mhe. Ismail Jussa Ladhu amechanganya chaguzi mbili, uchaguzi wa kwanza ulikuwa uchaguzi wa Spika, ambapo ndipo hatukuruhusu wagombea kujieleza na hatukuruhusu kwa sababu wakati ule kanuni zilikuwa bado hazijarekebishwa. Sasa hivi kanuni zinazohusiana na uchaguzi wa Spika zimerekebishwa ambazo zinaruhusu wagombea wa Spika, kujieleza.

Wanachosema hapa ni kwamba ziliwekwa kanuni kando na wagombe wote kwa pamoja wakajieleza na haukuwa uchaguzi wa wabunge tu, nakumbuka hata uchaguzi wa wajumbe wa kuingia katika tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi na wajumbe walioingia katika tume, walipewa nafasi ya kujieleza katika ukumbi huu kwa hivyo hiyo tayari ilikuwa imeshawekwa katika chaguzi zilizopita na ambayo Mhe. Spika, ameeleza kwamba tuifuate katika uchaguzi huu.

Mhe. Spika: mimi nafikiri kilichotendeka kipindi kilichopita ni kwamba kweli kabisa wakati wa uchaguzi wa Spika, kanuni zilikuwa ziko kimya juu ya suala la kujieleza au

laa, baadae ikatoka haja kwamba ingekuwa ni vyema wanaoomba nafasi basi wajieleze kanuni tukarekebisha ikawa inaonyesha hivyo. Lakini katika chaguzi zilizopita tukasema kwamba hawa tunafahamiana wala hakuna haja ya kujieleza nakumbuka hii kanuni tukaijenga kando na tukakubaliana kwamba sasa tuendelee moja kwa moja, lakini kimsingi kwa kufuata kanuni ni kwamba wajieleze.

Sasa kama na hawa tunasema wasijieleze iyo inabidi tutenge kanuni kando, sihivyo kikanuni inabidi wajieleze.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kwanza nikiangalia kanuni ya 142 na 143 ndizo ambazo zinaongoza taratibu za uchaguzi wa wawakilishi wa baraza wanaoingia katika bunge la Jamhuri. Katika kanuni ya 143 kanuni ndogo ya 4 inasema. Katibu atawasilisha orodha ya wagombea mbele ya baraza kwa kupigiwa kura ambayo itakuwa kama atakavyoamuru Spika, hapana kanuni inayozungumzia wagombea kujieleza na kuulizwa masuala.

Sasa bila shaka katika hilo nataka niseme kabisa naheshimu kabisa mamlaka ya kiti chako na ukituamuru kama ilivyosemwa hapa kwamba wajieleze na tuulize masuala ni sawa, lakini nasema mimi ninachozungumzia kwa sababu ni vizuri kwa baraza kama hili likawa na *cassistent* katika utaratibu wake. Kama nilivyosema wakati ule mimi nilikuwa mmoja kati ya waliogombea kwenye chama changu na nakumbuka tulikuwa watu watatu kwa kuwa kulikuwa hakuna maelekezo ikakubaliwa kwamba tunaeleweka na tupigiwe kura.

Nafasi ambazo nakumbuka tuliweka utaratibu wa kujieleza na kuuliza masuala ulikuwa ni uchaguzi wa Naibu Spika, uchaguzi wa wenyeviti wa Baraza na kwa upande wa Tume ya Bajeti nadhani kila mmoja alikuwa ameshatoa wajumbe wake kwa hivyo hata kuwapigia kura hatukuwapigia hapa. Lakini wale wa Naibu Spika, na Mwenyekiti ndio tuliowapigia kura walijieleza na kuulizwa masuala, lakini kwa nafasi za wawakilishi wanaokwenda katika bunge hatukuwapa nafasi ya kujieleza wala kuulizwa masuala.

Sasa kwa chombo kama hichi ni vizuri tuwe na mpangilio unaoeleweka kwamba leo tunfanya hivi na kesho kutwa tunafanya vyengine hapa, kwa sababu inaweza kutokezea hapa Mhe. Jaku, kesho katika nafasi hii basi akajiuzulu tutakujataka kupiga kura tena hapa, kwa hivyo ni vizuri tukaelewana tunafanya utaratibu huo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Katibu Baraza la Wawakilishi: Kama utaratibu uliotumika wa mwanzo ni kwamba wagombea hawakupewa nafasi ya kujieleza mimi nadhani basi tusitie katika urataibu huo kwa hivyo twende moja kwa moja kwenye uchaaguzi.

Mhe. Spika: Kwa hivyo tunaendelea bila ya kuwaita wajumbe na kujieleza na kama kuna masuali tusiwaulize tunaacha hiyo ni sawa.

Kaatibu Baraza la Wawakilishi: Naomba wasaidizi wanipe idadi ya wajumbe waliopo kwenye Ukumbi wapo wajumbe wangapi.

Naomba kutoa taarifa kwamba wajumbe waliopo kwenye ukumbi ni sabiini na mbili (72).

Mhe. Spika: Labda kuna mambo tuyatende kabla ya kuanza zoezi la kuanza uchaguzi, ili wajumbe wathibitishe kwamba ndani ya masanduku hamna kura iliyotangulizwa hebu yalete masanduku. Fungua na uoneshe Waheshimiwa Wajumbe

Katibu wa Baraza la Wawakilishi: Waheshimiwa Wajumbe sanduku lipo tupu, kwa hivyo tunalifunga kwa lakiri, ili kuhakikisha kwamba tuanze zoezi la uchaguzi.

Waheshimiwa Wajumbe sanduku tayari tumelifunga, kwa hivyo sasa tunaomba tugawe karatasi za kura.

Mhe. Spika: kabla ya kugawa karatasi hii ni kura ya siri. Hivi tunakubaliana tupige tulipo? Wajumbe wanasema wapigie kura huku.

UTARATIBU

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mimi nadhani Mhe. Spika, tujiridhishe na idadi ya watu 72. Kwa sababu nina wasi wasi sijui umetumika utaratibu gani wa kutuhesabu. Wasi wasi wangu asije akaongezeka mtu mmoja maana yake kura yetu ikawa imeharibika tukarudia tena. Kwa hivyo tujiridhishe kama kweli Wajumbe wote ni 72.

Mhe. Spika: Itabidi tuite majina. Tunaomba tuwe kimya ili kila mmoja asikie jina tuweze kuweka mahesabu yetu sawa sawa.

Katibu wa Baraza la Wawakilishi: Nitataja jina la kila mjumbe na aliyekuwepo atathibitisha kwamba yupo.

1. Mhe. Ali Abdalla Ali
2. Mhe. Moh'moud Mohammed Mussa
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi
5. Mhe. Dokta Mwinyihaji Makame Mwadini
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee
7. Mhe. Haji Omar Kheir
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed — Hayupo
10. Mhe. Abubakar Khamis Bakari
11. Mhe. Hamad Mosoud Hamad
12. Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban — Hayupo
13. Mhe. Juma Duni Haji
14. Mhe. Zainab Omar Mohammed
15. Mhe. Abdillahi Jihadi Hassan
16. Mhe. Ali Juma Shamuhuna
17. Mhe. Mansour Yussuf Himid — Hayupo

18. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
19. Mhe. Said Ali Mbarouk
20. Mhe. Harouna Ali Suleiman
21. Mhe. Suleiman Othman Nyanga Hayupo
22. Mhe. Haji Faki Shaali
23. Mhe. Machano Othman Said
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)
25. Mhe. Zahra Ali Hamad
26. Mhe. Sira Ubwa Mamboya
27. Mhe. Hindi Hamad Khamis
28. Mhe. Haji Mwadini Makame
29. Mhe. Thuwaibah Edington Kisasi
30. Mhe. Othman Masoud Othman
31. Mhe. Abdalla Juma Abdalla Hayupo
32. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
33. Mhe. Abdi Mossi Kombo
34. Mhe. Ali Mzee Ali
35. Mhe. Ali Salum Haji
36. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
37. Mhe. Asaa Othman Hamad Hayupo
38. Mhe. Asha Abdu Haji
39. Mhe. Asha Bakari Makame
40. Mhe. Ashura Sharif Ali Hayupo
41. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
42. Mhe. Farida Amour Mohammed
43. Mhe. Fatma Mbarouk Said
44. Mhe. Hamza Hassan Juma
45. Mhe. Hassan Hamad Omar
46. Mhe. Hijja Hassan Hija
47. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
48. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
49. Mhe. Kazija Khamis Kona
50. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
51. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)
52. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma
53. Mhe. Mohammed Haji Khalid
54. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
55. Mhe. Mohammed Said Mohammed
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
57. Mhe. Mussa Ali Hassan
58. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
59. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
60. Mhe. Nassor Salim Ali
61. Mhe. Omar Ali Shehe
62. Mhe. Panya Ali Abdalla
63. Mhe. Rashid Seif Suleiman

64. Mhe. Raya Suleiman Hamad
65. Mhe. Rufai Said Rufai
66. Mhe. Saleh Nassor Juma
67. Mhe. Salim Abdalla Hamad
68. Mhe. Salma Mohammed Ali
69. Mhe. Salma Mussa Bilal
70. Mhe. Salmin Awadh Salmin
71. Mhe. Salum Amour Mtondoo
72. Mhe. Shadiya Mohammed Suleiman
73. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Hayupo
74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan
75. Mhe. Subeit Khamis Faki
76. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
77. Mhe. Ussi Jecha Simai
78. Mhe. Viwe Hamis Abdallah
79. Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

Katibu wa Baraza la Wawakilishi: Kwa mujibu wa orodha hii wajumbe waliokuwemo ni 71. Mhe. Spika hapigi kura. Katiba inasema anayeongoza kiti akiwa Spika hana kura. Kifungu cha 83 cha Katiba.

Mhe. Spika: Wajumbe waliokuwepo ni 71. Katibu hatua inayofuata?

Katibu wa Baraza la Wawakilishi: Hatua inayofuata ni karatasi za kupiga kura kupewa kila mjumbe kwa ajili ya zoezi la upigaji kura.

Mhe. Spika: Utatoa karasi za kupigia kura kwa mujibu wa orodha. Taratibu ya upigaji kura ni kwamba unamchagua mjumbe mmoja tu ndiye unayempigia kura.

OMBI

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mheshimiwa nimekuletea barua kama mbili hapo, kuwa mimi nina maiti kitandani. Naomba kura yangu nipige ili niwahi Mheshimiwa na mimi ndio mzishi mwenyewe. Kwa hivyo naomba kura yangu nipige niondoke.

Katibu wa Baraza la Wawakilishi: Kila mpiga kura atatakiwa aje mwenyewe. Yatatajwa majina kutokana na orodha ya tuliyonayo ya majina ya wajumbe mmoja mmoja ataelekea kwenye kisanduku cha kupigia kura na kupiga kura yake na kuingiza ndani ya kisanduku.

(Ilitajwa orodha ya majina na mjumbe mmoja mmoja alitoka kwenye nafasi yake na kuelekea kwenye meza ya Makatibu mezani kwa kwendakuchukua karatasi ya kupigia kura na kupiga kura)

Katibu wa Baraza: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Waheshimiwa Wajumbe wote 71 wameshapiga kura zao. Hatua inayofuata ni uteuzi wa Mawakala kwa kila mgombea kwa ajili ya kuhesabu kura.

Mhe. Spika: Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) amekwenda mwenyewe kuhesabu kura, Mhe. Mohammed Said Mohammed mekwenda Mhe. Ali Salim Haji Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani na Mhe. Mussa Ali Hassan amekwenda mwenyewe.

Waheshimiwa Wajumbe kwa huruma kubwa sana na kwa sababu zoezi hili ni kubwa na zito, Jimbo la hapa tulipo Jimbo Kiembesamaki wanasema kama kutatokea tatizo lolote katika zoezi hili *ambulance* ya jimbo ipo na iko tayari kutoa huduma na mimi nitachangia mafuta kama ikibidi.

Pia Waheshimiwa Wajumbe ningesema kitu kimoja kwamba tusitawanyike kwa sababu kuna uwezekano wale wawili wa kwanza ambao mmoja tunamuhitaji wakafungana, kwa hiyo kuna uwezekano kura hizi kuweza kurejea wakati wowote kwa wawili wa kwanza watakaofungana ikitokezea hivyo.

HOJA BINAFSI

KUHUSU MKOPO WA ELIMU YA JUU

Mhe Spika, kwa mara nyengine tena nakushukuru kunipa nafasi hii kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuleta hoja yangu binafsi kuhusu suala zima la mkopo wa elimu ya juu.

Mhe. Spika, naomba kuleta hoja binafsi kuhusu suala zito linaloikabili nchi yetu kuhusu wanafunzi walioomba mkopo wa kuendelea namasomo ya elimu ya juu katika vyuo mbali mbali hapa Tanzania.

Mhe Spika, chini ya kanuni ya 27 (i) (m), 27(3); 47(2); 48(1); na 49(1) ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2011) naliomba Baraza lako tukufu la Wawakilishi kuijadili hoja hii na pia kuiomba Serikali yetu kuijadili na hatimae kuikubali pamoja na miongozo mengine itakayotolewa na wajumbe wako Baraza hili na baadae kuipitisha.

Mhe Spika, kwa mwaka huu wa 2011/2012 wanafunzi wote walioomba mkopo walikuwa ni 1,630 na waliofanikiwa kupata mkopo huo ni 300 tu. Kwa hiyo ina maana ni wanafunzi 1,300 hao ndio waliokosa kupata mkopo na hapo utakuwa ndio mwisho wao kimasomo kwani takriban karibu wote hali zao ni mbaya kimaisha na si rahisi kuweza kuendelea na masomo kwa mwaka huu. Ambapo karibu bilioni mbili na nusu zinahitajika kuweza kutatua tatizo hili.

Mhe Spika, hii inaweza kupelekea kuwavunja moyo vijana wetu hao ambao ndio wasomi wetu tunaotegemea kuja kujenga taifa letu hapo baadae. Lakini isitoshe hii itapelekea na vijana wetu walioko mashuleni wanaotarajia kufanya mitihani yao na kuingia katika masomo ya elimu ya juu kuvunjika moyo wa kusoma kwani hawajui na wao hatma yao itakuwaje

Mhe Spika, ni lazima tukubali sote kwamba elimu ndio msingi wa maisha na taifa letu linategemewa kujengwa na vijana wenye elimu, kwani historia inatuambia kwamba mataifa yote yameendelea kutokana na elimu, kwani mtu akiwa na elimu hata shughuli zake yeye mwenyewe binafsi basi ataziendesha vizuri kulinganisha na yule asiyekuwa na elimu.

Mhe Spika, ukiangalia vijana wengi hawa wamesoma katika mazingira magumu sana, wengi wao wazazi wao hawana elimu ya kutosha na pia hawana uwezo wa kifedha, ushahidi tosha wengi wa wanafunzi hawa hutufuata majumbani mwetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wengine wanakujia hata kwako wewe Mhe. Spika, wetu kuomba msaada ili kuweza kujikimu kwa mambo mbali mbali ya masomo ili wapate kuendelea na masomo yao. Sasa pamoja na jitihada yote hiyo wazazi wao wamehangaika vya kutosha, lakini baada ya kufaulu wanagonga ukuta dakika ya mwisho kukosa pesa kutokana na (UMASIKINI). Ama kweli umasikini mbaya, mtu anakosa haki yake ya msingi ya kupata elimu kwa kukosa pesa, kwani hata Mtume wetu Muhaammad (S.A.W) aya ya mwanzo aliyoteremshiwa KATIKA QUR-AN aliambiwa kwanza asome kabla ya jambo jingine hapa ndio tunapouona umuhimu wa elimu.

Kwa hivyo, sisi tukiwa kama ndio wazazi wa watoto hawa, lakini pia Mwenyezi Mungu akatupa sisi uongozi wa kuliongoza taifa hili basi ni lazima tukae tutafakari, tuumize vichwa vyetu na mwisho tukitoka hapa tuamue ni nini tutafanya ili kuweza kuwaokoa vijana wetu hawa ili waendelee na masomo yao ya elimu ya juu. Naamini Mhe Spika, humu ndani ya Baraza hili mna watu wazima wenye mawazo tofauti tena wenye upeo mkubwa wa mawazo, naamini kila mmoja akitoa mchango wake wa mawazo basi tutaweza kutoka na jawabu ambayo itawaokoa vijana wetu hao. Mhe Spika, vijana wetu hawa hivi sasa wameshagonga ukuta wamechanganyikiwa hawajui la kufanya si ajabu tukaja kusikia miongoni mwao amejinyonga, Mwenyezi Mungu atuepushie mbali hilo lisijekutokea.

Mhe Spika, hivi sasa sisi Zanzibar tuna upungufu mkubwa wa wataalam katika nyanja mbali mbali, isitoshe tumo ndani ya Muungano wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki na tuko katika mfumo mpya wa soko la pamoja biashara huria, kwa hiyo ni lazima tuache yote ili tusomeshe vijana wetu waweze kushindana katika soko kubwa huria la ajira ndani ya jumuia hii ya Afrika Mashariki. Jumuiya hii ambapo tangu zilikuwa nchi tatu hadi sasa tano na hivi karibuni tumeshasikia na Sudan ya Kusini na wao wanataka kujiunga kwa hiyo hatuna budi kuhakikisha kwamba kila fursa ya ya kuwasomesha vijana wetu basi tuitumie vizuri.

Mhe Spika, tunaishukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuanzisha ujenzi wa skuli za sekondari za kila Wilaya, lakini isitoshe kuanzisha vyuo vikuu hapa

Zanzibar na hivi sasa matunda yake tunayaona kila kukicha idadi ya wasomi inaongezeka hapa Zanzibar. Lakini tunafahamu kila maendeleo yana athari zake kwani tumeanzisha mashule mengi kuazia msingi, Sekondari na Vyuo na sasa changamoto yetu kubwa ni namna gani tutahakikisha kila Mzanzibari asome hadi ukomo wa uwezo wake.

Mhe Spika, mimi nimeamua kuleta hoja yangu hii sio kwa utashi wangu, lakini ni hisia kali zilizonijia kwani nilipata taarifa kwamba vijana hawa wanafanya vikao vya kuandaa kufanya maandamano kwenda katika Ofisi ya Makamo wa wa Pili wa Rais kuitaka Serikali kulitatua tatizo lao hilo. Baada ya kupata taarifa hiyo mimi niliwaomba wasitishe kwanza maandamano hayo na nikawaomba wanialike kwenye kikao chao hicho na walifanya hivyo. Mimi sikuona busara kwenda peke yangu nikawomba baadhi ya Wajumbe wenzangu wa Baraza lako tukufu tuongozane ili kwenda kuwasikiliza, baada ya kuwasikiliza, ukweli machozi yalikaribia kututoka, lakini tukasema kulia sio suluhisho. Suluhisho la hili ni kuleta hoja Barazani kuishauri Serikali ni nini cha kufanya kuwasaidia vijana wetu. Na kama nilivyosema hapo awali naamini ndani ya sakafu ya moyo wangu suluhisho ndani ya Baraza lako hili tukufu litapatikana.

Mhe Spika, tunashukuru baada ya kuwashauri kwanza wasitishe maandamano hayo na kutuachia sisi wawakilishi wao tuwasaidie kutafuta ufufmbuzi wao walikubaliana na sisi na wanatusikiliza viongozi wao tunafanyaje. Mhe Spika, kwa ruksa yako na wao leo tumewaalika ili kuja kutusikiliza wazee wao nini tutawafanyia kumaliza kiu yao hiyo ya masomo. Mhe. Spika, naamini kwa mashirikiano ya pamoja tukiweza kulitatua hili basi vijana wetu hawa watatuthamini sana na watakuwa watii sana kwa taifa lao na wataamini kwamba ni kweli taifa lao linawajali na watakujakuwa ni watumishi waaminifu sana kwa taifa letu hapo baadae, na pia watazidisha bidii na maarifa katika masomo yao, na sio wao tu bali hata wazazi wao na familia zao kwa jumla watatuthamini sana na kuona kuwa ni kweli wamechagua watu ambao wanaweza kukabiliana na changamoto za maisha zinazowakabili.

Mhe Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kushauri mambo haya yafuatay:-

1. Serikali iiweke wazi *account* yake ya Mfuko wa Elimu wa juu Zanzibar ili mtu au taasisi yeyote anayetaka kuchangia mfuko huo aweze kuchangie hata kama yuko nje ya nchi.

2. Serikali iandae *Fund Rising* na mgeni rasmi awe Mhe Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi au Makamo wake yeyote, kwa kuwaalika wafanya biashara wote wa Tanzania, wafanyabiashara wa Zanzibar na wenye asili ya Zanzibar, wawekezaji waliokuwepo Zanzibar na nje ya Zanzibar, Makampuni yaliyokuwepo Zanzibar na nje ya Zanzibar, Mashirika Mabalozi na hata watu binafsi pamoja na watanzania walioko nje ili kuchangia mfuko huo maalum wa elimu ya juu, itakayosimamiwa na na Serikali.

3. Kuliomba Barazalako tukufu liitake Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ipunguze shilingi milioni 400 kutoka katika mafungu ya safari za viongozi ambazo

zimetengwa kiasi (4. Bil) na fungu la marekebisho ya mishahara na kiasi mil 600, ambapo zilitengwa shilingi 19 Bil, ambapo jumla itakuwa ni bilioni moja.

4. Tunawaomba Wajumbe wote 50 wa Baraza la Wawakilishi wenye majimbo kupitia kwenye mfuko wao wa majimbo yao kuchangia milioni mbili mbili kila jimbo ambapo itakuwa ni milioni mia moja kwenye *account* hiyo. Na itakuwa ndio chanzo cha harambee hiyo.

5. Tunawaomba Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wote kuuchangia mfuko huo ili kuwachangia vijana wetu.

6. Serikali kushauriana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kuangalia kitaalam kama itawezekana nao kusaidia kuendeleza mfuko huo wa elimu ya juu.

7. Serekali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kuitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kuweka (*ratio*) asilimia yetu maalum ya mgao wa fedha za mkopo wa elimu ya juu kwa Zanzibar kwani kwa utaratibu unaotumika hivi sasa kuwachanganya wanafunzi wote wa Tanzania nzima sio sahihi, na kuna uwezekano ukatokea mwaka mmoja kwa hapa Zanzibar akapata mwanafunzi mmoja tu.

8. Kwa kuwa hakuna nia wala muelekeo wa Tanzania kujiunga na Jumuiya ya *OIC* basi tunaiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iiruhusu Zanzibar kujiunga na jumuiya hii, kwani moja ya faida ya kujinga na jumuia hiyo ni kufadhili wanafunzi kutoka nchi wanachama katika elimu ya juu. Kwani hivi sasa kuna wanafunzi kutoka nchi mbali mbali wanafadhiliwa na Jumuia hii ya Kiislam.

9. Mwisho kabisa kuiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwaruhusu wanafunzi walioomba Chuo cha Chwaka pamoja na vyuo vyengine vilivyokuwepo hapa Zanzibar kwani hivi sasa kuna agizo baada ya wiki tatu kama hawajamaliza malipo yao hawataruhusiwa kujiunga au kuondolewa Chuoni hapo.

Mhe Spika, kwa heshima kubwa naliomba baraza lako tukufu kuijadili hoja yangu hiyo na kuichangia kwa kadiri ya uwezo wenu na tuishauri ipasavyo Serikali yetu na baadae tuje na maamuzi ya pamoja kwa maslahi ya taifa letu. Naamini Serikali yetu ni sikivu na wanao uwezo mkubwa wa kufanya maamuzi mazito hasa linapotokea jambo zito kama hili. Na sisi tunaahidi kushirikiana na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kulifanikisha suala hili.

Mhe Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunisikiliza pamoja na wajumbe wote, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana hoja imeungwa mkono na iko tayari sasa kwa kujadiliwa.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba uniruhusu nianze kwa kumshukuru Mola wetu Mtukufu kwa kunijalia mimi na wewe pamoja na wajumbe uhai na afya tukawepo tena katika kikao hiki cha Baraza lako tukufu kujadili mambo mazito yanayogusa maslahi ya watu wetu na nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nikushukuru na wewe, nikushukuru na kukupongeza kwa kuruhusu hoja hii kuwasilishwa mbele ya Baraza lako tukufu. Mhe. Spika, sisi sote ni mashahidi kwamba chini ya uongozi wako, Baraza hili limekuwa likipiga hatua kila siku katika kukuza demokrasia na kuhakikisha linafanya kazi yake ya msingi ililoundiwa ambalo ni kusimamia uwajibikaji wa serikali na vyombo vyengine vya utendaji katika nchi yetu.

Mhe. Spika, si rahisi kwa nchi kama zetu ambazo zimetokana na mfumo wa chama kimoja na baadae kuingia katika mfumo wa vyama vingi katika kipindi cha miaka kama 19 iliyopita kuweza kupiga hatua kwa kasi ya namna hii, kwamba vyombo vyake vya maamuzi na vya wananchi kama hiki kufikia nafasi ya kutoa fursa kwa wajumbe binafsi kuleta hoja zao, tofauti na zile ambazo zinazoletwa na serikali. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nataka nikupongeze na kushukuru kwa hilo kwani ni imani yangu kwamba katika Baraza hili basi hii haitakuwa hoja ya kwanza kuiruhusu kutoka kwa *backbencher*s katika kutoa changamoto, kuibua hoja kwa yale mambo ambayo pengine hayakupata fursa ya kutosha kujadiliwa kupitia hoja za serikali. Kwa hivyo, nakushukuru sana Mhe. Spika, na naomba uendelee na utaratibu huo.

Mhe. Spika, nitakuwa sifanyi haki kama simpongezi kaka yangu Mhe. Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura kwa kuchukua hatua hii ya kuleta hoja hii binafsi. Mhe. Spika, wiki iliyopita Mhe. Hamza alitupigia simu baadhi yetu akitueleza hisia zake alizonazo na jinsi alivyoguswa na kilio cha ndugu zetu ambao waliomba mikopo wawaruhusu kuweza kujiendeleza na elimu ya juu, lakini kutokana na bajeti ilivyokuwa imekaa Wizara ya Elimu kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ikashindwa kuwapatia.

Mhe. Spika, tumeshauriana na baadhi yetu hatukuweza kufika katika mkutano ambao aliomba tukutane na wawakilishi wa wanafunzi hao, lakini wengine walikwenda kutuwakilisha. Lakini tulimuhakikishia Mhe. Hamza kwamba hatua aliyoichukua ni ya ubunifu na ni ya kizalendo na sisi tunamuunga mkono. Ndio maana hata katika maelezo ya hoja yake hii akasema kwamba hakwenda peke yake aliwachukua na wenzake. Mimi nasema mbali ya wale aliowachukua lakini kuna wengine alitushauri tukasema katika hili tuko pamoja na yeye. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nataka nimpongeze na kumuunga mkono sana Mhe. Hamza, na nadhani Mhe. Hamza ni mfano wa aina ya wawakilishi tunaowataka katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, sio tu kwa maana ya ule ubinifu, lakini pia katika kuoneshwa kukerwa na mambo ambayo yanawagusa wananchi. Mhe. Spika, katika siasa za huko tulikotoka tulikuwa na mikwaruzano mingi na pengine isingekuwa rahisi leo kwa mimi kusimama hapa nikammiminia sifa ninazommiminia Mhe. Hamza. Lakini tunashukuru chini ya uongozi wa majamadari wawili wa kisiasa katika nchi yetu Rais Mstaafu Mhe. Amani

Abeid Karume na Katibu Mkuu wa CUF Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad walituwekea muongozo uliobadilisha siasa za nchi yetu. Mhe. Spika, leo tunaweza kushirikiana kama hivi kujadili mambo yanayogusa nchi yetu.

Mhe. Spika, na wewe pia kwa uongozi wako, kwa hekima zako na busara zako historia haiwezi kukusahau kwa sababu ulisimamia kwa dhati na wakati mwengine sisi tulikuwa hatumo katika Baraza lako wakati ule, lakini mwengine tunashuhudia watu ambao hawakuwa na muono wa mbali kama uliokuwa nao wewe na wenzako walikuwa wakikulaumu. Lakini leo kila mmoja mwenye nadhari yake kamili na anayetazama maslahi ya nchi anaona faida iliyopatikana kwa kuwa na muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika Zanzibar na kuwa na maridhiano ya kisiasa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nasema nayataja haya kwa sababu yanatuwezesha leo kushirikiana na ndio maana nasema nampongeza Mhe. Hamza namuomba aendelee na uzalendo wake, na hii tabia au mwenendo ulioujenga wa kushirikiana katika mambo yanayogusa maslahi ya nchi yetu tuendeleze tukiamini kwamba katika nchi kama yetu hatuna kitu chengine cha kukitegemea kama kwanza hatukujenga umoja na mshikamano miongoni mwetu. Mhe. Spika, nasema nampongeza sana Mhe. Hamza kwa hatua yake hii.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo labda niseme namuomba Mhe. Hamza kwamba asivunjike moyo kutokana na mikwaruzano anayoipata katika harakati za kisiasa. Lakini hii iwe kama ni moto uliotumika kupitisha dhahabu ikaichonga dhahabu ikazidi kung'ara, namuomba asimamie maslahi ya watu wetu na tuendelee kushirikiana hasa katika lile ambalo mimi na yeye mara nyingi tunafanana sana katika kuitetea na kuihami Zanzibar na maslahi yake pamoja na watu wake. Mhe. Spika, sasa niende katika hoja baada ya utangulizi huo.

Mhe. Spika, Baraza lako hili lina dhima muhimu sana katika nchi yetu, na katika hili naomba uniruhusu nifanye marejeo ya Katiba yetu sura ya pili kuhusu malengo na maamuru muhimu ya sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Spika, sura hii inafungwa na maelezo kwamba vifungu vilivyomo katika sura hii huwezi kuvitilia nguvu ya kisheria katika Mahakama. Kwa sababu hatujafika nchi yetu kuwa na kiwango cha maendeleo cha kuweza kuhakikisha yote, kwa hivyo ikafika pahala mtu akaona hajayapata haya akenda Mahakamani akaidai serikali.

Lakini sura hii fupi pamoja na kwamba haiwezi kutiliwa nguvu vifungu vyake katika Mahakama, lakini imetoa muongozo muhimu sana kwamba kadri inavyowezekana basi tuweze kutumia nafasi zetu kutekeleza yale mambo ambayo yanagusa maslahi ya nchi na watu wake. Nitaitumia sana sura hii katika mchango wangu, lakini naomba nianze kwa kuwaomba wajumbe tukipitie kifungu cha 10 (h) cha Katiba yetu katika sehemu hii ya malengo na maamuru muhimu ya Sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kifungu hicho kinasema:

“Vyeo vyote vya madaraka ni dhamana na vipo kwa faida na manufaa ya umma na wale wote walio na madaraka watawajibika ama moja kwa moja kwa umma au kupitia kwa vyombo vya uwakilishi”.
Mhe. Spika, katika hivyo vyombo vya kusimamia madaraka chombo kikubwa sana katika Zanzibar ni chombo hiki cha wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo, Mhe. Spika, sisi tupo hapa moja katika malengo yetu ni kwa faida na manufaa ya umma, na kama hivyo ndivyo basi tunapaswa sasa tulinde maslahi na manufaa ya umma huo.

Mhe. Spika, hoja aliyoileta Mhe. Hamza inaturejeshea mpira kwetu kwamba wawakilishi wa wananchi tunafanya nini kusimamia hayo manufaa ya umma kama chombo cha madaraka. Muda si mrefu sana Mhe. Spika, Baraza hili lilipitisha bajeti ya serikali miezi kama miwili iliyopita na siamini kama Mhe. Hamza ameleta hoja hii ili kuiparaganya mipango ya serikali ambayo tumeipitisha katika Baraza hili. Lakini naamini kaongozwa na hisia za ubinadamu na uzalendo kwamba katika hali ya dharura basi Baraza hili lina nafasi ya kupendekeza kwa serikali na serikali sikivu kama ilivyo serikali yetu ina nafasi ya kuyapokea na kuyafanyia kazi yale mapendekezo uliyoyatoa ili kuzingatia hayo manufaa ya umma ambayo yametajwa na Katiba yetu.

Mhe. Spika, jamii yoyote katika ulimwengu wa leo na hata huko nyuma haiwezi kuendelea kama haikutoa msukumo unaopaswa kwa elimu, na moja katika mambo ya mapema sana kufanya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuona inatoa nafasi hiyo ya kila mtu mwenye uwezo wa kujiendeleza kielimu aweze kujiendeleza na kufika ukomo wa uwezo wake. Mhe. Spika, katika ulimwengu wa leo elimu ya lazima kabla haitoshelezi kumfanya mtu kujiandaa na maisha yanayokuja, lakini hata kutoa mchango wake muhimu katika kujenga nchi yake.

Mhe. Spika, nchi leo zinajengwa na wataalamu huko tunakokwenda tukitembeza bakuli zilizotoa nafasi muhimu sana kwa elimu kusomesha watu wake, leo watu wake wanasaidia kuzijenga nchi zao. Kwa hivyo, Mhe. Spika, sisi kutokana na umasikini wetu tunashindwa kuhakikisha kwamba kila mtu ambaye anaomba nafasi kama hizi za masomo ya elimu ya juu aweze kupata nafasi hiyo kutoka serikalini.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme natambua kabisa msimamo wa Wizara ya Elimu kwamba kwa fungu walilowekewa wasingeweza kusomesha zaidi ya wale ambao ilikuwa imewapokea. Lakini hoja ya Mhe. Hamza imekuja na mapendekezo katika kusisitiza umuhimu wa elimu kwamba tutazame kwengine, na katika hilo Mhe. Spika, mimi nataka niyaunge mkono mapendekezo aliyoyatoa katika ukurasa wa 4 wa hoja yake na baadhi ya marekebisho nayapendekeza, kama alivyotuomba sisi wenyewe tufanye marekebisho.

Mhe. Spika, sina tatizo pendekezo la hoja ya kwanza kutoka katika mafungu ya safari za viongozi ambazo zimetengwa na ambazo kwa jumla ziko kama shilingi bilioni nne na fungu la marekebisho ya mishahara na kiasi shilingi 600 milioni ambazo zimetengwa shilingi 19 bilioni.

Sasa mimi wasi wasi wangu sina hakika kwa sababu wakati ule tulipoomba maelezo hapa hatukupewa maelezo ya kina katika bajeti, kwamba hizi shilingi 19 bilioni kiasi gani

zinatosheleza au zina ziada au lilikuwa ni fungu la ziada tu lililowekwa ambalo unaweza ukatenga hizo shilingi 600 milioni. Lakini nataka kuunga mkono kimsingi kupunguzwa shilingi 400 milioni kutoka katika fungu la safari za viongozi ili kuwapatia sehemu ya mikopo wanafunzi hawa ambao wamekosa.

Kama nilivyosema, kama Waziri wa Fedha ataturidhisha kwamba inawezekana kupunguza shilingi 600 milioni katika fungu la marekebisho ya mishahara na bado mishahara ikaendelea kulipwa kama ilivyokuwabliwa basi sina tatizo, lakini kama patakuwa na matatizo Mhe. Spika, mimi naomba tufanye marekebisho pia kifungu cha nne.

Katika kifungu hiki Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan amependekeza wajumbe wote 50 wa Baraza la Wawakilishi wenye majimbo kupitia Mfuko wao wa Majimbo kuchangia shilingi milioni mbili mbili, kila jimbo ambapo itakuwa ni shilingi 100 milioni kwenye *account* hiyo.

Mhe. Spika, mimi nina mawazo tofauti katika hili, nakumbuka katika fungu lile zilitengwa shilingi 600 milioni ambapo ilikuwa kila jimbo litengewe shilingi milioni kumi na shilingi 100 milioni nadhani ilikuwa inahusu mambo ya utawala na mambo mengine katika mfuko ule. Sasa mimi nataka kupendekeza Baraza lako likubali kufanya marekebisho katika hoja nambari nne kwamba fedha zote shilingi 600 milioni zilizotengwa katika ule uliokusudiwa uwe Mfuko wa Jimbo basi ziingizwe pamoja na hizo shilingi 400 milioni za kutengwa kutoka katika fungu la safari ziwahudumie wanafunzi wetu hawa.

Kwa nini nasema hivyo Mhe. Spika? Hata ukitupa shilingi milioni kumi kumi sisi hakuna maendeleo makubwa yatakayopatikana katika majimbo yetu, lakini hakuna maendeleo makubwa ya kuwapa watu wa majimbo yetu kama elimu. Hao wanaoomba waliokosa sina hakika na hii takwimu iliyotolewa na serikali, lakini kama takwimu sahihi hawa 1,300 basi hao Mhe. Spika, wanatoka Mji Mkongwe, Kwamtipura, Makunduchi, Tumbatu, Micheweni, Chake Chake, wanatoka katika majimbo yetu. Kwahivyo, ndio nikasema tukubali kwa mwaka huu fedha hizi zote ziende katika kuwasaidia wanafunzi hawa ambao wamekosa pesa.

Mhe. Spika, ikiwa pendekezo ninalolitoa la marekebisho litapita shilingi 600 milioni zile zitafidia ikiwa kule zilipwe mishahara zile ambazo zilipendekezwa zitolewe katika fungu la marekebisho ya mishahara.

Mhe. Spika, haya mengine ya kuomba Makatibu Wakuu wachangie na wao sina tatizo nalo na hasa kwa sababu miongoni mwao tumewawekea mafungu makubwa makubwa katika sheria ya utumishi wa umma nadhani watatoa sehemu ya fedha zao ili na wao wasaidie vijana wetu.

Lakini pia naomba nipendekeze marekebisho katika pendekezo nambari 7. Katika pendekezo hili Mhe. Hamza amependekeza Serikali yetu ya Zanzibar kuitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweka *ratio* mimi niseme uwiano wa asilimia yetu

maalum ya mgao wa fedha za mkopo wa elimu ya juu kwa Zanzibar, kwani kwa utaratibu unaotumika hivi sasa kuwachanganya wanafunzi wote wa Tanzania nzima sio sahihi na kuna uwezekano ukatokea mwaka mmoja akapata mwanafunzi mmoja tu kutoka Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nina pendekeoz tofauti kidogo, mimi nawaomba Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi na katika hili nawaomba wote mawaziri na sisi *back benchers* tupendekeze hapa kwamba kuitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipeleke maamuzi ya Baraza la Wawakilishi kwamba lile fungu ambalo Zanzibar inapaswa kupewa katika fedha za kusaidia elimu ya juu ambazo kwa mujibu wa katiba hii nyongeza ya kwanza ni suala la Muungano mpaka hii leo, haidhuru sisi wengine tunahoji uhalali wake, lakini mpaka leo liko hivyo. Mimi napendekeza sio tu kutenga *ratio* halafu *ratio* hiyo ikasimamiwa na Bodi ya Mkopo wa Elimu ya Juu ya Tanzania. Nasema ile *ratio* yao itakayoamuliwa iletwe isimamiwe na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ndugu zetu wa damu hawa mara nyingi tunawaamini katika mambo mengi sana, lakini unapokuja utekelezaji kuna matatizo. Juzi Mhe. Waziri Ardhi, Makaazi, Mjai na Nishati kawakuna Wazanzibari wengi hapa, kawakuna hasa na yeye bahati nzuri ni mkunaji mzuri sana yanapokuja masuala ya Muungano na kusimamia haki za Zanzibar kwa yale aliyowaambia *APRM* hapa. Sasa tunaona kila pahala kuna matatizo.

Mhe. Spika, katika hili badala ya kusema tufanye *ratio* tu watutengee, watuletee hapa ili Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar hili fungu wanalopaswa kupewa walisimamie wao kuona wanafunzi wetu wanafidiwa.

Mhe. Spika, mwisho kabisa hoja ya nane (8) hoja hii imeshakuwa tena inatuchosha kurejea kila siku. Hoja hii Mhe. Hamza amependekeza kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano iruhusu Zanzibar kujiunga na *OIC* ili tufaidike na fursa zake zikiwemo za kusaidia wanafunzi wetu kuweza kupata kufidiwa gharama za masomo.

Mhe. Spika, nilikuwa nazungumza na kijana mmoja alikuwa anasoma Uganda, amenambia Uganda kama unavyojua kwa sababu kuna watu wengine wanapenda kulifanya suala hili kama ni suala la kidini. Uganda Waisilamu ni wachache sana kwa asilimia, lakini Uganda imejiunga na *OIC* leo vijana wa Uganda wanapata manufaa, wanafunzi wao wanalipiwa masomo na *OIC* katika misaada wanayopewa. Sisi tumejikosesha kwa sababu tu ndugu zetu wa damu wanaotupenda sana wanaona fedha hizi zitakuja kutudhuru huku Zanzibar hawataki zije.

Mhe. Spika, mimi nasema imefika pahala katika suala hili tuamue na najua siwezi kusimama hapa kwa jazba nikasema Baraza hili liamue tukajiunge na *OIC* kwa sababu najua *OIC* sasa hivi haitatupokea. Lakini Mhe. Spika, mimi nadhani imefika pahala kama Serikali ya Muungano haiwezi kuona kila lenye maslahi ya Zanzibar wanaliridhia kwa maslahi ya upande huo mmoja wa Muungano, basi kama hawatutaki watwambie tutoke.

Mhe. Spika, vitimbi kama hivi vilipelekea Singapore na Malaysia shirikisho lao lilivunjia kwa sababu kama hizi, alisema Mhe. Waziri wa Ardhi hapa, kwamba upande mmoja hautaki kuona maslahi ya upande mwengine. Sasa nasema mimi katika hili imefika pahala tuwapelekee hoja watuamulie wanataka au hawataki. Kwa sababu kubembeleza tumeshabembeleza sana, tunabembeleza kuhusu *OIC*, kuhusu Mafuta, kuhusu kodi zinazotozwa mara mbili, tutabembeleza mpaka lini Mhe. Spika na sisi tuna haki sawa katika Muungano huu. Mara nyingi tunayowaambia kama wametuchoka ni mzigo kwao watutue.

Mhe. Spika, jana nilikuwa nazungumza na mwanafunzi mmoja nikamwamia hili kwamba mimi naamini uchumi wa Zanzibar ungekuwa mzuri tusingekuwa tunagombana katika kugawana hiki kidogo tulichokuwanacho. Kwa sababu suala la mikopo ya elimu ya juu sasa hivi imekuwa fitina kubwa kwa viongozi katika nchi, kwa sababu wananchi wanatuona labda hatuwajali. Sasa mimi naamini mkombozi yupo na ukombozi anao Mhe. Waziri wa Ardhi suala la mafuta. Kasema juzi kwamba hatuwezi kusubiri mpaka mjadala wa katiba umalizike mwaka 2014 ndio tuweze kuja kuruhusiwa kama suala la mafuta limo kwenye Muungano au hayamo.

Mhe. Spika, katika Baraza lako tuliamua sisi na tulipendekeza, kwamba kama wao wana uzito kupeleka hoja kuliondoa suala la mafuta katika mambo ya Muungano basi Wajumbe wa Baraza hili wawatake Wabunge wa Zanzibar walioko pale wapeleke hoja binafsi kama alivyoleta Mhe. Hamza leo suala hili liondolewe. Wabunge wa Zanzibar wana nafasi ya kupeleka hoja binafsi na haina kazi kubwa Mhe. Spika, ni kupeleka marekebisho kwamba katika nyongeza ya kwanza iliyoko katika ukurasa wa 128 wa Katiba kifungu Nam. 15 kinachosema maliasili ya mafuta pamoja na mafuta yasiochujwa ya *motor car* na mafuta aina ya *petrol* na aina nyenginezo za mafuta, bidhaa na gesi asilia basi kifungu hiki kiondolewe, kikishaondolewa itawezekana Zanzibar kusimamia suala kwamba litakuwa si suala tena la Muungano.

Kwa hivyo, nasema Mhe. Spika, hebu tuwatake wakati tunajadili leo hatima ya wanafunzi wetu ambao wanakosa haki zao nyengine kutokana na Muungano, basi hebu katika hili hebu tuliamue leo Mhe. Spika, kwamba tuwatake wabunge wetu wapeleke hoja binafsi kwa niaba ya Wazanzibari ikiwa Serikali ya Muungano inaburura miguu katika hili haitaki kupeleka marekebisho haya. Bahati mbaya kuna baadhi ya viongozi wetu inaonekana haya hayawagusi, tunapenda kuupaka mafuta Muungano tukausifu lakini katika mambo haya yanayotukwaza tunashindwa kuyasimamia na kuyatetea.

Mhe. Spika, bahati nzuri Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ambaye ni kiongozi wa shughuli za serikali katika Baraza hili yeye ni Mbunge katika Bunge la Muungano. Kwa hivyo, hebu tumuombe yeye akawasimamie wabune wenzetu waliko pale ili wapeleke hoja binafsi hii kwenye Bunge halafu hapa wakikataa kufanya marekebisho tutajua hapo tena kwa wazi wazi kwamba Muungano huu upo kwa maslahi ya Zanzibar au maslahi ya Tanganyika dhidi ya Zanziabar.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii na marekebisho niliyoyatoa na nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wote na katika hilo naomba tusigawanyike

Mhe. Spika, mawaziri kwa niaba ya serikali na sisi *back bnchers* katika hilo tuungane mkono kufanya marekebisho aliyopendekeza Mhe. Hamza ili tupate fedha hizi. Hazitatosheleza nimesema bajeti inahitaji kama shilingi bilioni mbili na nusu, lakini tukipata shilingi bilioni 1.1 angalau tukiwapa nusu tukienda tukiomba kila mmoja na kingine tukawaambia wazazi wao wakatafute kwa njia nyengi kama wanavyofanya wengine itakuwa tumeonesha nia ya kuwasaidia. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naiunga mkono hoja hii kwa asilimia moja na nawaomba wajumbe wengine wote tuunge mkono. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nikapata nafasi ya kuchangia hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura.

Mhe. Spika, mimi kwana nimpongeze sana Mhe. Hamza kwa hatua yake hii ya kuwasilisha hoja binafsi inayohusiana na suala zima la mikopo ya Bodi ya Elimu ya Juu kwa ujumla. Na kwa nini nikampongeza? Kwa sababu suala la mikopo ya elimu ya juu Zanzibar ni suala kubwa na ni muhimu. Kwa hivyo, nikiwa kama ni Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Magomeni na wanafunzi wenye sifa ambao wana asilimia kubwa katika jimbo langu wamekuwa kila wakati wakiulizia juu ya jambo hili. Sina budi kumpongeza na kumshukuru na mimi nitoe mchango na hisia zangu juu ya jambo hili.

Kwa kweli suala la wanafunzi 1,500 kukosa mkopo wa elimu ya juu kwa mwaka huu ni suala zito nathubutu kusema kwamba hili ni janga. Na kwa nini Mhe. Spika, nikasema ni janga? Ikiwa mwaka huu wa fedha wa 2011/2012 au mwaka wa masomo wanafunzi 1,500 wanakosa nafasi ya kupata mikopo ya elimu ya juu maana yake watashindwa kuendelea na masomo yao na ukizingatia kwamba wazazi wao hawana uwezo wa kuwasomesha. Je, kama mwaka huu idadi kama hiyo iko mitaani mwakani tutakuwa na idadi ya kiasi gani au kiwango kitakuwaje, tutegemee kiwango kama hicho au zaidi ya hicho kitakuwepo hapa kisiwani petu Zanzibar. Kwa hivyo, ni lazima serikali pamoja na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutafakari jambo hilo, tulitafutie ufumbuzi mapema katika kipindi hiki ili mwakani tunakokwenda basi serikali au wananchi wasiwe na mzigo mkubwa katika jambo hili.

Mhe. Spika, serikali imetenga shilingi bilioni nne katika bajeti hii kwa ajili ya mikopo ya watoto wetu wanaofaulu elimu ya juu, fedha ambazo kwa asilimia mia moja zote zimekwenda katika kuwalipia wale ambao tayari wako vyuoni. Kwa sababu tuna watoto wengi ambao tayari wako vyuoni wanasoma. Kwa hivyo, fedha hizi zitakidhi haja kwa wale wanafunzi ambao sasa hivi wako vyuoni, kwa maana hiyo, hata hao watoto 187 ambao tumewachukua mwaka huu basi na wao hali yao itakuwa si ya kuridhisha. Kwa maana hiyo, hii ni *challenge* kubwa sana kwa serikali juu ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya watoto wetu.

Katika bajeti hii ya elimu suala moja ambalo nililiangalia ni juu ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Katika kipindi kilichopita au mwaka wa fedha uliopita serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni tatu na mwaka huu imeongeza

shilingi bilioni moja, kwa jumla shilingi bilioni nne. Lakini kwa kweli hiyo bilioni moja iliyoongezwa ni fedha ambazo tayari zilikuwa zimetengewa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Wao wenyewe Wizara ya Elimu wakajipunguza katika mafungu yao ili angalau itimie shilingi bilioni moja ziwe shilingi bilioni nne, na wao wenyewe Wizara ya Elimu bila ya kufanya hivyo hata kiwango hicho cha fedha kisingeweza kufika.

Lakini sasa tuangalie wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mwaka jana bajeti yao ya Mfuko wa Elimu ya Juu walitenga shilingi 56 bilioni, lakini mwaka huu wa fedha wa 2011/2012 jumla ya shilingi 300 bilioni wametenga kwa ajili ya wanafunzi wa Mfuko wa Elimu ya Juu. Hebu tuangalie ni kwa kiasi gani cha fedha kilichoongezwa katika bajeti yao?

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ni lazima serikali wakati wa kupanga vipaumbele iweke umuhimu wa bajeti ya watoto wetu, ni lazima vipaumbele viangaliwe katika maeneo muhimu. Suala la kuwapatia elimu watoto wetu wanaosoma ni muhimu na kwa sababu bila ya taifa lenye watoto waliosoma maendeleo hayawezi kupatikana. Tupunguze baadhi ya mafungu yetu lakini serikali ni lazima itenge bajeti ya kutosha.

Mhe. Spika, hoja ambazo Mhe. Mwakilishi amezieleza mbele yetu mimi naziunga mkono na hii hoja nambari 3 ambayo Mhe. Mjumbe ameieleza ya kupunguza shilingi 400 milioni kutoka katika mafungu ya safari kwenye wizara mbali mbali hili nalo naliunga mkono ili kuwaokoa watoto wetu. Lakini hoja aliyowasilisha Mhe. Ismail Jussa Ladhu ya kutumika fedha za maendeleo ya majimbo zilizotengwa shilingi bilioni mia tano na kumi, Mhe. Jussa kasema shilingi 600 milioni lakini ni shilingi milioni 510 zilizotengwa zote tuzielekeze katika kuwasomesha watoto wetu katika Mfuko wa Elimu ya Juu. Mimi nakubaliana nalo kwa asilimia mia moja hakuna ubishi.

Lakini hii ni *challenge* katika bajeti ijayo. Tuna kasoro hapa ya shilingi 2.5 bilioni ili kukidhi haja ya watoto wetu. Kwa hivyo, hii ni *challenge* kwa serikali, kwa Wizara ya Fedha katika bajeti ijayo. Wakati wa bajeti ijayo Mwenyezi Mungu akitujalia Waheshimiwa Wajumbe tuangalie sana bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kuwapa mikopo watoto wetu, bajeti iliyotengwa kwa ajili wa Mfuko wa Elimu ya Juu, tuitupie macho sana, tuiangalie sana na kwa sababu hapa ndipo penye tatizo.

Kwa hivyo. Mhe. Spika, maelezo mengi yameelezwa na sisi kama wawakilishi wa wananchi ambao tunaguswa ni wajibu wetu kuunga mkono hoja hii ili watoto wetu hawa wasije wakavunjika moyo kama mtoa hoja alivyoeleza ili waendelee kusoma na serikali iwape nguvu wasomeshwe.

Lakini jengine kwa Wizara ya Elimu. Wizara ya Elimu wakati wanapotoa vipaumbele, vipaumbele wanavyovihitaji ni lazima wavitangaze ili wananchi, wazee wa wananchi na wanafunzi wenyewe waelewe kwamba sasa hivi serikali ina kipaumbele cha somo fulani na fulani na fulani. Na kwa sababu masomo yote haya huwa yanasomeshwa skuli kwa hivyo, watoto wana haja ya kuangalia na kuona nini kipaumbele cha serikali katika kipindi hiki. Vipaumbele hivi vinaweza kubadilika kila mwaka, lakini ni wajibu wa

wizara kuhakikisha kwamba wanafunzi au wazee wa wanafunzi wanafahamu nini vipaumbele.

Mwaka huu Mhe. Spika, kumetokea tatizo la watoto kutokuchukuliwa katika baadhi ya vyuo. Hili nalo tatizo, tunayo taasisi hapa wanaita wenyewe *TCU, TCU* wakati unapoomba maana yake unatakiwa uombe vyuo visivyopungua sita (6) na visivyozidi 8. kwa maana hiyo atakuwa anaomba katika vyuo mbali mbali, lakini inakuwa haipendezi kuona serikali au bodi inasema kwamba mtoto aliyepata *admission* katika chuo fulani serikali haiwezi kumdhamini au serikali iweke maelezo kabisa kwamba wanafunzi wanaoomba mkopo kupitia Bodi ya Elimu ya Juu wanatakiwa waombe chuo fulani, fulani na fulani. Serikali haitahusika na kuwafadhili watoto waliyoomba katika chuo fulani, fulani na fulani ili mwanafunzi aelewe mapema kwamba wanapoomba katika chuo fulani serikali itakuwa na uwezo wa kuwasaidia.

Lakini Mhe. Spika, kama baada ya wanafunzi kuomba baadae katika mchakato wa kuchuja halafu serikali inasema kwamba wanafunzi waliyoomba chuo fulani hatutowadhamini hiyo tutakuwa hatuwatendei haki watoto wetu na wakati huo wanakuwa wameshaomba. Kwa hivyo, ni lazima Wizara ya Elimu ijipange vizuri katika jambo hili ili wanafunzi wapate nafasi ya kuelewa na wazee wa wanafunzi wapate nafasi ya kuelewa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naunga mkono hoja hii ni hoja ambayo imetimia na kwa kweli imetugusa na hili ni tatizo la kitaifa lazima serikali nayo i-*act.* Lakini pia mbali ya maeneo ambayo Mheshimiwa mtoa hoja ameyaeleza, serikali inaweza ikaeleza maeneo mengine, si lazima yaangaliwe haya. Kwa sababu serikali ndio yenye kibweta chetu, wao wanajua kwamba tukitoa fedha kwenye maeneo fulani serikali haitoathirika katika utekelezaji wake, lakini hili lazima lizingatiwe kuhakikisha kwamba watoto wote wenye sifa ambao wanahitaji kwenda katika kuendelea na masomo yao serikali inawawezesha ili wapate haki yao ya msingi ya kuendelea na masomo.

Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hoja na nimpongeze Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kuwasilisha hoja hii. Ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii na naomba nichangie hoja hii ya Mhe. Hamza Hassan kwa upeo ninaofahamu. Lakini kabla ya kuchangia hoja hii nataka nikupongeze wewe kama Mhe. Ismail Jussa alivyosema. Mimi nimekuwa nikisema kwamba kuna haja ya kumuandaa Mzanzibari mwengine mwenye sifa angalau nusu za kuwa Spika wa baadae hapa Zanzibar. Kwa sababu Mhe. Spika, wewe ni mwanadamu na mwanadamu anazo hatua ambazo hupita, nina wasiwasi kwamba ukiondoka busara, mawazo na hekima ulizonazo zinaweza zikapotea sana Zanzibar. Kwa hivyo, mimi niseme wazi kwamba kuna haja Mhe. Spika, ukikaa ufikirie nani ataweza kuwa Spika hapa ili aweze kukumudu sifa zako kwa ajili ya kuendeleza Zanzibar hii.

Mhe. Spika, wafanyakazi wengi Zanzibar na duniani kote hasa wale wanaofanya kazi katika ofisi nyeti hupewa posho maalum kama *risk allowance*, hupewa maziwa kwa ajili

ya kutunza mioyo na *pressure* zao, sijui kama wewe unapewa chochote hapo lakini kwa kweli unafanya kazi ngumu sana. Unafanya kazi ngumu ambazo wakati mwengine kama si busara yako basi tungeshindwa kuamua. Kwa mfano hii hoja ya Mhe. Hamza Hassan hoja ambayo kwa kweli inahitaji upevu uliokuwanao kuweza kuisikiliza. Mimi nikupongeze na nimuombe Mwenyezi Mungu akujalie heri, naambiwa una safari hivi karibuni uende salama urudi salama *Inshaallah*.

Baada ya hoja hiyo ya kukushukuru niseme tukwamba mimi ni miongoni mwa watu ambao Mhe. Hamza alitualika kwenda kuona wanafunzi wetu kule *SUZA*. Tulikwenda si kwa ubabe, lakini tulikwenda kwa sababu ni sehemu ya viongozi wa Zanzibar, tukawasikiliza na tukawaomba kuwa kuna haja ya kusitisha mgomo na maandamano yao haraka sana. Tuliwaambia si kawaida sana kwa Serikali zetu za Afrika kusikiliza sauti za wananchi, mnaweza mkaandamana, mnaweza mkagoma nyinyi mkawa wakosa. Ingawa serikali pengine imewakosa au taifa limewaonea. Kwa busara kubwa ndugu zetu wale wakatufahamu na mimi niwapongeze sana kwamba wamesikiliza ushauri wa viongozi wao na waendelee kufanya hivyo, huo ndio uongozi bora, huo ndio uraia mwema na huo ndio uwajibikaji.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba mara kadhaa hapa Barazani Mhe. Waziri amekuwa akitwambia kuna zaidi ya shilingi bilioni saba ambazo wamekopeshwa Wazanzibari hawajalipa. Mimi nadhani hii isiwe sifa kwa serikali, hii ni dhahiri kwamba serikali inashindwa kusimamia mipango yake, hatuwezi tu kuwakopesha wananchi shilingi bilioni saba, pesa hizi ambazo zingewafaa wengine baadae tukajisifia kwamba tunawadai pesa nyingi.

Mimi nadhani serikali ijifunze kutokana na hili kwamba usimamizi mbovu wa idara tofauti ndio uliosababisha leo hii Wazanzibari wengi wakose mikopo. Laiti fedha hizi zingerejeshwa kwa wakati na kwa vile wengine ni waajiriwa wa serikali nadhani serikali isingekuwa na haja leo ya kuwadhalilisha watoto wetu wa Zanzibar kukosa mikopo hii.

Mhe. Spika, serikali lazima kupitia wizara husika wawe makini wanapotoa mikopo hii na lazima irejeshwe kwa ajili ya kuwafaa wengine. Hii ni fedha ya taifa, hii ni keki ya wananchi wote lazima haki kwa wote ipatikane kwa mujibu wa utaratibu wetu.

Jengine ambalo ningesema ni kwamba Zanzibar mwaka huu kama Mhe. Hamza alivyosema tumepokea maombi ya wanafunzi 1,630, wanafunzi 300 tu ndio waliofanikiwa kupata mkopo sawa na asilimia 18.9. Mhe. Spika, hatuwezi kujisifu kwamba tunasomesha wanafunzi wetu katika vyuo vikuu kwa asilimia 19, tukaacha asilimia nyengine 20 zikabaki mitaani.

Mhe. Spika, taifa hili ni sehemu ya dunia na taifa hili ni sehemu ya Afrika na leo tunaingia kwenye Afrika ya Mashariki kwenye ushindani mkubwa wa soko la ajira na ajira maana yake ni elimu. Mhe. Spika, serikali lazima kuanzia hapa ijifunze kwamba kama tunataka kuwekeza kwenye elimu maana yake tuweke mfumo mzuri wa fedha, tuweke fungu kubwa kwa ajili ya Wazanzibari kupata elimu. Wazanzibari wanahitaji kusoma, Wazanzibari wanahitaji maendeleo na maendeleo hayaji bila ya elimu.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba hoja binafsi ya Mhe. Hamza Hassan ni hoja sahihi, halali na kwa kweli wawakilishi wote nawaomba sana tuiunge mkono kwa ajili ya kuwawezesha Wazanzibari. Mhe. Spika, takwimu hii ya wanafunzi 300 ni sawa sawa na wastani wa wanafunzi 26 kwa wastani wa majimbo 50, hakuna jimbo ambalo limekosa wanafunzi 26 ambao hawakupata kuingia vyuo vikuu. Mhe. Spika, hivi ninavyokuambia zipo taarifa kwamba Wazanzibari leo wako Morogoro wanalala Misikitini, baada ya kukosa fedha za kujihudumia huduma za malazi ni aibu sio sifa ni hatari kubwa. Kwa hivyo, ikiwa Wazanzibari leo wake kwa waume wako Morogoro wanalala Misikitini kama vile wale tablihi sio sifa Mhe. Spika, ni lazima tuone kwamba hawa ni watoto wetu, taifa hili lilipinduliwa kwa ajili yao, tuwasaidie wapate elimu. Sisi wengine tumefikia hapa ni lazima na wao wafike hapa na wasonge mbele ili keshokutwa wawe viongozi wa taifa hili.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba hoja hii ya Mhe. Hamza Hassan ni hoja sahihi, ni lazima tukubaliane nayo na serikali ikubali hoja hii. Kama atatokezea mchawi leo itakuwa ni maajabu makubwa. Kama atatokezea mtu akasema hoja hii haina maana kwa ajili ya kuleta elimu kwa kweli mimi nitashangaa.

Mhe. Spika, niseme kwamba kabla ya hoja hii kuja Wazanzibari walikuwa wakilalamika kwamba Zanzibar hakuna uwazi. Mhe. Spika, uwazi kwenye uongozi ndio silaha pekee ambayo inawafanya wananchi wawe watiifu. Ikiwa Zanzibar tunatenga fedha za walipa kodi, fedha hii inatumiwa bila ya uwazi, sio haki kabisa.

Mhe. Spika, ziko taarifa zinasema kwamba fedha ambazo zimetolewa kwa mikopo wala hazikuwagusa wanyonge. Fedha hizi kama hazikuwagusa wanyonge basi Wazanzibari wataendelea kulalamika. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ni lazima kuwe na uwazi kwenye kutoa mikopo hii ambayo ni mikopo ya wananchi wote.

Mhe. Spika, hoja ya Mhe. Waziri mara nyingi amekuwa akituambia kwamba kipaumbele ni sayansi. Lakini wapo wanafunzi ambao sio wa sayansi na wanapewa mikopo hii na kuna wanafunzi ambao ni wa sayansi na wanasifa nzuri wameachwa, hii sio taratibu nzuri, sio nidhamu, sio utawala bora na wala sio haki.

Mhe. Spika, mimi nasema tu kwamba ni changamoto ya kamati yangu, pengine muda ujao Mhe. Waziri atupatie orodha ya wanafunzi wote waliopatiwa mikopo mwaka huu, ili tumjuwe nani Mzanzibari masikini aliyesaidiwa. Inawezekana Wazanzibari matajiri ndio waliopata mikopo hii. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba sana kwamba uwazi ni jambo muhimu sana.

Mhe. Spika, nasema tu kwamba hoja ya Mhe. Hamza Hassan ya mwanzo mpaka ya tisa, mimi naiunga mkono sana. Nasema kwamba kifungu nambari 4 Mhe. Hamza alipendekeza kwamba tutowe milioni 2, kwenye fungu la maendeleo la mfuko wa Jimbo. Mimi nasema kwamba maendeleo hayaji bila ya elimu, niungane na Mhe. Ismail Jussa, niungane na Mhe. Salmin Awadh kwamba fedha zote za fungu hili milioni 600 zitolewe

kwa ndugu zetu Wazanzibari waende wakasome, hakuna maendeleo ambayo yatapatikana bila ya elimu.

Mhe. Spika, fedha hizi milioni 600 kwa wastani wa milioni 10 kila jimbo tufanye nini. Hivi leo kila mwakilishi hapa ana zaidi ya wanafunzi 30 ambao anawafadhili, mshahara wenyewe Mhe. Spika, unaujua. Kwa hivyo, fedha hizi za mfuko wa jimbo ziingizwe haraka sana na nina wasi wasi mimi tukisema hivi basi Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wanaweza kusema basi tusiingize, fedha hizi ziingizwe ni haki yetu na zikiingizwa ziingizwe kwa wanafunzi wote na zigaiwe kwa usawa bila ya upendeleo.

Katika suala hili Mhe. Spika, bodi ya mikopo Zanzibar tafadhalini sana muwe na uwazi. Baada ya kutumia fedha mtupatie ripoti ya kwamba nani kapata na nani hakupata, kwa sababu nina wasi wasi mnatumia vibaya. Mhe. Spika, mkaguzi na PAC fedha hizo wazikaguwe, kwa sababu tukiwacha hivi hivi tu fedha hizi ukitoa wafadhili wakichangia inaweza ikaingia kwenye mkono wa mtu ambaye kwa kweli sio haki.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba fungu hili lipelekwe kwa wanafunzi wetu, lisikatwe na Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ni kaka yangu mimi najua ni msikivu, Mzanzibari halisi, mpendwa maendeleo na mtarajiwa wangu basi fedha hizi ziingizwe haraka sana ili wanafunzi wetu waokoke. Katika vyuo vya Chwaka, Tunguu, Chukwani, SUZA na Morogoro wanafunzi wanadhalilika jambo ambalo baadae wanaweza wakaamua kuingia kwenye masuala ya unga, masuala ya mapenzi jambo ambalo sio lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kumalizia niseme tu kwamba hoja hii ya Mhe. Hamza Hassan tuiunge mkono, mimi sioni cha kuongeza kitu chengine, ila fungu liongezwe lote la milioni 600 na serikali ikubali. Mara nyingi nimekuwa nikisema kwamba safari za nje zipunguzwe, labda huonekana kwa sababu mimi sijenda nje. Mhe. Spika, mimi sina haja ya kwenda nje, niko radhi watu wasitembee lakini watu wasome, hakuna maana Mhe. Spika, watu kutembea nje kila siku huku Wazanzibari wakiwa hawana elimu, nyie mtamalizika mtakufa, mkifa nyinyi mnayetembea nani ataongoza nchi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, fungu la safari za nje bilioni 4 zipunguzwe na sio milioni 400 zaidi ya milioni 600. Juzi tulikwenda China, China wamefanya mambo mazuri lakini kwa kutumia elimu, sasa elimu ile ya China ndio ije Zanzibar na itakuja Zanzibar bila ya elimu ya watoto wetu. Kwa hivyo, fungu la safari za nje lipunguzwe ili liingizwe kwenye fungu la elimu na lisimamiwe na ninapendekeza hasa ugavi wa fedha hizi na kamati yangu ishirikishwe, hatuwaamini bodi. Kwa nini mtoto wa Hija Hassan apewe mwanzo kuliko mtoto wa Ismail Jussa maskini, nasema wakati wa ugavi wa fedha hizi basi tushirikishwe, sisi ndio Wazanzibari, sisi ndio wananchi. Kwa hivyo, tuambiwe kwamba nani kapewa mkopo huu wazi wazi.

Mhe. Spika, sheria ambayo imepita juzi na mjumbe wa bodi ya mikopo ya elimu ya juu ambaye ni mwakilishi wa vyuo vikuu, Mhe. Waziri atuambie vikao vingapi amealikwa na kama amealikwa je, ni kwa ridhaa ya vyuo vikuu. Kwa hivyo, hakuna uwazi hapa. Mimi

nasema kwamba fedha ikipatikana igaiwe mbele ya macho ya viongozi wa Zanzibar wakiwemo wawakilishi.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja ya Mhe. Hamza Hassan ni sahihi na Mwenyezi Mungu akujaalie heri ahsante sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwanza namshukuru *Allah* kwa kutujaalia uzima na tukaweza kuzungumza hapa. Mhe. Spika, kabla sijasema maoni yangu kuhusu huu mswada wa hoja binafsi, naomba nitowe utangulizi ufuatao.

Mhe. Spika, nchi yoyote duniani inayotaka kuleta maendeleo au kujiletea maendeleo basi inaipa uzito elimu, lakini elimu haiachiwi ikenda tu yenyewe ni lazima wale wanaoshughulikia elimu na wanaowapokea wale wataalamu wakae pamoja na kupanga ni utaratibu gani utumike katika kuwasomesha vijana hao.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kila nchi huwa na vipaumbele vyake, kila nchi huwa na utaratibu wake wa kuona ni elimu ya aina gani itolewe. Sasa pamoja na kuzungumza kwamba tunataka kuwaendeleza vijana waende vyuo vikuu, lakini kuna haja pia ya kuchunguza je, elimu tunayotaka vijana wetu waendeleenayo itatusaidia huko mbele tunakokwenda. Hakuna pahala ambapo tumepakosea kidogo hata tukapata matatizo ya aina hii, hilo la mwanzo.

Lakini suala la pili, nchi nyingi zinazoendelea na zile zilizokwishaendelea, wanategemea sana takwimu kuwapatia hali kamili ya maendesho yao. Kama tatizo hili lingekuwa *projected* tokea mwanzo basi naamini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ingekosea padogo katika kupewa ile bajeti waliyoiomba au waliyopewa serikalini. Lakini kwa sababu Mhe. Spika, hatutumii takwimu, tunakwenda kimabavu basi ndio maana kukawa na pengo kubwa hilo. Maombi yaliyokwenda ni 1,800 lakini wanapata 300. Mimi naamini ingekuwa tunatumia takwimu basi tungekosea padogo tu, tungejitayarisha labda na 1,000 wakaleta 1,300 au 1,400, lakini kwa sababu hatutumii takwimu tunangojea, hatuna *projection*, vituo vyetu vitakwimu, vituo vyetu vya elimu havina *projection* ya mambo ndio yanakuja kutushtukizia tu, kwamba tunangojea fedha hii kumbe hali sivyo ilivyo.

Sasa kutokana na matatizo hayo Mhe. Spika, kwanza tufanye marekebisho katika maendesho ya shughuli zetu, hususan zinazohitaji fedha, lazima tuwe na mpango mkamilifu ambao utafanya *projection* ya matumizi halisi au mahitaji halisi tutakayo yahitaji.

La pili Mhe. Spika, mimi naunga mkono hoja ya Mhe. Hamza Hassan kuwa pafanywe mapitio mapya ya kuwaingiza zaidi ya wanafunzi hawa ambao waliopata, kwa sababu sasa hivi tunatibu hali ya dharura. Tuipeleke wizara ICU ili itiwe *drip* kidogo, halafu tuzuke na uhai angalau wa wanafunzi wengine 600 ili tupunguze pengo hilo.

Katika suala kama hili Mhe. Spika, mawizara yote yanakatwa fedha za kuendeleza utaalamu. Iko sheria ilipitishwa hapa na fedha zile zinakatwa na kwa sababu kuundwa

kwa mfuko huu wa bodi ya mikopo, umekata ule mfuko wa elimu ya juu kama ilivyotolewa leo. Sasa mfuko ule unatumika wapi na hii sasa ni *central board*. Kwa hivyo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali izidai fedha zake kule Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inazokata kule mawizarani. Siku nyingi tulikuwa tunawaambia lakini wanasema ndicho tulichopangiwa, mnacho kitu kimeshakatwa na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo daini fedha zenu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Ndio maana tukawapeleka ICU ili mjitetee.

Mhe. Spika, fedha zile zinaitwa *skill development fund.* Zile ni fedha za kuwaendeleza vijana wetu katika taaluma, sasa zinakwendea wapi. Sio kwamba Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wawape bilioni 4 tu, lakini watueleze na zile zinakwendea wapi na nyinyi kazidaini na ndio maana tukasema mawizara yawe na wataalamu ili waende wakajitetee kule Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, wazidai fedha zao. Kwa hivyo, kama zikipatikana basi zitaongeza kwenye kile kifungu ambacho tumepewa. Mbali ya mfuko kupangiwa bajeti, lakini kuna fedha ambazo zinakatwa mawizara yote kila mwezi kwa ajili ya kuendeleza elimu ya vijana. Sasa nyinyi hapa mnapotujia mnasema kwamba hizo ndizo tulizopewa tu. Mimi naunga mkono hoja hii, kwa sababu moja katika sababu inatokana na kutojitayarisha vizuri katika mambo yetu, ndio maana tukafikwa na mikasa hii. Lakini kwa sababu ilitajwa kwamba kutakuwa na fedha za kila jimbo milioni 10, zilitajwa kuwa zitakuwepo. Naomba sana ikiwa zipo na zishapatikana basi naomba niiunge mkono hoja hii na sahihisho alilotoa Mhe. Ismail Jussa kwamba fedha zote hizo kwa dharura hii basi ziende katika kuchangia elimu. *(Makofi).*

Kwa hivyo, tutakuwa na miwili hapo *skill development fund* itolewe na fedha hizi zilizotajwa kwamba zitakuwepo zitolewe ili tuone tumepunguza wanafunzi wangapi. Lakini Mhe. Spika, katika uendeshaji wa mfuko huu wa mkopo na nchi ndogo kama hii yetu. Ingepaswa wizara tokea mwanzo kabala haijatoa matokeo ya wangapi wamepata basi iseme uwezo wake, tena iseme katika vyombo vya habari kwamba uwezo wetu sisi ni kuchangia wanafunzi 500 wa mwaka wa tatu waliopo, 500 wa mwaka wa pili waliopo na wapya uwezo wetu ni 600. Sasa wale wanafunzi wajijuwe, lakini kuwaachia tu leteni maombi halafu unakuja kuwaambia kuwa wewe umepata na wewe hukupata ndio inayoleta migogoro.

Pia kuwe na utaratibu wa *waiting list* kwamba kama mtu kapeleka maombi yake mwaka huu na hakupata, basi yeye anapewa kipaumbele katika kipindi kijacho. Sisi wakati wetu ulikuwa huwezi kwenda kusoma mpaka uwe umetimiza miaka miwili kazini. Kama umeshaajiriwa unataka kwenda kuongeza elimu, sasa ni lazima kuwe na utaratibu ambao kila mmoja atajipima mwenyewe, badala ya kuwa mtu kamaliza sasa hivi huyu keshakaa miaka miwili na *qualification* nazo hapewi na hapo ndipo linapokuja suala kuwa je kuna upendeleo wowote katika mifuko kama hii.

Mhe. Spika, mimi sitaki nizungumze sana, baada ya kuunga mkono hoja kwamba kuwe na marekebisho katika kuongeza nafasi, maana yake simu kubwa ya mswada huu ni kwamba mwaka huu kupatikane uwezekano wa kuongeza nafasi zaidi kwa vijana walioomba masomo ya juu. Lakini serikali ione haja kwa ujumla kwamba mahitaji ya

nchi ni makubwa, na baadhi ya nyenzo za mahitaji yetu yamezuiwa na utaratibu uliopo katika shughuli za Muungano. Kwa sababu sisi tuliyataja mwanzo mafuta kuliko Uganda. Uganda wameshaanza taratibu za kuchimbua mafuta, sisi ndio kwanza tunasema yetu au si yetu.

Mhe. Spika, Seychelles, Madagascar pamoja na vile visiwa vya Pacific kule vinategemea sana uvuvi wa bahari kuu. Sisi ndio kwanza tunaanza kusema. Sasa kama hatujawa *aggressive* katika kushughulikia mambo ya kiuchumi na ndio hapo tunapoiona Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo bado imelegeza kamba, kwa sababu matatizo haya ni ya kiuchumi, iwe vijana wetu hawawezi kusoma kwa sababu ya fedha tu ni matatizo ya kichumi, tusiangalie pengine. Sasa lazima wizara zinazohusika ziwe *aggressive* katika mambo ya kiuchumi, ili tuweze kujikwamua kiuchumi.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, baadhi ya mawaziri hususan katika kipindi kilichopita, wakati tulikuwa tukitetea kwamba serikali inategemea sana bajeti yake kutoka mataifa ya nje wanasema ndio wajibu kwa sababu yale ya nje yameendelea na sisi ni maskini tutegemee. Sisi tukawakubalia sawa tutegemee mataifa ya nje, lakini je ikiwa sisi hatuna uwezo wa kujipapatua tukaweza kujiunga na baadhi ya jumuiya. Ukija kwenye michezo FIFA chini, ukija OIC zii, jumuiya ya Afrika ya mashariki gati hamna. Sasa tuelekee wapi, suala hili baada ya uchumi sasa linakuja suala la kisiasa kwamba lazima tujikwamuwe katika masuala haya kiuchumi na kisiasa na tunawataka majemedari wetu wapiganie katika suala la Muungano ili tuweze kujikwamua. Nakushukuru sana Mhe. Spika. Naunga mkono hoja na ninawaomba wajumbe wenzangu waiunge mkono, ili vijana wetu wapate ziada ya kuweza kujiunga na vyuo vikuu. Ahsante.*(Makofi).*

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ndogo. Makofi haya yanaashiria kuwa nina roho beni, kwa sababu hujatoa matokeo na mimi nitazungumza kidogo, kwa sababu hili jambo la bodi limenigusa.

Mhe. Spika, namshukuru sana kaka yangu Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kuleta mswada huu. Mimi nasema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kuna kitu hata kinaitwa *Tanzania Commission of University*. Hiki ni chombo kikubwa cha kuwadahili wanafunzi wote wa Tanzania na kuna bodi ya elimu ya juu ya Tanzania ambayo hiki ni chombo cha Muungano. Sasa mimi naanza kupatwa na wasi wasi mkubwa sana, kwa sababu wanafunzi wote walioomba kwenye bodi hii ni wanafunzi 112 tu wa vyuo vya Zanzibar vilivyoweza kupata mkopo katika vyuo vyote vya Zanzibar.

Lakini kubwa zaidi utagundua kuwa vyuo vyote ambavyo vimejiondoa katika *CAS*, yaani *Central Admission System* ndio vyuo ambavyo vimekosa mkopo huu wa elimu ya juu, kwa sababu gani. Hapa inaelekea pana mbinu ambayo inafanyika. Nimepata mashaka kwamba sio vyuo vya Zanzibar tu vilivyojiondoa katika hii *Central Admission System*, hata Chuo cha Kiislamu kule Morogoro kimejiondoa kwa sababu zake inazojua wenyewe. Nataka kusema kwamba ningeshauri wizara husika ikae na Serikali ya Muungano ili iweze kujua basi hiyo *potion* ambayo sisi tunaipata kwa kupitia bodi ya

mkopo basi bora tupewe wenyewe. Mhe. Zahra Hamad dada yangu alisema pale kuwa aligeuza kutoka mfuko wa elimu kuwa bodi kwa sababu ya kuimarisha na kuwa na nguvu zaidi, nakubaliana naye sana na namshukuru sana. Kwa hivyo, kwa kuwa tuna nguvu zaidi katika hii bodi yetu, tungeomba basi na hizi pesa ambazo zinatoka katika hii elimu ya juu ambazo ni za Muungano, sisi tupewe wenyewe ili tuzitie kwenye bodi yetu tuweze kuwa na nguvu ya ziada ili kuwasomesha watu wetu wengi zaidi.

Mhe. Spika, inasikitisha sana, leo wanafunzi 1,630 na kuweza kupata wanafunzi 300. Mimi nakaribia hata kulia, inasikitisha sana hawa wanafunzi wende wapi. Mhe. Spika, Jimbo la Mpendae limetoa milioni 10 juzi tu ili kuweza kuwasaidia wanafunzi wa jimbo lake angalau cha kuweza kuwakimu. Lakini nataka niahidi kuwa sasa hatulali, kama tuliochukua ndimu tukaipiga kwenye sega la nyuki, inaonesha vipi wananchi wetu ilivyokuwa umaskini umewajaa, hawana chochote, wanafunzi wanataka kusoma lakini hawana mtaji wa kuweza kuwasomesha, inasikitisha Mhe. Spika.

Mhe. Spika, niunge mkono hoja ya Mhe. Hamza Hassan katika kifungu chake nambari 1 inasema *account* iweko wazi. Hiki ni kitu muhimu, kuna wafanyabiashara wengi Mhe. Spika, nataka kusema wazi kabisa, hata Chuo cha Morogoro nina ushahidi tosha kuwa kimepewa na mfanyabiashara mmoja milioni 100 kwa kuwasaidia wanafunzi pale. Sasa tunao uwezo mkubwa wa kuweza kuwashawishi wafanyabiashara wetu, hata na sisi wenyewe. Kifungu cha 2 Mhe. Hamza Hassan amesema tufanye *razing fund*, kwa sababu Mhe. Spika, hivi sasa hii bodi tunaita kama iko ICU, wanafunzi wanataka kuingia barabarani, hiki ni kitu kimoja kigumu.

Mhe. Spika, mimi mwenyewe alinipigia simu Mhe. Hamza Hassan nikashiriki kwenye mazungumzo yale, lakini pale Mhe. Spika, unaweza kulia wale wanafunzi ambao tumekaa nao pale na sheria ya nchi yetu maandamano ni haramu. Kwa hivyo, mimi niliwaasa sana wasifanye maandamano, lakini Mhe. Hamza Hassan alituwahi kuleta hoja hii binafsi, tunaiinga mkono. Sasa tukae tayari basi wizara iandae programu yoyote ya kuweza kufanya *razing fund*. Ningeishauri wizara kwa sababu tuna viongozi wazoefu sana, kwa nini basi wasikae na Mhe. Haroun akakaa kidogo akatoa vipi alivyokuwa amepanga. Mhe. Haroun ana-*strategic* kubwa sana na nzuri za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, angalau hao wanafunzi wakaweza kupata mafao ya kuweza kusoma. Naiomba wizara sana kwa kupitia hoja hii binafsi leo ikae na Mhe. Haroun ili atuambie *strategic* nyengine alizokuwa akizifanya na wanafunzi wengi walikuwa wakipata huu mkopo wa kwenda kusoma.

Mhe. Spika, labda nichukuwe maneno ya kaka yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba sina shaka nayo kuwa fedha zote za majimbo hivi sasa tuzielekeze kwenye huu Mfuko wa Elimu ya Juu, ili wanafunzi wetu waweze kupata.

Mhe. Spika, naomba kutoa wito kwa wizara kama itaweza kutusikia basi izungumze na vyuo vyetu vilivyopo hapa Zanzibar kuongeza huu muda wa *registration*, kwa sababu muda unamalizika kesho kutwa na wanafunzi wanahaha mitaani, yaani mpaka kwenye chumba cha wageni wanatusubiri.

Kwa hivyo, namumba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali aombe muda wa *registration* uongezwe japo wiki moja, ili waweze kutafuta na Mhe. Hamza Hassan Juma alisema atatoa kiasi kidogo cha kuwapa kwa ajili na wao waweze kwenda kufanya *registration*.

Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na wala sitaki kusema mengi zaidi, kwa sababu bado roho yangu inanidunda kwani matokeo hujayatoa. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe na matokeo ninayo hapa lakini sisemi. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametujaalia mchana huu kuweza kuwa salama katika Baraza lako hili tukufu. Vile vile nichukue fursa hii Mhe. Spika, kukushukuru wewe binafsi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii muhimu tena adhim kwetu.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila iwapo sitompongeza kwa dhati Mhe. Hamza Hassan Juma, ambaye ametuonesha moyo wa uzalendo, kuipenda nchi yake pamoja na kuwapenda wananchi wan chini hii, ili waweze kupata mafanikio yale ambayo tunayatarajia. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kuleta Hoja hii Binafsi. *(Makofi)*

Pia nichuku fursa hii kuwaomba wenzangu wote ambao wenye uwezo kama Mhe. Hamza Hassan Juma, basi wasisite kuleta mambo muhimu kama hayo yanayosogeza taifa letu mbele. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza na mimi niungane na wenzangu wote wale waliochangia hoja hii kwa kweli nawapongeza. Kwa hivyo, pongezi zangu ni kwa wale Waheshimiwa Wajumbe wote waliobahatika kuchangia na kuweza kusema kwamba zile fedha zao za Mfuko wa Jimbo, basi kwanza ziende zikaokoe watoto wetu ambao ndio tegemeo letu. *(Makofi)*

Kwa kipindi kirefu tulikuwa na tatizo tena tumepoteza nafasi nyingi kwa kuona kuwa tulikosa wasomi, yaani watoto wetu walikuwa bado hawajapata hamasa ya kuendelea na masomo na Mwenyezi Mungu tumemuomba na ametukubali. Kwa kweli tumewahamasisha watoto wetu na sasa wako tayari wamesoma na tumeweza kupata watoto, ambao wenye bidii kubwa ya kufuatilia masomo mpaka wakaweza kufikia hatua hii ya Masomo ya Elimu ya Juu.

Mhe. Spika, tunasononekana sana kuona watoto wetu hivi sasa wamehamasika na sisi tumekosa uwezo wa kuendeleza zile juhudi ambazi tulikuwa tukizipigia kelele.

Nikiendelea na mchango wangu niungane na wenzangu pamoja na hii hoja ambayo imeeleza vifungu mbali mbali basi kwanza niseme naviunga mkono, ili viweze

kutukwamua katika matatizo haya. Mhe. Spika, uchungu wa mwana aujuae ni mzazi. *(Makofi)*

Kwa kweli tunasononeka sana tunapowaona watoto wetu wameshakuwa tayari wanataka kusoma, lakini hali ya kuwasomesha ikawa hatuna. Mhe. Spika, hivi sasa katika majimbo au mitaa yetu kuna foleni za watoto wetu kama hawa ambao wanapita kwa ajili ya kutuomba msaada.

Kutokana na hali hiyo, mimi nitashukuru sana kama hoja hii itaungwa mkono na itachukuliwa kwamba kikwazo hiki tukaweza kukishughulikia, ili watoto wetu wakaweza kufaidika na elimu hii, kwa lengo la baadaye tuje kuwa na taifa zuri, ambalo litakuwa na wasomi pamoja na wataalamu mbali mbali.

Mhe. Spika, sisi Wanawake Viti Maalum kwa bahati mbaya hatuna ule mfuko ule mfuko kama walionao wenzetu ambao wamejitolea hapa mfuko ule kwamba tayari uchukuliwe, kwa ajili ya kuwakomboa watoto wetu.

Kwa hivyo, kwa kupitia nafasi hii labda niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu wa Viti Maalum, ili nasi tukaweza kuchanga mchango wetu japo mdogo angalau na sisi tukaweza kuongeza nyongeza kidogo. Lengo ni kutaka kuwakwamua watoto wetu hawa na baadaye haya mengine maombi mbali mbali yameletwa katika hoja hii binafsi, basi yakaweza kushughulikiwa, kwa ajili ya kufaidika watoto wetu na masomo yao. *(Makofi)*

Kwa kuwa sisi mfuko huu hatujapewa basi nadhani iko haja mfuko huu tukapewa na sisi angalau japo usilingane na wale wenye majimbo, lakini na sisi mfuko huu unatusaidia sana. Kwa hiyo, ni vyema na sisi tukapewa mfuko huu, ili nasi wakati vinapotokea vikwazo kama hivi basi tukaonesha moyo wetu wa kizalendo na kuweza kujitolewa kwa kuweza kuwachangia watoto wetu, kwa ajili ya kufaidika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naiomba wizara kupitia kwako kwa sababu hili ni tatizo kwa watoto wetu na tunaoumia matumbo ni sote wazazi. Kwa kweli wizara ijipange pamoja na juhudi zote zinazofanyika, lakini bado wizara ijipange, ili kuweza kuona kwamba tunakwamua maendeleo ya watoto wetu ambao tayari wanataka kusuma, kwa sababu sisi wenyewe ni mashahidi.

Kwa mfano, kazi mbali mbali tunazikosa na tunasema hasa kama watoto wetu wamekosa kutokana na hawa sifa, yaani hawana ile elimu ambayo inatakiwa. Kwa kweli tumeona nafasi nyingi sana zinakuja kuchukuliwa na wenzetu kutoka nje kwa sababu ya kukosa elimu watoto wetu na hatimaye kazi zinachukuliwa na watoto wetu wanakosa na kupelekea kubali na wimbi kubwa la watoto wanaozurura hawana kazi yoyote.

Hivyo, niiombe wizara kupitia kwako Mhe. Spika kwamba ijitahidi kutafuta mbinu mbadala, lakini ihakikishe watoto wetu wanapata Elimu ya Juu, ili na sisi tuweze kupata wafanyakazi ambao tunawatarajia pia tuwe na wataalamu mbali mbali katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi nilitaka nisimame hapa kwa nia ya kuunga mkono tu hoja hii kwa asilimia mia moja, ili iweze kutusaidia na iwe dira yetu na baadaye tutaweza kufikiria mambo mengi yaliyomuhimu kuliko haya. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kuhusiana na hili niwashawishi Waheshimiwa Wajumbe wenzangu ambao wamo ndani ya Baraza hili tukufu kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ili tuone tunayemkomboa hapa ni Mzanzibari mwenzetu, ambaye badala ya sisi atakuwa yeye hapa. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kutoa machache juu ya Hoja hii Binafsi ya Mhe. Hamza Hassan Juma ambaye ni Mwenyekiti wangu wa Kamati. *(Makofi)*

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha asubuhi hii kukutana hapa kwa ajili ya kujadili mambo yanayotuhusu katika nchi yetu.

Pili nikushuksuru wewe kwa busara, hekima pamoja na utaratibu wako wa kutuongoza katika mambo mengi magumu na hatimaye kupata ufumbuzi wa kufaa.

Ni imani yangu kwa hivyo na hoja hii hatimaye itapata ufumbuzi na hawa tunaowaombea watoto wetu wataweza kusoma *Inshaallah*.

Mhe. Spika, mimi nina mengi ya kuzungumza. Lakini nataka nianze kwa msemo wa Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliposema kwamba “Ili tuendelee tunahitaji mambo manne nayo ni; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora”. Mhe. Spika, watu tunao miongoni mwa watu ndio hao tunaowataka wasome, ardhi ipo na mawili sina hakika kama yapo katika kiwango ambacho kinahitajiwa kuwa kipo, kuhusu siasa safi na uongozi bora. Lakini nizungumzie kuhusu uongozi bora ambao ndio ninaomashaka zaidi kuwa haupo.

Mhe. Spika, kwenye bajeti iliyopita serikali ilijitengea shilingi bilioni 4 kwa ajili ya Safari za Viongozi kwenda nje wakati ambapo kuna watoto wanaotaka kusoma na wala fedha hizo hazipo. Kwa hivyo, hapa maslahi ya watoto wetu hayakuangaliwa na ilionekana bora watu kutembea kuliko watoto wetu kusoma. Kwa kweli hapa nimetishika kidogo kwamba safari za matembezi ni bora kuliko masomo.

Vile vile niliwahi kusoma kidogo vitabu vya nyuma vya Kikoloni kuna kitabu cha kitoto kikiitwa Someni kwa Furaha. Sasa kuna kitabu moja cha tatu kilichosema kuwa Utaweza Kazi Gani? Mhuzi au Karani, Asiyejua Kusoma ni Mjinga Mjinga Mno. Kwa kweli kitabu hiki kilikuwa ninasisitiza umuhimu wa elimu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sisi tunasisitiza kuhusu elimu, lakini hatuwapi vijana wetu uwezo wa kupata hiyo elimu. Kwa hivyo, inakuwa mahubiri yetu na vitendo vyetu havikubaliani ndio maana nikasema uongozi bora bado haujakuwepo, kwa sababu hatuyaamini yale tunayoyasema. *(Makofi)*

Katika kuanzishwa Muungano wa Tanzania, basi mambo ya mwanzo ya msingi yaliyokuwemo yalikuwa ni kama 11 na hili la Elimu ya Juu lilichukuliwa kuwa ni jambo la muungano. Sasa kwa kuwa Zanzibar ni nchi na upande wa pili ni nchi nyengine, hivyo hapa Zanzibar sio idokolewe tu kile ambacho upande wa pili kinataka. Kwa mfano, kule mashamba watu wanapopiga huwa wanapelekeana vijisahani kwa hivyo Zanzibar isipelekewe tu.

Kwa maana hiyo, Zanzibar iwe na hisa tena na sehemu inayojulikana kuwa hii ni ya Zanzibar na wala sio wakubwa wakae na kusema wale tunawapelekea kiasi fulani, basi kwa kuwa na sisi ni nchi na kwamba fedha hizi za Elimu ya Juu zinakusanywa kwa misingi ya kimuungano. Kwa hiyo, Zanzibar iwe na haki sawa bila ya kujali ukubwa au udogo wake, kwa sababu wakati walipoungana walijua kuwa Zanzibar ni ndogo na walikubali kuungana, hivyo ipate haki sawa ya kila kitu katika mambo haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwenye mapendekezo ya hoja hii imetajwa Mfuko wa Jimbo, mimi sijauona katika jimbo langu hivyo siwezi kusema jambo ambalo sijaliona. Lakini kama upo kweli basi na mimi naunga mkono kuwa fedha zote zitakazopangwa kwa mwaka huu ziende kuwahudumia watoto wetu, ili wapate elimu. *(Makofi)*

Jambo la msingi ni kwamba zitumiwe kwa uadilifu pamoja na uangalifu tena bila ya upendeleo wowote wa mtu yeyote.

Wakati nilipokuwa nikichangia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika mchango wangu kuhusu mambo haya ya elimu sidhani kama Mhe. Waziri wa Elimu kama alinifahamu, lakini aliniambia hakuna rushwa au mpenyo wowote unaotumika. Kwa kweli inao wasi wasi pale ambapo kitu kipo kidogo basi watu huangalia kwa kujuana kwenye kugawa kitu kilichopo. Kwa hivyo, ninaomba pindipo hoja hii ikipita au ikikubaliwa basi kuwe na uadilifu wa hali ya juu.

Mhe. Spika, mimi binafsi sitokuwa tayari kama Mfuko wa Jimbo upo kweli basi kuuhamisha huko na halafu ukatumika kinyume na vile ambavyo tutakubaliana. *(Makofi)*

Nikiendela na mchango wangu sasa niende kwenye pendekezo la pili ambalo naliunga mkono, kwa sababu nimeona mara kadhaa pengine Mhe. Rais anakamata kalamu yake tu kuinadisha tena karamu yenye ya shilingi 200/- basi inanunuliwa kwa shilingi milioni 200/- na zaidi.

Kwa hivyo, nadhani *fund* hii ikianzishwa na Mhe. Rais akaamua kutoa kofia, kalamu basi kuna watu wataipandisha daraja ya hali ya juu na itaweza kuisaidia kuchangia Mfuko huu wa Elimu, ili watoto wetu wapate elimu tunayotarajia, kwa sababu taifa ambalo halina elimu hatimaye ni kumalizika. *(Makofi)*

Kwa kweli elimu ambayo ninayo mimi sasa ni *just* najua kusoma na kuandika tu, hivyo mtu yeyote mwenye elimu kama yangu basi asijieone kuwa amesoma, isipokuwa ajione kwamba angalau anajua kusoma barua yangu. Kwa maana hiyo, tusiliache taifa letu na

watu wenye elimu ya kiwango cha elimu yangu mimi, tukiliacha hivyo basi tutakuja kutawaliwa upya. Mhe. Spika, tunatawaliwa kidogo kidogo bila ya kujijua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hoja ya mwisho ya Mhe. Hamza Hassan Juma kuhusu Jumuia ya *OIC*. Kwa upande wangu nadhani Zanzibar isiogope na ikae kama mwanamke wa shamba wakati anapogombana na mumewe na saa 8:00 usiku akamuacha, basi wakati huo huo anatoka mle halali hata kama kwao ni mbali anakwenda zake.

Kwa hivyo, na sisi tusiogope mtu juu ya kutetea haki zetu, kwa hivyo tunayo haki kwa sababu ni nchi ya kujiunga na Taasisi yoyote ya Kimataifa kwa maslahi ya nchi yetu. Mhe. Spika, tusiwe ngalawa ya Kiwani, isipokuwa tuwe na maamuzi na wala ngalawa ya Kiwani siifafanui naiwacha hivyo hivyo, kwa kweli tuwe na maamuzi, kwa sababu tukikaa tunamuogopa bwana, basi tutalala na njaa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nchi yetu inao uwezo wa kuendelea lakini kuna mtu anatukwaza na sisi tunamtii, yeye anakwenda mbele ya yake na sisi ametufunga kamba ya kiuno na huku anatuvuta nyuma, kwa bahati mbaya tunaridhia kuvutwa nyuma. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi sitaki niseme sana kuhusu suala hili. Lakini nimeona kwa sababu mimi mzazi tena ninao watoto ambao wanahitaji kusoma, basi nimeona angalau niseme chochote kuhusu hili.

Vile vile nimpongeze sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa uoni wake wa kuweza kuleta hoja hii, basi niseme naunga mkono na ninawaomba kwanza Waheshimiwa Mawaziri kwa kuwa na wao ni Wazanzibari, pia na wao wanao watoto kwa vyovyote vile ingawa wao wanao uwezo wa kuwasomesha tena wanapotaka na wala si lazima hapa. *(Makofi)*

Hivyo ni vyema waunge mkono kwa maslahi ya watoto kwa wanyonge wengine na hatimaye *backbenchers* wenzangu wote kwa jumla hoja hii waiunge mkono, kwa yule ambaye hatounga mkono hoja hii basi tumuone kuwa ni mchawi kwa watoto wa Wazanzibari. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Ussi Jecha Simai: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii adhim ya kuchangia Hoja Binafsi ambayo imewasilishwa kwetu hapa na Mhe. Hamza Hassan Juma, ambaye ni Mwanaharakati wa Haki za Binadamu. *(Makofi)*

Pili namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa mzima wa afya na kuweza kusimama hapa kwa ajili ya kuchangia hoja hii.

Vile vile nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwa kuikubali na kuichangia hoja hii adhim.

Mhe. Spika, nataka niwapongeze wanafunzi wote ambao walikubali ushauri wa viongozi wetu wa kusitisha maandamano, kwani maandamano ilikuwa sio suluhisho zuri kwa ajili ya kudai haki. *(Makofi)*

Nianze mchango wangu kuhusu hoja hii, kwanza kabisa juzi tu tumepitisha sheria ambayo inaongoza Bodi ya Elimu ya Juu pamoja na mambo mengine sheria hii iliweka bayana kwamba pamoja na kupewa mkopo wa kusomea tu, basi sheria hii imeonesha kuwa itatoa na zile gharama nyengine kama vile chakula na usafiri. Kwa kweli tulifurahi sana hapa baada ya kuona hivyo, kwa sababu ni kilio cha wanafunzi cha muda mrefu cha kukosa yale mambo muhimu katika masuala ya masomo.

Lakini jambo la kusikitisha Mhe. Spika, sheria hii inaanza kazi, yaani utekelezaji wake ndio unaanza sasa katika kuanza utekelezaji huu naona tumepata maafa makubwa sana.

Kwa mfano, tukiangalia utaona bora ule awali kwamba wanafunzi wanapata ile *tuition fee* tupu na wala hawapati mambo mengine, lakini baada ya kuingiza mambo mengine sasa imekuwa hata ule uwezo wa kuwachukua wanafunzi kusoma katika kile kiwango peke yake cha mkopo mtupu wa masuala ya *tuition fee* hazikupatikana kwa mwaka huu. Kwa kweli jambo hili ni la kusikitisha sana.

Mhe. Spika, katika suala la Mfuko wa Jimbo naunga na hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na hoja za Waheshimiwa Wajumbe wengine kidogo nitakenda kinyume nazo, kwa sababu huo Mfuko wenyewe wa Jimbo mpaka leo hatujajua kama kweli upo au haupo, kwani bado hatujaupata. Lakini kila Mjumbe wa Baraza lako hili tukufu tayari ameshapanga mambo mengi sana kwa ajili ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi pamoja na ahadi za wananchi kwa kupitia mfuko huu.

Sasa tunataka kufundisha Elimu ya Juu kwa kutumia mfuko huu, lakini sasa tukubali ukweli uliowazi kwamba wanafunzi wetu wa ngazi za chini Skuli za Msingi wanaendelea kusoma nje ya mabanda ya skuli na pia wanafanya mitihani katika maeneo ya wazi ambayo kuna miti kama vile minazi pamoja na miembe na hii ni hatari. Kwa hivyo, katika hoja hii nakubali kwamba zile shilingi milioni mbili basi zichukuliwe kwa ajili ya kuchangia mfuko huu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ukweli uliopo ni kwamba kupata mkopo wanafunzi 300 haya ni maafa makubwa yaani yanakaribiana na yale tuliyoyapata juzi ya Meli ya *MV. Spice Islander*. Kwa hiyo, hapa katika kushauri ni kwamba tulipata msiba mkubwa juzi hapa na serikali ilifanya juhudi mbali mbali kama vile kuwaomba wahisani pamoja na wafadhili mbali mbali kutuchangia kutokana na maafa yale ambayo tumeyapata. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, ni vyema na hili tulichukue ni jambo zito sana serikali ifanye jitihada zake za kutafuta watu wengine ambao ni wafadhili kwa ajili ya kuweza kutuchangia, ili tunusuru maisha ya wanafunzi wetu hawa ambao kwa sasa hawajajijua kama ni wanyama au ndege.

Nikiendelea na mchango wangu naomba kutoa ushauri ni kwamba kwa kuwa hivi sasa panaharibika lakini bado hapajaharibika kabisa na muda tunao na serikali inao uwezo. Sasa kwa kuwa panaharibika basi naomba idara pamoja na mashirika yake ya serikali angalau wakapunguza asilimia ndogo kwenye bajeti zao kwa ajili ya kuchangia huu mfuko, ili tuweze kupunguza idadi kubwa ya wanafunzi ambao wamekosa huu mkopo.

Mhe. Spika, ushauri wangu wa pili serikali kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali basi izungumze na hivi Vyuo Vikuu vilivyopo katika nchi yetu na hata kama hapa Zanzibar peke yake, kwa ajili ya kukubaliana nao kwamba kwa mwaka huu itakuwa hatuna fedha za kuwalipa wao kwa wale wanafunzi wetu waliomba vyuo.

Kwa hivyo, nadhani ni vyema tungelikubaliana nao na kuweza kutupunguzia watu kidogo kwa ajili ya kuja kuwalipa kuanzia mwakani, ambapo hapo tutakuwa tumeshapata maarifa ya kuzipata fedha.

Ushauri wangu mwengine Mhe. Spika, kuhusu Fungu la Bajeti la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia mfuko huu basi lingeliongezwa kwa bajeti ijao, tukahakikisha kwamba angalau hatupati wanafunzi 600 kamili, basi angalau tungelipata wanafunzi 500 tukaweza kuwasomesha kwa mwaka.

Sasa nikija moja kwa moja katika ushauri ambao Mhe. Hamza Hassan Juma aliutoa katika Hoja yake hii Binafsi mimi niseme kwanza nakubaliana nayo yote haya, kwa sababu ushauri wote uliotolewa hapa unaonekana kuwa ni mzuri na una nia ya kuwaendeleza wanafunzi wetu, pia una nia ya kulisaidia taifa letu kwa ajili ya kupata wataalam walio bora zaidi hapo siku za mbele.

La kwanza katika ushauri wake serikali iweke wazi *account* yake ya mfuko wa Elimu ya Juu ili kila asasi au mtu binafsi au shirika liweze kuchangia kwa yule mwenye nia ya kuchangia kwa ajili ya kuutunisha mfuko wetu huu, hili nakubaliana nalo sina mashaka nalo.

Lakini ushauri wa pili pia serikali iandae *reusing fund* na mgeni rasmi awe Mhe. Rais nalo hili halina mashaka kabisa.

Lakini niangalie jengine alilolipendekeza nambari saba hapa kwamba serikali yetu ya SMZ kuitaka serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweka ile asilimia maalum, kwamba Zanzibar asilimia yake ngapi kutokana na mfuko huu hapa , hii itatuwezesha sisi wenyewe kuweza kujiamulia kipaumbele chetu ni kipi mwaka huu cha kusomesha wanafunzi wetu na wepi tutawachukua, hili litatusaidia sana.

Kwa kuwa muda unakwenda mimi niseme tu kukubaliana na wenzengu kwamba naunga mkono hoja hii kuanzia herufi ya kwanza, hadi herufi ya mwisho ya maelezo yake Mhe. Spika,.

Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia fursa hii na mimi niungane na wenzangu kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha siku ya leo tukiwa hai, na kutupa uwezo wa kuijadili hii hoja.

Pili nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikuitumia fursa hii Mhe. Spika, kukushukuru wewe binafsi kwa kuweza kuipokea hoja hii na kuileta mbele yetu, nilikuwa nazungumza na wenzagu sasa hivi hapo nje wananipigia jamaa wamefurahi sana. Kwa kweli katika kitu ambacho wamekisifu ni hichi na nadhani kuipokena na kuileta hoja hii mbele yetu imetujengea kuwa na kiwango cha mabunge ya *Commonwealth* ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Spika, vile vile nadhani nitakuwa mwizi wa shukurani kama sikutumia fursa hii kumshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa kuweza kuwa mbunifu wa kuona matatizo ya nchi na kujajengea hoja, laiti ingelikuwa tunazungumzia mambo mengine ya jamii kama vile mabo ya tamatheli na semi fasihi simulizi basi hoja yake hii Mhe. Hamza Hassan Juma tungesema ni kioo, ambacho serikali wangeweza kukiangalia na hatimae kujirekebisha.

Mhe. Spika, sasa nadhani niende kwenye hoja moja kwa moja kwa kuanza na kutoa tanbihi ndogo kwa kum- *cort* mwandishi mmoja makini na mahiri bwana Shaban Robart, katika kitabu chake cha kusadikika bwana Shaban Robert alisema elimu ilipokuwa haijulikani mvi zilihisabiwa kuwa ni alama ya hekima. Wale waliokuwa hawajui mvi ni kongwe ambazo mimi ninazo hizo na Spika wetu nadhani anazo vile vile mvi. Kwa hivyo elimu ilipokuwa haijulikani mvi zilihisabiwa kuwa alama ya hekima lakini wakati wake umepita na wala haurejei tena, jambo lisilokubalika ni kwamba mtu yoyote kama hakuelimishwa mvi zake hazihisabiwi kama ni hekima.

Kwa hivyo Mhe. Spika, viongozi wa SMZ baada ya kuiangalia nadharia hii viongozi wa SMZ wa wakati ule wakiongozwa na Jemedari wetu wa Mapinduzi Mhe. Mzee Abeid Aman Karume marehemu amlaze mahali pema peponi, kwa kuangalia nadharia hizi akaanza kutumia nguvu zake zote za kiuchumi kutusomesha mkiwemo nyie mawaziri ambao mnatuongoza sasa hivi. Mzee Karume yeye mwenyewe hakwenda shule lakini aliwasomesha nyinyi, kwa nini nyie wataalam mlioko kwenye B araza la Mawaziri hakuna mwenye degree moja au mbili au ana master, lakini nyie mnashindwa kuwasomesha watoto wa nchi hii aibu. Tena inasikitisha sana hapa Mzee Karume pamoja na kwamba hakuwa na elimu akaamua kutusomesha mkachukua madegree mliyokuwa nayo mkachukua serikali mnatuongoza, lakini nyinyi mnashindwa kutusomesha.

Mhe. Spika, nadhani sasa imefika wakati eti wanasema kwamba kuna tatizo na tatizo lenyewe ni kwamba hakuna pesa za kuwasomeshea watoto wetu, mimi nadhani ukiachilia mbali na SMZ sisi tuna haki zetu kwenye SMT Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zingeweza kuwasomeshea watoto wetu asilimia mia moja, lakini sisi tuna hofu kudai haki zetu kule. Kuna bodi ya Elimu ya Juu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaweza kusomesha pekee karibu asilimia sitini ya watoto wetu hapa, lakini hakuna habari wanatupa tu akiamua waziri wa elimu sijui ni nani siku hizi tunapeleka watu ishirini ndio hao hao.

Mimi nadhani waheshimiwa musiwe na hofu nyinyi tumewapa dhamana na Mwenyezi Mungu atawahoji vipi mmetuongoza, mnaogopa nini kudai haki zetu eti, kwa mujibu wa bwana mmoja anaitwa Lennin katika kitabu chake cha *fridown cand united* alisema

kama kuna uso mbaya sana katika uso wa ulimwengu basi ni utumwa wa hofu, kwa hivyo nyinyi mliopewa dhamana ya kutuongozea nchi mnatuingiza katika utumwa mbaya nasa.

Mhe. Spika, mimi nadhani imeshafika wakati sasa sisi tulipojiunga na *OIC* wale wenzetu wakatuletea ngebe wakatukatalia Jumuiya ambayo ingetusidia sana katika kupata mambo kama haya ya elimu, mimi nadhani sasa hivi umefika wakati Mhe. Balozi Seif Ali Iddi yupa hapo Makamo wetu wa pili wa Rais na Mkuu wa shughuli za serikali wakitaka wasitake sasa SMT tuingike kwenye ile *OIC.* Mhe. Spika, wakitaka wasitake na ni kosa bwana mimi nadhani nataka kusema wanasheria tutafute kipengele kidogo tu na sisi tujisukue kwenye *OIC* tupate.

Mhe. Spika, nashukuru kwamba katiba zetu zote mbili zinatoa haki kwa kila Mzanzibari kupata elimu kwa mujibu wa uwezo wake, lakusikitisha sana pamoja na kwamba mwaziri wetu wana elimu lakini *there are not creative* na kuweza *ku-translate* hii katiba yetu kuifanya katika metendo yenye kutekelezeka, kwa mfano hawajatujengea mazingira maruzi hawa ya kupata elimu kuanzia kwenye skuli ya vidudu siku hizi wanaita maandalizi mpaka Chuo Kikuu sasa hivi kuna hiyo hoja ya kuchangia elimu inakuwa ni mashaka makubwa.

Mzazi akiwa na watoto wawili tu kuanzia *primary* inakuwa tabu kuchangia elimu achilia mbali hiyo elimu ya juu, tunataka mutujengee misingi ya utekelezaji wa hii katiba yetu ya nchi kwamba haki ya kupata elimu kwa kila Mzanzibari iweze kutekelezeka lazima mtujengee misingi kabisa kabisa Mhe. Spika, serikali na katiba unaambiwa inasema hivi lakini kila mwezi mtoto wa chekechea umlipie zaidi ya shilingi elfu nne sisi tunazaa sana, mfano mtu ana wake wawili na ana watoto wa chekechea watatu inakuwa mtihani, mwenye wake wanne kama mimi inakuwa na watoto wa chekechea wanane utalipia vipi

Kwa hivyo tujengeni mazingira ya kuwapatia watoto wetu taaluma kwa hivyo mnampa mzigo Mhe. Hija Hassan Hija, watu wenye wake wanne kama Mhe. Hija Hassan Hija pale inakuwa tatizo.

Mhe. Spika, hiyo mikopo inayotolewa sasa hivi katika kwenda vyuo vikuu inatolewa katika misingi ya ubaguzi, wanabagua sasa unaweza kuwa *first division* lakini unakwenda kufanya Sheria au *Public administration* akaja kuchukuliwa mtu ana *second division* ana mambo ya *PCM with aducation*. Sasa huu ni ubaguzi hawa wote ni watoto wetu hawa wote ni Wazanzibari lakini unasema mara hii tunachukua watu wa sayansi wa art hatuchukui, ni ubaguzi wazee wao hawa wanalipa kodi sawa sawa bila ya kubagua. Leo nyinyi mnawabagua nini ikiwa hamna uwezo wa kusomesha msisomeshe wote lakini kusema leo tutachukua art hawa hatuwachukui.

Waheshimiwa mawaziri mliokuwepo huko mbele nyote mnatokea vyama viwili tu aidha CCM au CUF mimi sijawahi kuwa mwana CCM ila nimeshawahi kuwa Mwana AFRO SHIRAZI, lakini siku moja niliokota kadi ya CCM nikaisoma huku nyuma imeandikwa binaadamu wote ni sawa kila mtu anastahiki heshima na kutambuliwa utu wake, Sasa leo nyie mnawabagua kwamba huyu ni artist awa ni nani wote wanastahiki heshima na kulindwa utu wao.*(Makofi)*

Ukija kwenye kati ya CUF haki sawa kwa wote haya ikowapi hiyo sawa jamani msitucheze shere sisi tuna akili pengine kuliko nyie.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naunga mkono hoja nay ale mapendekezo yote ya Mhe. Hamza Hassan Juma nayaunga mkono mia kwa mia. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Nashukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii leo hii kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, awali ya yote Mhe. Spika, ningependa kumpongeza Mhe. Hamza Hassan Juma kwa hoja ambayo ameifikisha mbele yetu ni hoja ya msingi sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma ni mwenyekiti wangu wa kamati ya kusimamia viongozi, katika kipindi kifupi sana ambacho nimekuwa na Mhe. Hamza Hassan Juma ana sifa mbili muhimu. Sifa ya kwanza ni mzalendo lakini sifa ya pili ni mjasiri, mara nyingi huwa anathubutu na anaweza. Kwa hivyo sina budi kumshukuru sana kutuletea hoja hii ya elimu kwa sababu inatuhusu sote, labda niseme kwamba hoja hii ilikuwa ndani ya nyoyo za kila muwakilishi aliyemo ndani ya nyumba hii pamoja na wananchi wa Zanzibar.

Mimi kwanza ningesema lazima tuelewe elimu ndio msingi wa maendeleo ya nchi yetu, na tunafahamu kwa nini tunasema hivyo na Mapinduzi yetu matukufu ya Zanzibar yaliona umuhimu mkubwa wa elimu ndio maana elimu ilipewa kipaumbele kwa Wazanzibari wote, elimu ambayo tuliambiwa atuitafute tuliambiwa tufike mpaka China kwa sababu elimu utaipata pahala popote ikiwa kama wewe utataka kupata elimu.

Mhe. Spika, mara nyingi elimu yetu Zanzibar inakumbwa na misuko suko mingi sana lakini hili ambalo leo tumelileta hapa huu ni msuko suko mkubwa, vijana wetu wanataka kusoma wanaitafuta elimu lakini wanawekewa vikwazo wakati elimu ni haki yao lakini wanawekewa vikkwazo ili wasiipate hii elimu. Tunawaambia wasome sana wakiwa kwenye madarasa mpaka kufikia la kumi na nne tunawaambia wasome sana, lakini wanapata vile vigezo ambavyo vinawataka wapate elimu ya juu, lakini wakiomba mikopo wanaambiwa kwamba bado hawajatimiza vigezo au wanaambiwa sasbabu nyengine yoyote.

Sasa mimi niseme kwamba hizi sababu ambazo mara nyingi tunapewa kwamba vijana wetu hawapati hii mikopo ni sababu fedki kwa kweli, kwa sababu kama wametimiza vigezo basi hakuna sababu ya kuwazuia wasipata mikopo, ikiwa kama kweli tumejipanga kuwasomesha hawa vijana, vijana wetu tukiwaachia hapa kwa sababu bado umri wanaomaliza madarasa yao ni umri wa vijana bado watakwenda kuingia katika matatizo mengine, kama hawajapa elimu ya juu.

Mhe. Spika, tuna vijana wetu wengi ambao wamemaliza madarasa ya kumi na nne hawakufanikiwa kupata elimu ya juu wameingia katika tabia mbaya za kutumia unga na madawa ya kulevya, wapo tunawajua , sasa mimi namshukuru Mhe. Hamza Hassan kwamba ameleta hii ili kuwanusuru vijana wetu ambao wako katika njia panda, elimu

wanataka lakini sisi bado hatujajipanga vizuri kuhakikisha kwamba vijana wetu watapata elimu.

Mhe. Spika, mimi labda niunge mkono mapendekezo yote ambayo ameyatoa Mhe. Hamza katika hoja yake kwa sababu mapendekezo haya yatatoa nafasi kubwa zaidi ya vijana wetu kupata elimu ya juu, naweza kusema kwamba hata sisi wenyewe tukishiriki katika kuchangia sisi wawakilishi na wananchi wengine ambao wana uwezo wakishiriki katika kuchangia, basi nina hakika kwamba tutawasaidia vijana wengi kuweza kupata elimu yao ya juu.

Kwa hivyo mimi ningeseme kwamba sisi wenyewe Wazanzibari kabla ya kuwatizama hao wenzetu ambao wanatutenga lakini sisi wenyewe Wazanzibari tuhakikishe kwamba tunafunga mikanda awatoto wetu wapate kusoma, Inanisikitisha sana kuona watu wetu wanaokosa elimu ni watoto wa wakulima na wafanyakazi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, tukiendelea na mtindo huu huu umasikini hautotuondoka kwa sababu ikiwa kama hatutowapa nafasi watoto wetu wakawa wataalam wakaijenga nchi hii kwa kuwa na visingizio vyengine , nina hakika nchi hii haitoendelea wataalam tunawahitaji. Tunakwenda Afrika ya Mashariki sasa hivi soko huria, sasa kama hatuna wataalam hapa watakuja wakenda, waganda na kazi ambazo sisi wenyewe tunaweza kuzifanya Wazanaibar, inachosikitisha zaidi kwamba hawa watoto na vijana wetu uwezo wanao na wanatuonyesha kama uwezo wanao, lakini sasa sisi tunafunga macho sisi viongozi tunafumba macho.

Mhe. Spika, mimi nimekuwa mwalimu wa skuli nimesomesha watoto wa aina mbali mbali wakiwemo watoto wa kimasikini, wakati huo skuli zilikuwa hazina tabaka niliposomesha mimi kulikuwa na *public School* Skuli za Serikali tu *private* hamna, pale unaona kwamba watoto weote walikuwa ni sawa uwezo wao ulikuwa hata walikuwa hawashiriki vizuri lakini wengi wao walikuwa na uwezo, watoto wa wakulima na wafanyakazi watoto wa masinkini. Lakini leo watoto hawa hawa masikini tunawanyima uwezo wa kusoma na ninawajua wanafunzi wangu ambao walikuwa watoto wa masikini na wamefanikiwa na wamefika elimu ya juu wakati huo changamoto hizi zilikuwa hazipo.

Lakini leo watoto wa masikini wanakosa kwa sababu wengine wanao watu wa kuwafadhili na kuwapa pesa wakapata elimu ya juu, kilio changu ni watoto wa masikini wataendelea kuwa masikini. Ipo haja serikali yetu kuliangalia hili suala kwa makini sana, kwa sababu hapa tutakosa imani za wananchi wetu kwa sababu sisi kila siku tunasimama na kuwaambia kwamba tunaendelea. Lakini ukiangalia hayapo maendeleo sasa mimi nafikiria serikali hapa ijikaze itafute mbinu yoyote kuhakikisha fedha zinapatikana na wanafunzi hawa wanapata fursa ya kuendeelea na masomo yao ya juu.

Mhe. Spika, mimi mara nyingi huwa nasikitishwa sana namna tunavyotumia fedha zetu mimi naamini tukijipanga vizuri fedha zetu tunaweza kuzitumia vizuri, huwa nasema mambo mengine tunajitakia wenyewe, tunajua kwamba tunahitaji wataalam lakini basi kwa nini tunapanga vitu ambavyo havina ulazima, tukisema kwamba ni sawa na sahihi

kushehekea sherehe zetu tukazifanya zikawa nzuri, lakini hakuna ulazima kuzifanya sherehe zile kuwa kubwa, tutoe fedha zetu tuingize kwenye elimu watoto wasome. Vijana wetu wanataka kusoma lakini sisi tunachukua fedha tunaziweka pale ambapo hapahitajiki kuwekwa sio lazima kufanywa sherehe. *(Makofi)*

Lakini la pili Mhe. Hamza Hassan Juma amesema hapa kuhusu safari tupunguze tuangalie uwezekano wa kwamba tunapunguza safari ili kuhakikisha watoto wetu wapate kusoma.

Mhe. Spika, mwisho kabisa mimi ingawa nimesema kwamba nimeunga mkono mapendekezo yote lakini suala la Zanzibar kujiunga na *OIC* nafikiria ni muhimu tusiikose hiyo nafasi, hiyo nafasi ni muhimu kwa sababu wenzetu wanaitumia na sisi Zanzibar basi tuitumie, tujiunge na sisi tupate manufaa ya *OIC*, lakini tukisema kwamba tunasubiri tunasubiri. Bila ya shaka kuna taratibu ambazo tunatakiwa tuzifuate lakini mimi naamini tuna watu wetu ambao wanaweza kuzisimamia hizi taratibu lakini kuhakikisha kwamba na sisi tumejiunga na *OIC*, tukisema kila siku tunangojea wenzetu wa upande wa pili watufanyie haya hawatufanyii Wazanzibari tujifanyie wenyewe. *(Makofi)*

Hapa hakuna wa kutubeba tujifanyie wenyewe, mimi ningemuomba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali katika mchakato huu ambao utafanywa tena kama alivyotuahidi kwa mara ya pili naomba watoto wetu wa kike wafikiriwe katika hil, wafikiriwe tena kwa mara ya pili ili na wao angalau basi waweze kupata fursa ya elimu ya juu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache kwa niaba ya wanawake wote wa Unguja na Pemba naunga mkono hoja hii, narudia tena nampongeza sana Mhe. Hamza Hassan Hija kwa kuleta hoja hii na naamini kwamba hii hoja italeta mafanikio katika taifa letu. Ahssante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Muda uliobakia sio wa kutosha na kuna mambo mawili matatu ambayo nataka nitoe maelekezo kwa Baraza kuhusiana na hoja hii pamoja na shughuli zetu nyengine zilizobaki, kwa hivyo nimuombe Mhe. Subeit anistahamilie mungu akipenda achangie jioni pamoja na Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Ali Salim Salum Haji, Mhe. Suleiman Hemed Khamis, Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Omar Yussuf Mzee Waziri wa Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Pengine baada ya maelezo nitakayotoa pengine kun wengine wanaweza kujitokeza hasa kwa upande wa serikali ili kuweza kuweka vizuri masuala haya yanayohusu hoja hii kwa mujibu wa taratibu zetu kisheria, mwengine wa mwisho katika waombaji ni Mhe. Abdalla Mohammed Ali.

Waheshimiwa wajumbe kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa kuendesha shughuli zetu vizuru na ufanisi mzuri, naomba kwanza nitoe tangazo moja muhimu kwamba mara baara ya kuahirisha shughuli zetu mchana huu basi nawaomba

waheshimiwa Mawaziri wote bila ya shaka na Mhe. Mwanasheria Mkuu na Naibu Mawaziri kubaki kuna mazungumza na Makamo wa pili wa Rais.

Jambo la pili unapoiangalia hii hoja kuna mambo yanagusa bajeti ambayo tuliipitisha na hatimae tukaipitisha kwa mujibu wa sheria, Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo atakuja kuchangia na anaweza kutuelekeza suala hilo, kwa sababu yaliyomo ndani humu yanagusa bajeti ambayo tulikwisha kuiptisha kisheria, pengine na Mwanasheria Mkuu nae anaweza kuja kuwa na maneno katika jambo hilo. Hivyo ningeomba basi serikali hilo mlioni na mtizame vipi tunaweza kumaliza jambo hili kwa mujibu wa taratibu bila ya kukiuka sheria tuliyoipitisha katika baraza hili.

Lakini la pili nilipendekeze kabisa ukiangalia michango ya wajumbe juu ya hoja hii mengine yamekuja moja kwa moja kama wajumbe walivyoeleza kuunga mkono hoja hii kama ilivyo, lakini kumekuwa na marekebisho ya hapa na pale sasa ili tuende vizuri nitakuja kuomba utaratibu wa kupitisha basi twende kwenye *Item* moja baada ya nyengine ili tuhakikishe kwamba tumekwenda vizuri bila, kuliko kuja kuichukua kwa ujumla halafu mengine kumbe mna marekebisho yake ambayo sisi wenyewe waheshimiwa wajumbe tumeyapendekeza huo ndio utakuwa utaratibu namna ya kupitisha hii hoja.

Jengine ni kazi muliyoifanya muda sio mkubwa kabla ya hoja hii kuwasilishwa, uchaguzi wa mwenzetu mmoja muwakilishi wa baraza hili ili kujaza nafasi iliyoachwa wazi na Marehemu Mhe. Mussa Khamis Silima, mmefanya kazi hiyo vizuri hakutakuwa na marejeo ya uchaguzi, saini zimetiwa na wote waliohudhuria pale kwenye kuhesabu kura kwamba wameridhika na mtokeo yale na hakukuwa na malalamiko kabla kama uchaguzi umeingiliwa hapa na pale. Uchaguzi ulikwenda vizuri na pia kuhesabu kura kulikwenda vyema.

Sasa naomba basi nichukue nafasi hii kutoa matokeo ya uchaguzi mlioufanya vizuri sana kama saa mbili zilizopita, waheshimiwa wajumbe idadi ya wapiga kura ilikuwa ni wajumbe sabini na moja (71) kama tulivyopiga mahesabu na tukathibitisha hivyo kwamba wajumbe (71) ndio waliopiga kura.

Wajumbe waliopiga kura (71) Hakuna kura iliyoharibika hata moja.

Matokeo ya Kura:

Mhe. Mussa Ali Hassan	Kura	15
Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Kura	23
Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa)	Kura	33

Waheshimiwa Wajumbe kutokana na matokeo hayo napenda kumtangaza rasmi Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa jimbo la Mpendae ninakoishi mimi, amechaguliwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kuwa mbunge wa bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *(Makofi)*

Matokeo haya yameridhiwa na wote waliochaguliwa kuhesabu kura kwenye chumba cha kuhesabu kura na *returning officer* ambae ni katiba wa Baraza la Wawakilishi ndio ametuletea matokeo haya yaliyosainiwa na wote waliohudhuria uhisabuji kura huu. Naomba tuchukue nafasi hii kumpongeza sana mwenzetu Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano *(Makofi)*

Kuna muda mchache kama kuna maneno ya shukurani mawili matatu tukianzia na Mhe. Mussa Ali Hassan.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Nashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kutoa maelezo kidogo kuhusu uchaguzi wetu tuliofanya hivi sasa, sina budi kutoa shukurani nyingi sana kwa uchaguzi huu jinsi ulivyokwenda vizuri na ulivyokuwa wa haki, mimi mwenyewe binafsi sina budi kumshukuru Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa kupata ushindi mkubwa tena wa uhakika. *(Makofi)*

Nina hakika tumepata kiongozi mzuri ambae atakwenda kutuwakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wawakilishi wote wa Zanzibar, kwa kumkumbuka mwenzetu ambae amefika mbele ya haki Mhe. Mussa Ame Silima sasa ukanda huo tunampa ndugu yetu atuwakilishe vizuri kama alivyotuwakilisha Marehemu.

Ahsate sana kwa yote Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kutoa shukurani baada ya uchaguzi wetu uliomalizika, nianze shukurani zangu kwa wale wote ambao walinipa kura za ndio nawashukuru san asana, lakini vile vile nitoe shukurani zangu za dhati kwa wale ambao hawakunipigia kura ya ndio kwa sababu wametumia demokrasia yao kwa sababu ni haki yao hiyo. Nawashukuru sana *(Makofi)*

Lakini vile vile nichukue nafasi hii Mhe. Spika, kumpongeza Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa ushindi mnono alioupata, naahidi nitashirikiana nae na tupo pamoja nae na aende akatuwakilishe na sisi tunamsukuma pamoja nay eye. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahasante sana Mhe. Spika, kwanza sina budi kukushukuru wewe mwenyewe juu ya kiti chako hapo, vile vile nichukue fursa hii kuwashukuru ndugu zangu mawaziri, vile vile niwashukuru *back benchers* wenzangu ambao kwa muda wote wa uchaugzi walikuwa watulivu tena wenye upendo mkubwa sana. Nataka kusema hakuna mshindi sote ni washindi isipokuwa kura zao hazikutosha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni imani yangu kuwa wote wataniunga mkono na huko walikonipeleka nitawakilisha ipasavyo ndani ya nafsi yangu na wale ambao tumeshindana pamoja basi niko nao pamoja bila ya wasi wasi wowote. Vile vile nichukue fursa hii kuwapongeza sana wale ambao wamenipa kura zao za ndio, nalini nitakuwa mwizi wa fadhila kama

sitowapongeza walionipa kura za hapana. Wametumia demokrasia na nawashukuru sana na nawambia tuko pamoja kwa hali na mali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwapongeza. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe nawashukuru sana nyote na sasa wakati umefika tukapumzike ili jioni tuje kumaliza shughuli ya hoja hii na pia baadae kumkaribisha Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa ajili ya kufunga mkutano wetu huu wa tano.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa fursa jioni hii ya leo kuchangia hoja hii binafsi iliyoletwa mbele yetu na Mhe. Hamza Hassan Juma wa Jimbo la Kwamtipura. Mhe. Spika, kwanza na mimi napenda niungane na wenzangu kuiunga mkono hoja hii kwa sababu ni hoja muhimu kwa taifa letu.

Mhe. Spika, utakubaliana na mimi kama bila ya elimu huwezi kufanya kitu chochote, na kama wenzetu waliotangulia kuzungumza wamesema kama hata Mtume wetu Muhammad (S.A.W) kitu cha mwanzo kabisa alisisitizwa ni kusoma kwanza. Na yeye Mtume wetu Muhammad akatuhimiza na sisi kama tutafute elimu japo kama tutaikuta iko China. Kwa hivyo, mbele yetu ni muhimu vijana wetu na wao wapate suala hili la elimu, kwa maana hiyo katika nchi yetu hii ya Tanzania hasa Zanzibar kumeanzishwa Bodi hii ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wetu katika kutafuta hiyo elimu.

Mhe. Spika, na mimi nina masikitiko makubwa kutokana na Bodi hii ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa sababu kama tunavyojua nchi yetu umasikini ni mkubwa, na hilo nikiri kama Mwenyezi Mungu yeye mwenyewe anajua lini atatuepusha na umasikini huu. Kwa hivyo, ni kazi ya Mwenyezi Mungu lakini na jitihada yetu inatakikana kama lazima tufanye na jitihada na sisi wenyewe. Kwa sababu huwezi kusema tu kama mimi nitapata rizki ukalala ukamngojea Mwenyezi Mungu kwa sababu anateremsha rizki akuteremshie tu, ni lazima uitafute kwa kujituma.

Mhe. Spika, mimi ninachosikitika ni kwamba nasikitika kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa ajili ya kucheleweshe kuwapa mikopo wanafunzi wetu kwa ajili ya kutafuta hiyo elimu ya juu. Mhe. Spika, kwa kweli wanafunzi wetu walio wengi umasikini ni mkubwa na hawawezi kusoma bila ya kusaidiwa. Kwa maana hiyo serikali iliona kama kuna haja ya kutoa mikopo kwa wanafunzi hawa wa elimu ya juu, ili waweze kujikimu na waweze kuendeleza masomo yao.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, chakusikitisha ni kwamba Bodi ya Mikopo imechelewesha kuwapa watoto mikopo hali ya kuwa wanafunzi wameshindwa kusoma kwa sababu vyuo

vinajua wao unapofika muda wao wanasajili watu kwa ajili ya kwamba ajue kama mimi tayari nimeshapata kusoma. Kwa maana hiyo muda wao ulipofika wao wametangaza kama muda wetu ikifika siku fulani itakuwa ni siku ya mwisho ya kurejesha fomu, kama mtu hajaja kulipia na akachukua fomu basi itakuwa amekosa.

Mhe. Spika, kwa hiyo wanafunzi wamekwenda kuchukua fomu katika vyuo na mtu mmoja anatakiwa alipe dola, hivyo mwanafunzi huyo mwisho wake hakupata mkopo na yeye alikuwa hajui kama atakosa, tamaa yake yote alikuwa anajua kwamba mimi nitapata mkopo kwa ajili ya kujiendeleza. Kwa hivyo, wanafunzi hawawezi kujiendeleza kama hawakupata hii mikopo na wakati huku mtu ameshatoa fedha zake zaidi ya shilingi 600,000 au 1,000,000 kwa ajili ya kupata nafasi ya masomo.

Mhe. Spika, mwanafunzi huyo inakuwa hawezi kujiendeleza na fedha zake hizi za mwisho alizozitanguliza zimeshapotea, inabidi tunawasababishia wanafunzi wetu hasara kubwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naiomba serikali yetu kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ione kama kuna haja ya kukaa kitako na kurekebisha utoaji wa mikopo kwa ajili ya wanafunzi wetu mapema zaidi kabla ya vyuo kutoa siku za mwisho. Kwa sababu bila ya kufanya hivyo mheshimiwa inakuwa tunawasababishia wanafunzi wetu tokea hapo wana umasikini, halafu inakuwa tunawazidishia huo umasikini. Maana mtu ameshakwenda kutoa fedha zake na hawezi kujiendeleza kwa kujilipia masomo yake inabidi pesa zake zinakwenda ovyo, anakuwa kama popo si ndege wala si mnyama.

Mhe. Spika, naomba Bodi hii ya Mikopo ya Elimu ya Juu isiwe kama jungu la nyiza, jungu la nyiza linapwaga lakini halinekani moshi wala hulisikii kupwaga. Kwa maana hiyo na Bodi hii ya Mikopo isiwe kama jungu la nyiza kwa sababu iwe na uwazi ni kweli kunakiwa usiri, lakini ule usiri uwe na muda. Kwa hivyo, watoto bila ya kupewa mikopo mapema wakajua hivyo inakuwa tunawasababishia hasara kubwa.

Mhe. Spika, mimi namuomba Mhe. Waziri au naiomba serikali kupitia Wizara ya Elimu ikae kitako ili irejekebisho na ione kama kuna haja ya kutoa hiyo mikopo ili wale wanafunzi wajijue mapema kama mimi nimekosa ajue nini cha kufanya. Lakini kuliko kuwatia hasara halafu ikabidi pesa zao zinakwenda ovyo.

Mhe. Spika, suala jengine ni kwamba mimi namshukuru sana Mhe. Hamza kwa sababu nakubaliana na yeye kuhusu masuala aliyoyaelekeza kama lazima mfuko huu uchangiwe kwa hali na mali. Kwa hivyo, serikali ione kama kuna haja ya kuanzisha mfuko maalum kama alivyosema kaka yangu Mhe. Hamza wa kuwasaidia hawa wanafunzi ili waweze kusoma, kwa sababu kama tunavyozungumza bila ya elimu itakuwa hatuna tutakachokifanya. Mhe. Spika, sisi wazee wao wengine ndio tumeshakosa elimu, lakini na hawa watoto wetu wasije wakakosa elimu. Kwa hivyo, tunaijua nchi yetu ilivyo kama wanavyozungumza wenzangu sasa hivi tunaingia kwenye ushindani wa Afrika Mashariki, leo ikiwa watoto wetu tunawadumaza hii mikopo haipatikani basi itakuwa hawezi kuendelea.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu ni mfupi sana nimeona na mimi hoja itakuwa sikutenda haki kama sikutoa maneno yangu japo mawili matatu. Kwa hivyo, naunga

mkono hoja hii na ninawaomba na wenzangu wote tuiunge mkono na tuwatetee watoto wetu kwa hali na mali ili wapate mikopo waweze kujiendeleza kielimu na elimu ipatikane katika nchi yetu. Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu juu ya hoja ambayo iliyoikabili Baraza hili lako tukufu. Mhe. Spika, pia napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kuleta hoja hii mbele ya Baraza kwa ajili ya mjadala jambo ambalo sote tunaliunga mkonio.

Mhe. Spika, hii ni hoja ya binafsi ambayo iliyotolewa na Mhe. Hamza juu ya mkopo wa elimu ya juu. Mhe. Spika, suala hili linawakabili wanafunzi wetu waliofanya mtihani kuelekea Vyuo Vikuu mbali mbali ndani ya nchi na nje ya nchi halikadhalika. Suala hili Mhe. Spika, ni kubwa sana, ni zito na linahitaji ufumbuzi kusema kweli. Kwa hivyo, hili suala liko mbele ya Baraza lako tukufu hivi sasa tunalijadili, na *inshaallah* ndani ya Baraza hili hii leo tutaweza kupata ufumbuzi ambao ufumbuzi huo tunategemea utaleta kheri ndani yake.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tangu mwaka 1964 hadi hii leo imejitahidi sana, imeendeleza elimu Zanzibar kwa visiwa vyote viwili kuanzia elimu ya msingi hadi elimu ya sekondari. Tunamshukuru Mhe. Waziri aliyepita kwamba alifanya kila bidii Mhe. Haroun Ali Suleiman ya kuisambaza elimu Zanzibar kila mahala, elimu ya msingi, elimu ya sekondari mpaka elimu ya Vyuo Vikuu. Kwa jitihada zake alizozipitisha nahisi kwamba Mhe. Waziri alifanya jambo kubwa na la kheri katika nchi hii kwani vyuo vingi vimefunguliwa hapa Zanzibar ambapo kabla yake vyuo vikuu vilikuwa hapana, sasa hivi ndani ya Zanzibar hii tuna vyuo vikuu vingi sana.

Mhe. Spika, katika suala zima la wazee tunawashukuru sana wazee pamoja na walezi wa watoto wetu kwa jitihada zao katika kuisaidia serikali. Nathubutu kusema kwamba wazee ndio waasisi wa skuli zote za msingi Pemba na Unguja kwa sababu wazee walipania katika kutanua elimu bila ya kuisubiri serikali iwafanyie. Kwa hivyo, ni jambo la kuwashukuru sana wazee wetu na wazee hawa walikubwa na misukosuko mikubwa sana kwa ajili ya kuwasaidia watoto wao kutoa ada, hata *uniform* za skuli vile vile wazee walifanya kazi kubwa sana kuwasaidia watoto.

Kwa hivyo, kama hii ni hali yenyewe ambayo iliyokuwa wakati ule tunasema kwa kifupi kwamba wazee walikuwa na mwamko wa elimu. Sasa kutokana na mwamko huu wa kielimu hawakufanya kama wanavyohisi wao, lakini walifanya kwa sababu ya matumaini ya baadae na ndio maana msingi ule waliouchimba wazee kuanzisha elimu ya msingi mpaka elimu ya sekondari na mpaka ya vyuo ni kwa sababu walijipanga wazee kuanzia chini kwenda juu. Na walifanya hivyo kwa makusudi ili wapate matumaini mazuri ya baadae, na matumaini yenyewe ya baadae ni haya ambayo leo tunayazungumza hapa ndani ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, suala hili ni muhimu vijana wamefanya mtihani ambao matumaini ya kufanay mtihani huo kuelekea katika vyuo mbali mbali vya Zanzibar na nje ya Zanzibar.

Matokeo ya wanafunzi tumeyaona kwamba wamefanya jitihada wamepatikana wanafunzi 1,330 ili waweze kupata mikopo waweze kujiendeleza na elimu yao. Lakini kutokana na wanafunzi wote hao 1,330 waliobahatikana kupata mikopo ni wanafunzi 300, jambo ambalo hili linatusikitisha sote. Kwa hivyo, waliobakia ni wengi sana kuliko wale waliofaidika na mkopo huo.

Mhe. Spika, mimi niseme kwamba hiki ni kilio tena kikubwa sana, kilio hiki tunawapa pole wazee wote na walezi wote kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi ambao wamekosa mikopo katika Serikali yao ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo, wazee wamo ndani ya masikitiko na majonzi makubwa, walezi wamo ndani ya masikitiko makubwa sana, walimu wao waliowasomesha wanafunzi hawa wana masikitiko makubwa sana na Baraza la Wawakilishi halikadhalika liliopo hapa tuna masikitiko makubwa sana. Hali ambayo na sisi inatufanya tuwaunge mkono wazee, wazazi na walezi wote kwa jumla kutokana na hali hii, hali ambayo ni ya kusikitisha. Mhe. Spika, si hao tu mpaka wafanyakazi wa serikali pia wanawaunga mkono kutokana na suala hili ambalo unaliona taifa hapa tunaliwacha mkono.

Mhe. Spika, nataka nichukue fursa hii kusema kwamba hao wanafunzi mpaka kufikia hatua hii ya leo wakapata nafasi kutaka kuingia katika Chuo Kikuu wamesoma katika hali ya mazingira magumu sana, mazingira haya ambayo yanasababisha na wazee wao kwamba wamefunga mkanda kulipa ada zote kila mpaka hadi kufika hapa. Mhe. Spika, leo wanawaambia watoto kadha wa kadha wameshindwa kupata mkopo hicho si kilio kwa wananchi na sisi sote.

Mhe. Spika, mimi namuuliza Mhe. Waziri kilio hiki cha wazee pamoja na walezi wa watoto hawa utawanyamazisha vipi, kwa sababu ni suala ambalo linazungumzwa mitaani kila pembe ya Zanzibar hii linazungumzwa suala hili, watoto wamo ndani ya masikitiko na majozi makubwa sana hali ambayo sisi sote tunajua kwa jumla kwamba iwapo watoto wetu wataweza kufaidika kielimu hili ni jambo zuri kwa taifa letu. Mhe. Spika, ni kwamba idadi ya wanafunzi 300 kusema kweli ni kidogo sana kati ya wale 1,630, na tuelewe au wizara ielewe kwamba dhamira ya kutoa elimu hii kuna namna mbili. Mhe. Spika, tukiwapa watoto wetu elimu ama tutaweza kuwachukua tuwaajiri wao ili kuliendeleza taifa hili au katika elimu ambayo wataopata watoto hawa iweze kuwasaidia wao wenyewe binafsi yao. Lakini kutokana na hali hii inaonesha kwamba watoto wengi wameanguka chini hawakuweza kupata mikopo hii.

Mhe. Spika, kama ingelikuwa watoto hawa walipata nafasi ya kuweza kujiendeleza vyuo vikuu, naamini katika nchi yetu tungeliongeza marudufu ma-*engineer* kwa wingi, madaktari kwa wingi, walimu wazuri wazuri kwa wingi, wahandisi wa barabara kwa wingi hasa katika suala zima la ufundi ambalo ni taaluma ya pekee, hili lingeweza kuwasaidia watoto wetu bila ya kutegemea kazi za serikali wangeweza kujiajiri wao wenyewe. Mhe. Spika, tunajua faida ya elimu sote kwamba elimu ndio msingi wa maendeleo, ndio ufunguo wa binadamu katika jitihada zake zote, na tunasema *any human being is progressive*. Kwa hivyo, tukimnyima hii hali kwamba binadamu yeyote ni maendeleo hatuoni kwamba sisi tunafanya vibaya kwa taifa hili.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme katika Wizara ya Elimu hili suala la mikopo kwa wanafunzi si suala la kutegewa tegewa au kufanywa kama ni *allahu ya alam* au kama hivi maamuzi yalivyotoka kwamba kutoa idadi ndogo ya mikopo na wengi wakabakia bila ya mikopo. Mhe. Spika, hii itakuwa si haki hata kidogo, na mimi hapa nasema wizara hakuwa makini nalo, hawakuwa na hali ya kuona kwamba hili suala ni muhimu tutoe kipaumbele kwa hali yoyote na kwa fedha yoyote tuangalie kila mahala tuweze kupata fedha ya kutosha ili angalau asilimia 60 au 70 ya wanafunzi wale hizo kelele zisingekuwepo. Mhe. Spika, mimi nataka niambie Wizara ya Elimu kwamba kwa hivi sasa kelele ni nyingi kwa sababu ukienda katika *percentage wise* 300 ni kidogo sana. Kwa hivyo, ni lazima wazee watapiga kelele katika nchi hii.

Kwa hivyo, kama Wizara ya Elimu wangeweza kufanya utaratibu hapa tulipofikia wakaweza kuongeza idadi ya wanafunzi kuweza kupata mikopo ingekuwa ni jambo la busara sana. Lakini bado wizara hii haijachelewa kwenye suala hili, itafute mipango na utaratibu wowote ili tuongeze idadi ya wanafunzi ili waweze kupata mikopo na waweze kuendelea na elimu yao.

Mhe. Spika, kama sio hapo tu katika Wizara ya Elimu basi tuweze kukubaliana sote kwa ujumla kwamba hali yenyewe ni hivi ndivyo inavyojitokeza. Kwa hivyo, tuweze kuziambia taasisi zote za serikali au wizara zote ziweze kutoa mchango wao kusaidia suala hili. Lakini mimi sitaki nione kwamba hili suala tumelizungumza leo hapa halafu tukaliweka nyuma ya mgongo, hii itakuwa si haki hata kidogo. Mhe. Spika, ni lazima wizara izungumze na taasisi nyengine iweze kusaidia mchango ili angalau ile *percentage* iweze kuwa nusu ya pale au zaidi ya pale. Kwa hivyo, taasisi tunazo nyingi kila wizara tunaweza tukasaidia hili suala, wafanyabiashara halikadhalika vile vile washajihishwe waweze kusaidia wanafunzi hawa kuweza kuwasaidia mikopo.

Mhe. Spika, naamini kwa mujibu wa bajeti yake wizara labda imeona hicho ndio uwezo wake, lakini haikuangalia nini matokeo baada ya idadi ndogo. Mhe. Spika, kama wizara ilikaa kitako kutokana na idadi kubwa na waliopata ni idadi ndogo pengine wangelifikiria wakaona hii idadi ni ndogo lazima tuwasukume ipatikane idadi kubwa. Kwa hivyo, wafanyabiashara na wao wasiachiliwe na wao katika maelezo yetu haya tangu asubuhi bila shaka watakuwa wametusikia na wao wana haki ya kulisaidia taifa hili. Kwa sababu taifa hili halijengwi na mtu mmoja, sote sisi tunatakiwa tulijenge taifa hili kama ikiwa wewe ni mfanyabiashara, ikiwa ni mwalimu, ikiwa ni mfanyakazi, ikiwa ni daktari sisi tunahamu kwamba unapokuwa wewe unasoma katika skuli yako basi umepata nafasi ya kupata nafasi kubwa ukitoka nje na Mwenyezi Mungu akakujalia rizki kubwa, basi lazima unarudi katika skuli yako kuisaidia.

Kwa hivyo, kwa nini tusiwe na huruma hizi iwe walimu tu waliowasomesha watoto hawa ndio wenye huruma, lakini waliobakia wote si wamesomeshwa na walimu, walimu wanalia hivi sasa kwani kilio ni kikubwa sana. Kwa hivyo, mimi naona kuwanyamaza hawa waliofanya kazi wakaona hii haki yao haikupatikana, kwa hivyo wenzetu ambao waliosoma na wakamaliza maskuli wana haki ya kusaidia na wafanyabiashara wana haki kusaidia na tasisi zote za serikali ziweze kusaidia katika suala hili.

Mhe. Spika, sasa nazungumza na Wizara ya Fedha tunajua kama bajeti yake ambayo inayokwenda Wizara ya Elimu ni ndogo, na Wizara ya Elimu ni wizara mama kwani ni moja katika wizara kubwa sana. Pia inahitaji kupewa uangalifu wa hali ya juu kwa sababu ni wizara ambayo ina matawi mengi sana, ina wafanyakazi wengi sana na ina mahitajio mengi sana. Kwa hivyo, ningeliomba wakati wanapokaa Makatibu Wakuu wa wizara kujadili masuala ya bajeti ya mawizara mbali mbali hebu iipe kipaumbele baina ya Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu kwani hizi ni wizara mama mbili ni wizara muhimu sana. Mhe. Spika, ndio maana kila siku hapa tunaizungumza Wizara ya Afya hivi na hivi lakini kipaumbele kinachochelewa wakati wa bajeti inakuwa ni ndogo sana. Kwa hivyo, mimi nafikiri kwa upande wa elimu nao Waziri wa Fedha ana mchango mkubwa sana hasa leo alikuwepo tangu asubuhi akisikiliza na hivi sasa nafikiri yupo anaendelea kusikiliza, basi tuone angalau kasma ya ya mara hii ni nzuri sana.

Mhe. Spika, naamini kwamba Baraza lako tukufu kwa hali hii ya leo katika mazungumzo haya ni muhimu sana na mimi nathubutu kuwaambia wenzangu tukae tulifikirie hili suala, kwani ni suala muhimu na lisipuuzwe. Mhe. Spika, kwa sababu ikiwa hatukutoa maamuzi kwani unapozungumza mwisho wa kuzungumza ni nini? Mwisho wa kuzungumza ni kutoa maamuzi, kwa hivyo, na sisi tunahitaji kutoa maamuzi kwenye suala hili, tunasemaje juu ya suala hili. Je, tunaliacha hivi hivi kama ilivyoamuliwa au kunahitajika kitu chengine cha Baraza kuweza kuamua katika suala hili.

Mhe. Spika, mimi niwape pole wanafunzi wote wale ambao hawakubahatika kuweza kupata mikopo hii, naamini watoto hawa hawakufurahi wako katika majonzi na masikitiko makubwa sana. Lakini kwa sababu suala limefika mbele ya Baraza na sisi tuna imani kubwa sana kwamba ndani ya mazungumza yetu leo tutafikia mahala pazuri ili kuweza kuwasadia wanafunzi wetu waliobakia ambao hawakuweza kupata mikopo hii.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu japo kwa kidogo, lakini nafikiri umefahamika. Mhe. Spika, mimi binafsi yangu naunga mkono hoja hii mia juu ya mia, ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa fursa hii na mimi kuchangia hoja hii. Kwa kweli kwanza nimshukuru Mhe. Mwakilishi aliyeleta hoja hii katika Baraza lako tukufu, niseme kwamba ni mkereketwa wa elimu katika nchi yetu. Kwa kweli hoja hii ni ya msingi sana na tunaombwa tuizingatie kwa kima kikubwa kwani elimu ni muhimu na elimu ni ufunguo wa maisha. Mhe. Spika, tuliambiwa kama wanadamu basi tutafute elimu hata Uchina.

Mhe. Spika, suala hili na mimi limenigusa sana kwa sababu na mimi ninao vijana wangu katika Jimbo la Amani ambao wamehamasika na kutafuta elimu. Mhe. Spika, ni jambo la kuzingatiwa sana kwa sababu vijana hawa kwa mujibu wa ripoti hii ya Mhe. Hamza walifikia maamuzi ya kutaka kufanya maandamano. Mhe. Spika, tumeona ni namna gani *new generation* sasa hivi zimekuwa zinapashana habari na mambo mengi kupitia hii mitandano ya kijamii. Kwa hivyo, hili ni suala ambalo la kuzingatiwa sana kwani kuna hii mitandao ya kijamii ndio inayowapelekea hata kule nchi ya Tunisia na nchi za Arabuni kuleta machafuko. Kwa hivyo, hili ni jambo la kulizingatia sana.

Mhe. Spika, mimi niseme kwamba Wizara ya Elimu ni lazima iandae mikakati kuhusu suala hili. Vile vile niseme kwamba wizara hiki kidogo kinachopatikana basi hiki hiki kigaiwe kwa mujibu wa kutokuwa na ubaguzi. Wenzangu walisema hapa kwamba unapita ubaguzi lakini sio vizuri na mimi ninukuu yale maneno ambayo wakisema viongozi wetu, bora kuwa na chakula kidogo tukagawana kidogo kidogo, kuliko kuwa na chakula kingi tukaanza kukigombea. Kwa hivyo, hiki kidogo tulichokuwa nacho basi tuwajulishe vijana wetu watakuwa ni wasikifu angalau basi wote wafaidike na kile kidogo ambacho kipo.

Mhe. Spika, kwa kweli kama ulivyokwishakusema kwamba wakati ni mdogo na kuna wenzangu ambao wanataka kuchangia na mimi ili nisiwe mchawi wa suala hili, kwa sababu asubuhi tulisema hapa atakayekuwa hakuunga mkono hoja hii atakuwa ni mchawi. Kwa hivyo, nasema kwamba na mimi nimechukua fursa hii ya kuichangia hoja hii binafsi kuhusu mkopo wa elimu ya juu.

Mhe. Spika, naiambia Wizara ya Elimu sasa ni wakati wa kuanzisha kozi mbali mbali, na vile vile tuwashirikishe hizi Jumuiya za Kimataifa ambazo zinaweza kutusaidia na wako tayari kutusaidia kwa watoto wetu ili kuzidisha elimu. Kwa hivyo, nafikiria na wao Wizara ya Elimu wajitahidi kuwatafuta hawa washirika wa maendeleo ili watusaidie.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi sina mengi sana na kwa sababu wakati unakwenda na wenzangu wanataka kuchangia, mimi niseme kwamba naunga mkono hoja hii ya Mhe. Mwakilishi mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Salim Haji: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kupata nafasi hii ya jioni kuweza kuchangia hoja binafsi iliyowasilishwa na Mhe. Hamza Hassan Juma wa Jimbo la Kwamtipura.

Mhe. Spika, niseme kwamba na mimi kama nisingesimama hapa kuchangia hoja hii, basi nisingetenda haki kwa sababu miongoni mwa watu ambao walioweza kukutana na vijana hawa pale *university* na mimi nilikuwa ni miongoni mwa Waheshimiwa ambao tulikwenda kuzungumza nao, kuona ni namna gani wale vijana tunawaelekeza na tunawafahamisha katika kufahamu taratibu za kudai haki zao za msingi. Mhe. Spika, hatimae niwashukuru vijana wale kwa dhati kabisa kwani ni wanafunzi ambao waliamua kutukubalia kusitisha maandamano na kukubali kuwa watavuta subra, ili kuisubiri serikali yao kuwasaidia kwa namna moja au nyengine kuondokana na kadhia hii.

Mhe. Spika, kuna mambo duniani basi iwe mwanadamu, iwe Mwenyezi Mungu basi mambo haya yamekuwa *priority*, hususan mambo matatu nayo ni elimu, afya na mengineyo. Mhe. Spika, ndio maana muasisi wa nchi hii Mzee Amani Abeid Karume baada ya mapinduzi matukufu akatangaza baadhi ya vituo hivi ameviweka kuwa serikali ndio itakuwa inawasaidia wananchi wake. Mhe. Spika, kuhusu suala la afya kila mtu anaumwa, suala la elimu kwa kweli kila mtu anahitaji elimu na wanaohitaji wanakuwa hawana nyanja maalum, iwe masikini na iwe tajiri.

Mhe. Spika, kutokana na umuhimu huo basi ndio ikaonekana kwamba vitu hivi serikali iwe inavibebea mzigo tangu vilianza katika hatua ya bure, mpaka sasa hivi tumekuwa tunaingia katika hatua ya kuchangia kutokana na mazingira ya dunia vile yalivyo lazima yachangiwe. Lakini pamoja na hali hiyo lazima tukiri kwamba hali ya Wazanzibari walio wengi ni masikini, na hakuna watu ambao wanaweza kumudu kwa asilimia zote kuweza kuyatekeleza haya.

Mhe. Spika, mshahara wa kima cha chini cha mfanyakazi wa Zanzibar ni shilingi 120,000 kwa mahesabu ya haraka haraka kwa familia zetu za kawaida ni pesa ambazo mtu au fedha hizo zinaweza kutosheleza mlo wa siku 10. Kwa hivyo, ikiwa mlo wa mwezi pesa hizo basi hazimtoshelezi, lakini leo wanaambiwa wazee wasaidie kuwasomesha watoto wao. Mhe. Spika, hili suala linakuwa ni gumu sana na ndio maana nasema kwamba hata serikali yetu ndipo ilipoandaa utaratibu wa kuunda bodi na kuunda vyombo vyengine vya kuweza kuwasaidia vijana hawa. Mhe. Spika, kilichojitokeza hapa ni kwamba pamoja na hali yote lakini kuna mazingira ndio yaliyofikisha hapa, na ndio yaliyofikisha vijana wetu kujihisi kwamba wamewekwa pweke na wamewekwa wanyonge. Mhe. Spika, laiti wewe ungelikuja katika hicho kikao basi ungekuwa katika hali mbaya, kwa sababu vijana walisema mwisho walikuwa wanalia machozi, baada ya kuwasikiliza kwanza tulifanya kazi ya kuwabembeleza.

Mhe. Spika, muda wa mwezi mmoja au mwezi mmoja na nusu mtu amepeleka maombi anasubiri majibu akiwa na matarajio ya kupata mkopo, unamwambia kwamba hakufanikiwa lakini ndani ya mwezi mmoja na nusu tufikirie ni mtu wa aina gani na mnyonge gani anaweza kupata pesa za kwenda kujisomesha. Kwa hivyo, hapa nalo tatizo ilikuwa ni muda, hata Mhe. Naibu Waziri alifika kusema kwamba kulikuwa kuna tatizo.

Mhe. Spika, mimi niseme kwamba mengi yamezungumzwa mimi nilitaka nisimame ili vijana waone kwamba yale tuliyoyaahidi tumeyatekeleza kwa vitendo. Mhe. Spika, njia ya kuzisaidia suala hili ziko nyingi, na nina imani kwa serikali hii ninavyoifahamu kwa upendo waliokuwa nao kwa wananchi wake, nina imani watakaa, watavuta fikira zao kutafuta busara ili tatizo hili liweze kutatuliwa. Mhe. Spika, nina imani kwamba hili linawezekana.

Mhe. Spika, ni kwamba tuna mashirika mengi ya binafsi yanasaidia vitu mbali mbali, hivyo ningeiomba serikali itafute mbinu ya kuzungumza na vyombo hivyo ili kuweza kulitatua tatizo hili. Mhe. Spika, juzi tu kuna fununu kwamba Kampuni yetu ya *Seagull* imeamua kudhamini *league* ya Zanzibar sasa hiyo ni kampuni moja, nina imani kwamba kampuni hii ilikuwa na uwezo huo basi ushawishi kama utapita, basi nina imani mashirika mengi nayo yataweza kusaidia ili kutunusha mfuko wetu kuweza kuwasaidia vijana wetu katika suala muhimu la kupata elimu.

Mhe. Spika, tuliangalia upande mmoja tu lakini upande mwengine hatukuangalia, serikali yetu mara nyingi tunapiga kelele kwamba vijana wasome, na wakisoma tunawafanyia mahafali makubwa na tunawazawadia mazawadi makubwa makubwa. Vile vile serikali yetu ilipiga hatua kubwa kwa kujenga vyuo vingi, lakini tulijisahau kwamba tunapohimiza kujenga vyuo vingi basi na wanafunzi watakuwa wengi. Kwa hivyo, huko

ilikuwa hatukujipanga, lakini nina imani sasa hivi kutokana na hali halisi basi serikali itajipanga na ione namna gani inawasaidia vijana wa wanyonge wasome ili wapate matarajio ya baadae.
Mhe. Spika, moja katika adhma ya kutaka kuonesha dhamira ya kuonesha kadhia hii, wenzangu wengi waliozungumza wameeleza jinsi gani ya kujitolea kupitia mfuko wa majimbo kuamua kuzipeleka katika majimbo yetu. Mhe. Spika, kwa sababu hawa vijana wanatoka katika majimbo yetu, mimi katika jimbo langu nina rekodi ya wanafunzi hata idadi hawana kwani kila siku huko nyumbani hawaondoki wanataka wasaidiwe kusoma. Mhe. Spika, mimi naunga mkono nao kuona kwamba mfuko wa jimbo milioni 10 tunaunganisha ili tuanze harambee ya kuwachangia vijana hawa katika kuondosha kadhia yao.

Mhe. Spika, mwisho niseme kwabma na mimi naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Spika, alaasiri hii na mimi kunipa fursa ya kuzungumza machache kuhusu hoja iliyoko mbele yetu. Mhe. Spika, mimi nataka nianze kwenye suala la *fund rising*, hoja hii imependekeza kwamba ili kupata fedha tufanye kitu kinachoitwa *fund rising*. Hili ni suala zuri sana.

Mhe. Spika, lakini ninachokumbusha tu ni kwamba hii imo katika *function* za bodi ambayo hivi karibuni tuliipitisha katika Baraza letu tukufu. Kwa hivyo, chakufanya hapa labda itakuwa hawa watu wako wamelala, hivyo huyu ambaye anashughulikia mfuko huu sasa ameshaona kwamba mapambano yanamuelekea kwa hivyo sasa hii kitu aifanye kabla hatari haijatufikia.

Mhe. Spika, hivi sasa tumepata ishara mbaya sana na hii inayonipelekea kusema labda kwamba katika bajeti zetu tunakuwa hatuko makini kwa utungaji wa zile bajeti, kwani kama sisahau moja katika vipaumbele tulivyoviweka ni elimu. Lakini sasa hivi chakushangaza ni kwamba kipaumbele hiki tumekiwekea fungu dogo sana na matokeo yake huu ni mwezi wa tatu baada ya kumalizika bajeti. Lakini sasa wananchi wanataka kuandamana kwamba hakuna kitu tena kwenye karai kumeshamalizika na hatuna njia nyengine yoyote ile.

Mhe. Spika, mimi ninachosema kwamba ikiwa tumeshasema kuwa hiki ni kipaumbele basi kiwe ni kipaumbele tuweke fedha ambayo angalau itafika nusu ya yale tunayoyatarajia. Mhe. Spika, lakini juu ya hayo pia inavyoonesha kwamba Wizara ya Fedha na Wizara ya Elimu hazikuwa hata na matarajio kwamba sisi mwaka huu tutaingiza wanafunzi fulani katika vyuo vyetu. Labda hii ndio iliyowapelekea kutenga fedha finyu sana kwa ajili ya wanafunzi watakaoingia vyuoni, kwa hiyo miaka inayokwenda inatuonesha kwamba tunatakiwa tuwe makini katika hili, na Wizara ya Elimu ijue kabla kwamba mimi mwaka wangu huu nitakuwa na wanafunzi fulani katika fani fulani.

Mhe. Spika, katika kuomba unakwenda Wizara ya Fedha *ceiling* kama wataipunguza niweze kuwakumbusha kwamba sisi *vision 2020* inasema kipaumbele ni hiki. Kwa hivyo,

kwa nini unakipunguza mpaka kifikie lengo hilo, kwa maana hiyo hivi sasa Wizara hii ya Elimu inatusomesha mpaka kidato cha sita, lakini anayetaka kuingia Chuo Kikuu tayari ameshakuwa *blocked* anaambiwa wewe sisi hivi sasa hatusomeshi watu ambao wanataka kuingia Chuo Kikuu wakipitia fani za lugha za Kiarabu, Kiswahili na Art. Mhe. Spika, hii ina maana kwamba sisi hatujajipanga bado kwa nini tumsomeshe mpaka huku na awe na uwezo wa kuingia Chuo Kikuu, baadae tuje tum-*block* hapo kati kati. Hivyo atakuwa hana haki huyu mtu ya kuingia Chuo Kikuu basi atatudai na kesho ataandamana kweli. Kwa hivyo, sasa ni juu ya wizara kuwa na mpango kazi ambao utatuanishia sisi tunataka kusomesha kwa kipindi hiki watu wa aina fulani. Mhe. Spika, hivi sasa kuna taarifa kwamba wanaotaka kuingia Chuo cha Chwaka mkopo upo lakini wanafunzi hamna. Mhe. Spika, ni kwamba ile *system* yetu ya kusomesha haiko vizuri. Kwa hivyo, mimi ningeiomba wizara nayo ikajua nini inachokifanya kabla ya kufika kulaumiana hapa kwamba huyu hivi, huyu vile.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kusema ni kwamba wengi hapa wamechangia au wametoa mawazo kwamba ili kuokoa jahazi basi mfuko wa *CDF* upelekwe huko. Kwanza mimi najiuliza hii *CDF* iko wapi? Hatuna, sasa hatujajifunza hata sisi kutembea tufanye vipi tayari unasema mfuko wa CDF upelekwe huko, utapelekwaje zipo kwani, hazipo. Lakini ukiachia hayo kwa nini mfuko huu tuupeleke huko, si tumeupanga kwa sababu nako kuna vipaumbele.

Mhe. Spika, katika mfuko wa CDF sisi tuna shughuli nyingi za kufanya na ndio maana ukawekwa huo, tukiondoa elimu sawa ni kipaumbele, lakini kuna kipaumbele chengine cha maji, cha hayo maskuli. Mhe. Spika, kabla ya mwanafunzi kufikia katika lengo hilo la kwenda Chuo Kikuu anapita *preparatory school* anaandaliwa huyu, na maandalizi yake yanahitaji fedha. Mhe. Spika, yeye anakwenda skuli anayechangia kujenga skuli ile ni sisi kwa mfuko huu huu. Pia yeye anataka walimu kwa taarifa yako sisi wengine katika majimbo yetu tunachukua walimu kutoka Vyuo Vikuu kwa ajili ya kwenda kusomesha wanafunzi ili waweze kupasi vizuri katika mitihani yao.

Mhe. Spika, nakupa mfano hai ulionikutia juzi, nimefanya *write up* na baada ya kufanya *write up* nikaomba hawa ambao wanatusaidia siku zote. Bahati nzuri nimefanikiwa na nimeomba vifaa vya *laboratory*, lakini walinipa masharti kwamba mimi au sisi hatutoweza kuleta hili mpaka tuone mazingira mazuri katika sehemu yako. Inatakiwa chumba kiwe hivi na hivi, namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba Wabunge wao wameshaupata huu mfuko.

Mhe. Spika, nilimwambia Mbunge wangu *please* atayarishe shilingi 3.5 milioni kwa ajili ya kutayarisha hicho ili hawa wafadhili sisi watuwezeshe kutupatia hivi vitu. Mhe. Spika, kama ingelikuwa hii pesa ya Mbunge haijafika basi Mhe. Spika, tungeliadhirika kwa sababu huu msaada tungeliukosa. Kwa hivyo, mimi ninachokisema labda serikali iandae mpangilio mwengine na sio sisi tuseme hizi pesa kwani hizi pesa bado zinahitajika katika majimbo yetu.

Mhe. Spika, sambamba na hilo ni kwamba inaweza baadae ikaleta fitna, mimi nawezekana pengine katika jimbo langu sina mtu yeyote yule ambaye kaingia chuoni

kwa muda wa miaka miwili. Mhe. Spika, basi wapiga kura wataniuliza hivyo hizi pesa zetu za CDF ziko wapi, nitawaambia aa mimi hizi ninazo katika mkoba, nimeziweka kwa sababu tunachangia mfuko mkuu. Hivyo hawatakubali kwa sababu mimi sikutoa mtu. Kwa hivyo, ili kuondoa hayo na kuja kunikosesha labda mara nyengine nisije hapa, mimi nahisi serikali iandae mpangilio mwengine wa kutafuta pesa wa kuingiza katika mfuko huu. Nafikiri pesa zipo.

Mhe. Spika, mimi kumbukumbu yangu kwamba serikali katika miaka ya 2000 ilikuwa na matatizo makubwa ya barabara, ikasema kwamba sisi ili kutatua tatizo letu hili la barabara tuandae utaratibu maalum wa kutafuta fedha ili kuzikarabati au kuzitengeneza barabara zetu. Mhe. Spika, utaratibu huu ulitujumuisha wananchi wengi hasa tuliokuwa na magari, na ikasema kwa kila mwenye kwenda kununua mafuta kwa kila lita atalipia shilingi mia. Mhe. Spika, ikiwa tuko makini kwamba sisi kweli tunataka vijana wetu waliokuwa hawakupata fursa ya kwenda kwenye masomo, basi na utaratibu huo tuuandae tuseme tu kwamba sasa ni shilingi 50 hivyo tuiweke kwa ajili ya mfuko wa kusomesha vijana wetu.

Mhe. Spika, mimi nasema kwa hayo machache juu ya kwamba nimekwenda huku na huku naunga mkono hoja hii.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii, mimi kwanza naomba kumpongeza Mhe. Hamza Hassan Juma kila mtu amempa sifa zake Mhe. Hamza wanamjua wapi, mkereketwa wa chama. Mhe. Spika, asubuhi Mhe. Ismail Jussa Ladhu alikutaja wewe kwamba ni Muumin wa serikali kwa unavyojitahidi, na mimi nathibitisha hilo wewe ni muumini kwa maneno, maneno yako uliyoyatoa wakati ule ni ushahidi kamili kama ni muumini na leo hapa tuko na Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, hii hoja ya Mhe. Hamza ina mapendekezo aliyoyatoa mheshimiwa. Mapendekezo aliyotoa mheshimiwa Mhe. Spika, naomba pendekezo la kwanza serikali iweke wazi *account* yake ya Mfuko wa Elimu ya Juu Zanzibar mtu, taasisi yoyote anayetaka kuchangia achangie hata kama yuko nje ya nchi. Hapa *account* hii ipo ndani ya sheria, sheria yenyewe Mhe. Spika, ilipitishwa ndani ya Baraza lako hili na ikatiwa saini na Mhe. Rais tarehe 01 Julai, 2011 *page* 17 ya sheria inazungumza *establishmen of the fund uwepo* mfuko huu. Kwa hivyo, mfuko huu upo, lakini na sheria ya mwaka 2001 tuliyoipitisha katika Baraza la Wawakilishi nayo inasema hivyo hivyo iwepo *source of the fund*. Kwa hivyo, hili serikali ni kuikumbusha halitaki maamuzi, kwa sababu sheria ipo na mfuko upo.

Mhe. Spika, kuhusu hoja ya pili ni kwamba serikali iandae *fund rising* na mgeni rasmi awe ni Mhe. Rais na makamo wake wote wawili. Sheria inasema *fund rising* mheshimiwa utanistahamilia kwa sababu tusaidie saidie unajua mimi nimekuja juzi ndio najifunza funza hivi. Ni kwamba inazungumza kwamba bodi ile ina mamlaka ya *fund rising*, na sheria iliyopita inazungumza *fund rising*. Kwa hivyo, hili lipo linataka kukumbushwa tu halitaki maamuzi kwa sababu *fund rising* ifanywe na Rais afanye halitaki maamuzi.

Kuhusu hoja ya tatu ni kuliomba Baraza lako tukufu lichukue fedha, sasa hapa sheria imetengeneza *source of fund* namna ya kukatwa pesa. Mhe. Spika, mwaka 2001 tuliweka kanuni tukasema kila anayejitia *ZRB* na kwengineko kwa hiyo kitu cha muhimu ni kwamba sheria ipo isipokuwa zitafutwe *funds* kama tulivyokubaliana mwanzo, na sasa hivi sheria hii iwe na utaratibu wake. Mhe. Spika, kwanza katika sheria inataka kila mwanafunzi anayesomeshwa atakaporudi alipe zile pesa na vile vile mfano tatizo letu kwenye *fund* mwaka 2001 tulikuwa na mfuko huu, na mimi kwa taarifa yako mheshimiwa kwa miaka 9 nimekuwa Mjumbe wa Mfuko wa Elimu ya Juu uteuzi. Ni kwamba mfuko hata mara moja haujatiliwa *fund* wala *affect* haijafanywa ile Bodi ya Mfuko wa Juu. Mimi nilikuwa Bodi ya Mfuko wa Uteuzi sasa bodi hii sheria imeshawaambiwa wafanye *affect* za kupitisha *fund*.

Mhe. Spika, mara nyingi sheria tunazozipitisha ni kwamba hatuzifuati, na *fund* zipo. Mhe. Hamza alimwambia Mufti kwamba tuliwahi kupitisha sheria ndani ya Baraza hili tukufu kwa kuwa kila mwenye nyumba ya kukodisha anatakiwa alipe *percentage* fulani, kila ambaye ana nyumba ya biashara tumepitisha, tumezozana pale, lakini kimya fedha zipo zitafutwe.

Mhe. Spika, jengine ambalo limeamuliwa hapa ni suala la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba tuombe *ratio*, mimi huko sitaki. Kwa nini sitaki? Ni kwamba elimu ya juu ukisoma mambo ya Muungano utakuta yako 14, katika mambo asili ya muungano elimu ya juu hamna. Lakini hii hapa Katiba ya Tanzania elimu ya juu ni ya 14, lakini Mhe. Spika, kwa miaka 46 Serikali ya Muungano elimu ya juu haijapata kuleta senti moja Zanzibar hata tulipotaka kuanzisha *SUZA*. Mhe. Spika, unajua Mhe. Ali Juma Shamuhuna ndio waanzilishi na Mhe. Msabaha Mhe. Salmini aliwachagua hao kuanzisha namna elimu yote jitihada zetu za kujitegemea kwa sababu wenzetu wanatufanyia mambo hayana maana. Mhe. Spika, tulifanya juhudi *SUZA* ndio ikazaliwa, lakini tulipigwa, tulitaabishwa na mpaka leo *SUZA* senti moja ya Serikali ya Muungano haijatoa kusaidia.

Mhe. Spika, kwa hivyo sisi kwa nini tuliamua mwaka 2001 kuleta sheria ni kwa sababu mwaka 1992 Baraza la Mapinduzi liliunda kamati, kamati hiyo Mhe. Shamuhuna alikuwa ni Katibu. Mhe. Spika, katika mambo yaliyopendekezwa ni kwamba elimu ya juu iondoke kwenye muungano, mimi nasema kwa uhakika na ninazo nyaraka. Mwaka 2003 Baraza la Mapinduzi tena limetengeneza waraka kupeleka kule wakaomba iondoshwe, sisi wenyewe tumeona hawa hawaondoshi. Na mwaka 2011 sheria tumeipitisha hiyo ya elimu ya juu, sasa hivi elimu ya juu Mhe. Hamza alikumbusha kwamba tufanye juhudi.

Mhe. Spika, tukisema wanafunzi 1,630 wameomba mkopo katika wanafunzi 300 ndio wameanza kufadhiliwa masomo ya Phd na masters, mfuko umesema hawawezi hawana pesa. Lakini bado wanafunzi 1,300 hawajachaguliwa hawa ni wanafunzi wapya. Kwa hivyo, wanafunzi hao wapya tukachukua mfuko wa JK na AK, mfuko wa barabara, mfuko wa maafa, pesa za meli tupeleke zote huko wataweza kusoma. Mhe. Spika, mwakani hawa wanaingia *second year* kero ziko wapi, labda kila mifuko ikija basi tusiiguse. Lakini *source* zipo halafu tukae kitako Mhe. Hamza alitoa *guide line* kwa hiyo

sheria itazamwe na tuishughulikie na sasa hivi hapa hakuna serikali, sisi sote humu ndani Mhe. Spika, ni serikali.

Mhe. Spika, Mhe. Abubakar Khamis Bakary alileta hoja yake hapa, tukaiteka nyara tukaichukua sisi CCM, leo hii hoja ni yetu sote mwenzetu mmoja sisi *backbenchers* ameleta hoja, na serikali isiwe *desensive*, serikali ni yetu sote pamoja na mimi ni serikali ni uteuzi wa Rais, serikali hii ni ya umoja wa kitaifa. Na wale ambao wenye mawazo ya kizamani mimi nasema tukae pamoja tushirikiane sheria ipo na yote aliyoyasema Mhe. Hamza yamo. Mhe. Spika, haya ya *OIC* nimemsikia Makamo wa Pili wa Rais mimi nilikuwa sio mwakilishi anasema *OIC* imeshafungwa lakini sasa *OIC* tuingie lini? Keshokutwa? Watapata fedha wanafunzi hawa mpaka tuingie *OIC*, lakini serikali inazo *source* zake za fedha na serikali anayesimamia fedha ni rais, rais ndiye ni waziri wa fedha anaye waziri wa nchi anayeshughulikia fedha na sisi katika Mfuko wa Elimu ya Juu mwaka jana tulipeleka wanafunzi 900.

Leo nasikia sijui wizara ilikosea, ni (rais) sheni, serikali ya awamu ya sita tunaipongeza imepeleka wanafunzi 600 isiyokuwa na mfumo wa Mapinduzi ya Zanzibar. Hii ya sasa hivi Serikali ya Mapinduzi yenye mfumo, sasa hii imepeleka wanafunzi 300. Sasa lazima tushirikiane, lazima serikali ni wende hii sio hali ya mtu. Kwa hivyo, hayo ndio Mhe. Spika, niliotaka kusema.

Suala la mwisho kabisa kwa hayo niliyoyasema yote, sisi wenzetu hawa wa Jamhuri ya Muungano najibu hili suala la kuwa tupate *quota*. *Quota* Chuo Kikuu imeshafutwa haipo sasa, mimi Mhe. Spika, nilikuwa mjumbe wa *TCU* wanataka lazima waichukue *SUZA* sisi hatutaki kwa sababu hawatusaidii, sasa Mheshimiwa tumepata Mfuko wetu tuuendeleze kwa hali na mali. Vile vile tunapowapa hoja wanasema wao katika Mfuko wa Elimu ya Juu ule wao wanasema…

Mhe. Spika, tuliomba orodha sisi ya Mfuko wa Zanzibar tulitaka kujua wanafunzi wangapi wa Zanzibar wamesaidiwa kwenye Mfuko wakajibu hawana idadi hawajui. Kwa sababu wao hawatizami Zanzibar hawatizami Tanga. Sasa itakuwaje wasijue. Kwa hivyo, la muhimu sasa Mfuko wetu huu tulioupitisha juzi hapa ukatiwa sahihi tuupe nguvu, yale yote yaliokuwemo kwenye sheria yatekelezwe na japo kamati ndogo ya Baraza iundwe sio ya posho, iundwe kusaidia ule Mfuko na njia nyingi zipo za Mfuko, tutawasahauri tutawaambia.

Sasa Mhe. Spika, niliona hayo niyaseme kwa sababu Mhe. Hamza alisema hivi, ndani ya Baraza hili kuna wazee wenye busara na hekima na mimi nikaona nitumie hekima na busara zangu hizo ndogo ndogo ili niweke sawa haya mambo. Hili jambo zuri, tulizungumze, tulipokee na tulifanyie kazi. Ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii niweze kuchangia. Nitajitahidi kwenda kwa *point* ili niweze kumaliza kwa dakika zangu tano.

Mhe. Spika, kwanza mimi nishukuru sana kwa Mwenyezi Mungu kutujalia kupata pumzi zetu za leo. Pia nimsifu sana Mhe. Hamza Hassan Juma niseme kwa historia katika

Baraza hili kwa mara ya kwanza kuletwa hoja ya Mhe. Mjumbe na ikakubalika, hii ni historia peke yake tena itaandikwa.

Niende katika ukurasa wa nne, mwalimu wangu aliyekaa kitako sasa hivi alisema kuwa sheria ipo na watu wakapiga makofi pa pa pa, lakini hawakujifahamu ile kofi kujipiga hawakuielewa tafsiri yake. Kwa sababu tunaonesha ni dhahiri udhaifu wetu tuliokuwanao, kwa sababu sheria tumetunga ndani ya Baraza hili haikufuatiliwa, ndio maana yake. Kwa sababu kungekuwa na sheria hii mawaziri husika wameitekeleza vizuri basi tusingepata tabu leo, watoto wetu wasingeandamana.

Mhe. Spika, kama kusema ndio kufanikiwa mimi ningemuomba Mhe. Rais hebu anipe nafasi moja katika uwaziri nioneshe mfano. Kwa sababu lazima tuseme ukweli unapopewa dhamana uwe *serious* na lile jambo, ni aibu kabisa leo vijana wetu wanafika hadi kutaka kuandamana tunashindwa kutafuta *funds*, fedha za kuwasomesha hiki kilio kinasikitisha sana Mhe. Spika, na ndio maana ikawa waheshimiwa wote hapa wako *serious* kabisa kwa suala hili na muda umetupa mdogo ungetuongeza na keshi hii hoja nzito Mhe. Spika. Kama hakuna pesa za kikao kesho wajumbe wako tayari wakopeshe, wako tayari kwenda *free* hao ili hoja hii twendenayo vizuri.

Lakini niseme kwamba wenzetu wanapokwenda katika vikao vya Muungano mawaziri bado hawajawa *serious*. Mhe. Spika, hii 4.5 tungeikazania yasingetukuta yote haya, mishahara ungekwenda vizuri, mambo ya masomo yangekwenda vizuri, lakini isiwe mimi waziri nakwenda pale na *briefcase* mchezo umekwisha narudi basi, tutafika wapi? Hii ni haki yetu 4.5 imo ndani ya sheria ya Katiba ya Muungano lazima tupewe, lakini hatusimamii vizuri. Mawaziri jamani mnatuchosha huku *back bencher*, ukweli ni huu tukwambieni halafu mkiambiwa ukweli mtununie, tutasema kweli hatutoacha hali ngumu huko.

Leo wanafunzi wanaandamana usione ajabu kesho na wafanyakazi wakaandamana pesa haitoshi, mpaka leo hawajalipwa mishahara yao, kwa nini wasiandamane. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ninachoomba kuwa tunakubaliana na hoja hii ya Mhe. Hamza kwa asilimia mia moja.

Lakini kifungu cha 6 kuhusu habari ya safari za viongozi. Mawaziri wetu wengi wanasafiri lakini *Wallahi* mpaka leo sijawahi kusikia hata mmoja kusema nimekuja na *activity* hii tuifanyeni hii kazi.

Mhe. Spika, tumekwenda China juzi sisi tumetoa *proposal document* yetu lakini mpaka leo sijaona, tumekwenda nute kuifunga Ramadhani kule na Ramadhani yenyewe sijui kama itakuwa halali Mwenyezi Mungu atusamehe. Lakini tumerudi ripoti yetu mpaka leo sijuii kama Waziri wa Fedha tayari yuko katika *plan* ya kuifanyia kazi, sidhani kama kuna kitu kama hicho. Kama tunakwenda na mfumo wa China basi sidhani kama tutafikia watoto wetu katika hali hii ya kushindwa kusoma.

Mhe. Spika, la mwisho hivi karibuni kuna vijana wetu wamekwenda kusoma China, la kusikitisha wamerejeshwa, wamekwenda kusomeshwa katika Mfuko wa *MACEMP*. Hii

inasikitisha hebu tukae nao tuwasikilize, wamefika katika *level* nzuri sana ndugu zetu hawa, wametumia muda mkubwa sasa tutaingia hasara bure serikali, leo wanaulizwa wako wapi wale wanafunzi? Jamani hii aibu, tunakwenda kusomesha vizuri *finishing* yake inakuwa *poor* hatuwamalizii. Sasa na hilo Mhe. Spika, ningeomba kabisa tuwaone hawa na tuwamalizie katika matatizo madogo madogo ili tuwarejeshe wameshajua lugha ya Kichina na wako katika *standard* nzuri ningeomba tuwarudishe hao watu ili waweze kumaliza *course* zao kwa salama usalimini.

Lakini tunakuja katika kifungu nambari 8. Mhe. Spika, si vibaya mtu kwenda kumuomba baba yake jambo. *OIC* siku zote tunaisema hapa tunaambiwa kwa mujibu wa katiba haturuhusiki, lakini kwa nini tusiombe na sisi binadamu. Ametoa mfano hapa Mheshimiwa wangu kuna mambo mengi tu yalifanyiwa marekebisho na yakapelekwa kule, kwa nini hili tushindwe? Hii ni moja katika mkombozi basi naomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais suala hili lazima likaliwe vizuri tukawaombe wenzetu tuondoshe tatizo hili la kila siku kuwa hatuna pesa.

Juzi kwa taarifa fupi tu *ZRB* wamekusanya fedha shilingi *billions* kwa muda wa mwezi mmoja. Ukizunguka huku unaambiwa hakuna pesa sasa mimi najiuliza *why?* Najiuliza kabisa kuwa huku mwezi mmoja wamekusanya mabilioni ya fedha tena nawashukuru sana kwa makusanya yao mazuri hakuna myao inayopenya kule. Mhe. Waziri hongera sana wapelekee hao *ZRB*.

Lakini ukija katika kusaidia unaambiwa fedha hakuna, sasa Mhe. Spika, ningeomba hilo tuliangalie tuwe makini kabisa. Kwa kumalizia mimi nasema ingekuwa inawezekana basi ningemuomba Mhe. Rais anipe wizara moja tu nifanye *example*, siisemi ipi kwa sababu nikiisema wizara fulani nitatiwa chura wa tumbo, lakini siisemi, niambiwe tu hiyo hidaya chukua muone kama sikuifanyia kazi.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, naomba na mimi niunge mkono hoja pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope kwa kuwa wengi wasomi na hii *effect* imewakuta na wao. Ahsante sana Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwana napenda nikushukuru na mimi kunipatia nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu katika hoja ambayo imewasilishwa asubuhi ya leo na Mhe. Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura.

Mhe. Spika, kwanza nataka niseme kwamba Mhe. Hamza ametumia nafasi yake na sisi Wajumbe wa Baraza lako tukufu tumemsikiliza na serikali imemsikiliza. Lakini mimi nitakuwa na machache tu ambayo nataka nieleze kwa kutoa zaidi ufafanuzi katika maelezo ambayo Mhe. Hamza ameyasema.

Kwanza nataka nimhakikishie Mhe. Hamza na wananchi kwa ujumla kwamba serikali haina ubaguzi wowote katika kuwasomesha vijana wake. Tokea Mapinduzi ya mwaka 1964 serikali imekuwa ikifanya hivyo na itaendelea kufanya hivyo, sioni sababu ya msingi ambayo serikali itaweza kuieleza kwa kusema kwamba inawabagua wanafunzi

wake. Serikali haiwezi ikawabagua vijana wake. Kwa sababu vijana wanaosomeshwa leo ndio viongozi wa kesho.

Mimi niliposomeshwa nilikuwa kijana sikudhani kama nitakuwa kiongozi lakini leo nathubutu kusema kwamba ni kiongozi. Kwa hivyo, serikali haina ubaguzi katika hili na ndio maana tukawa tunawasomesha wanawake na wanaume, weupe, weusi, walemavu, wenye viungo, wote sawa tu kila mmoja anasomeshwa. Nasema Mhe. Spika, ilimradi sifa zilizoelezwa ndani ya sheria hii unakidhi ndio hapo utakapoweza kufaidika na mkopo.

Nataka nitaje *paragraph* mbili, namshukuru sana kaka yangu Mhe. Ali Mzee Ali kwa kutoa ufafanuzi katika sheria hii. Nataka niseme sheria hii tumeipitisha mwanzoni mwa mwaka huu, Mhe. Rais ameisaini mwezi wa nane mwaka huu, bajeti tumehitimisha tarehe 30 Julai, 2011 wakati huo ilikuwa tayari bajeti imeshapita sheria hii imesainiwa. Ni hivi juzi tu Wajumbe wa Bodi wameteuliwa sio rahisi kwa muda mfupi huu wajumbe hawa kutekeleza maoni ambayo hapa yamezungumzwa.

Lakini kuna mjumbe mmoja alizungumzia kuwa serikali haikuwa makini kujua ni idadi ya wanafunzi wangapi. Serikali ilikuwa makini sana, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali walileta mahitajio yao shilingi 15.3 bilioni, wali-*focus* kwamba kama hao wanafunzi ambao watamaliza kidato cha sita wata-*qualify* kuingia Chuo Kikuu mahitaji ni shilingi 15.3 bilioni. Uwezo wa serikali ukaangaliwa ikaonekana shilingi 15.3 bilioni kwa sekta moja hatuna tukawapa shilingi 4 bilioni ili waweze kufanya majukumu ambayo sheria hii iliwataka na wao wafanye.

Kuna kifungu kimoja hapa Mhe. Spika, kinaeleza *very clear* na naomba nikinukuu kwa ruhusa yako, kinasema: "*Eligibility for loan* kifungu cha 20(2), *the quested course must be in line with the demand of the National Development Programs"*. Sijui kama hao wanafunzi ambao wanaambiwa wamekosa mikopo kama *course* zilizoombwa ziko *in line* na *National Development Programs*. Nasema Mhe. Spika, tunapokuwa tunazungumza mambo mengi tuangalie sheria tulizozitunga sisi wenyewe.

Sasa Mhe. Spika, nataka niseme tena jengine. Mhe. Waziri asubuhi hapa alipokuwa anazungumza tulisema kwamba huu Mfuko ni *revolving fund* si mfuko wa kukopa halafu watu wanaondoka tu hawalipi. Mhe. Waziri alisema kuna shilingi bilioni saba hazijarudishwa, Mhe. Hamza katika taarifa yake anatafuta shilingi bilioni mbili na nusu, kuna saba hazijarudishwa.

Lakini nasoma tena naomba ninukuu Mhe. Spika, kwa sababu hizi sheria tumezitunga wenyewe.

Kifungu cha 24 kinasema kwamba,*"Loan repayment*,

Kifungu cha 24(2)

> "*The loan granted under sub section 19 of this act shall be paid immediately by the student when he is employed as the board may direct"*

Sheria inataka walipe wanafunzi shilingi bilioni saba zimekaa wanafunzi wanatembea nazo wenzao wanasababisha na wao wakose mikopo. Lakini Mhe. Spika, tusiangalie mwanafunzi ambaye anaingia sasa hivi tukasema kuwa kuna wanafunzi 1300 hawajapata mikopo, ukiwapa leo mikopo wote 1300 maana yake mwaka kesho huna wanafunzi 1300 wanaohitajia mikopo, utakuwa na wanafunzi zaidi ya 6000 wanaohitaji mikopo, hawa uliowapa leo, wanaoendelea na mwaka kesho watakaokuja, serikali uwezo wake ni mdogo.

Mhe. Spika, serikali nasema uwezo wake ni mdogo sio katika sekta ya kutoa mikopo tu, katika sekta zote. Namshukuru sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ameipongeza sana *ZRB*, nataka nimwambie *ZRB* na *TRA* kwa umoja wao tunakusanya *nearly* shilingi 18 bilioni. Katika pesa hizo Mhe. Spika, kuanzia mwezi wa Oktoba mwaka huu shilingi 9.9 bilioni zinakwenda kwenye mishahara.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, sio kama serikali ina ubaguzi, serikali haitaki, lakini kitambaa cha shati shona shati, kitambaa cha koti utashona koti. Tumesema kwa umoja wetu na Baraza hili limepitisha Mhe. Spika, mwaka huu tunaanza na kupandisha mishahara. Tume-*change structure* ya mishahara tumeambiwa na Baraza hili walimu wa sayansi wanatukimbia, madaktari wanatukimbia, leo Mhe. Spika, tumemtoa daktari kutoka shilingi laki tatu mpaka laki saba, tumemtoa mwalimu wa *art graduate* anafika laki tatu na nusu sasa anaanza.

Amezungumza mmoja pale kwamba mishahara mpaka leo haijatoka, nataka nimwambie huwezi ukatoa mishahara *time* unayoitaka wewe mishahara ina *time frame* yake, kuanzia tarehe 23 mpaka tarehe 30 muda wowote unaweza ukatoa mishahara. Nataka niwahakikishie Baraza hili tumesha-*deposit* pesa zote za mishahara kwenye *account* ya mishahara.

Kulikuwa na tatizo tu hapa Mhe. Spika, kwa sababu katika ile balance sheet ya wanfayakazi wa mishahara kuna mapengo tumeyagundua mule, kuna mfanyakazi huyu utakuta hapa ana pengo lazima watu wende wakaangalie kwa nini pana pengo pale wajaze kilichopungua, lakini kuanzia kesho watu wataanza kucheka.

Kwa hivyo, ninachoataka kukisema ni kwamba serikali hii tunaongozwa sisi na Baraza lako tukufu na ndio maana tulipokubaliana kwamba mwaka huu tupandishe mishahara. Tumepandisha mishahara tena tumepandisha vizuri sana.

Lakini Mhe. Spika, nataka niseme jengine kuhusu habari ya hizi hoja ambazo zimetajwa hapa na Mhe. Hamza au mapendekezo yake, kwa kusaidia tu Baraza lako tukufu liweze kufahamu. Mhe. Spika, huwezi ukaondoa pesa kutoka hapa ukapeleka hapa bajeti ya serikali ina njia zake, *it is a continues process.* Katika bajeti za serikali lazima tufuate utaratibu ndio kwa maana Waheshimiwa Wawakilishi nataka niwakumbushe, kuna kitu tulikipitisha hapa tukakiita *Appropriation bill,* ile *Appropriation Bill* ni sheria tuliipitisha sisi hapa.

Sasa haya yote ambayo ameyapendekeza Mhe. Hamza kwamba katika suala la kifedha lazima turudi serikalini, hapa hatuwezi kufanya mahesabu lazima turudi serikalini wataalamu wa utumishi na wataalamu wa Wizara ya Fedha wakae wapeleke kwenye Baraza la Mapinduzi na Baraza la Mapinduzi liseme sasa hicho kinawezekana hicho hakiwezekeni pelekeni tena kwenye Baraza la Wawakilishi, *is a continues process.*
Mhe. Spika, hapa mapendekezo sawa, lakini labda niseme tu hii shilingi 19 bilioni ambayo imeonekana hapa tunataka kuipunguza shilingi 600 milioni labda wenzangu wengine hawakufahamu hizi shilingi 19 bilioni ipo hapa ya nini. Tuliweka sisi wakati wa bajeti wakati ule tulisema hatujajua wenzetu wa utumishi bajeti yao ya mshahara *wage bill* yao itakuwa ni kiasi gain sisi tukaweka *approximately* 19 bilioni.

Mwezi wa *September* Mhe. Spika, mishahara yetu ilikuwa ni *7.7 billion*, kuanzia *October* hii ni *9.9 billion, 2.2 billions* zimeongezeka *monthly* miezi tisa uki-*multiply* unazungumzia suala la *almost 19.8 billion*. Ninalazimika sasa hivi kuwatafutia point 8 niwapatie hawa *extra*, hizi 19 hazijawatosha bado leo tunaambiana hapa tukate hili nikasema aa, bora tufahamishane ili kila mmoja aweze kufahamu msingi wa ile 19 bilioni.

La pili Mhe. Spika, tumezungumza shilingi bilioni nne, pesa hizi ni safari za viongozi wakuu, sio safari hizi jamani za kwenda Unguja, Pemba na Nje aa, mpaka safari zao za kwenda kwenye matatibabu tunatoa hapa hapa na viongozi wakuu labda niwataje hapa muwajue. Kwanza kuna
Rais wa Zanzibar, Makamo wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar hawa ndio walioko madarakani sasa hivi. Kuna marais wastaafau wa Zanzibar tuwahesabuni wangapi wahai, kuna mawaziri Kiongozi wastaafu tuwahesabuni wangapi wahai na kila unapokuwa mzee Mhe. Spika, ndio unahtaji zaidi kwenda kufanya *checking* na matibabu.

Mimi kama siogopi kukwambieni hizi shilingi bilioni nne hazitoshi kabisa, lakini tumeweka hivi kwa sababu tu angalau na wao twende nao, hali sio kama hivyo tunavyoiona Mhe. Spika. Mimi hukamata kichwa kila baada ya muda natafuta fedha zaidi tumeingia hapa tunakusanya shilingi 13 bilioni leo tunazungumzia *almost* 18 – 19 bilioni kwa sababu hiyo.

Nataka nieleze Mhe. Spika, wenzetu Tanzania Bara kuna mmoja hapa alipojadili alizungumzia kuhusu Tanzania Bara. Wenzeti Tanzania Bara katika Mfuko huu wa Elimu ya Juu wakati mwaka juzi na mimi nilikuwa ni naibu Waziri wa Fedha kule katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano waliweka ni nani na nani ambaye anastahiki kuingia huku. Naomba ninukuu, kwanza wakasema wanafunzi wote watakaotoka na *first division*, wanafunzi watakaotoka na *second division* kwa maana ya wanawake tu, wanaume hata wakitoka *second division* hawaingii. Wakaweka sasa *priority areas* madaktari, walimu wa sayansi na mainjinia.

Sasa Mhe. Spika, hapa kwetu hebu tuambizaneni, madaktari ambao wamekosa mkopo kupitia Elimu ya Juu kwa hapa Zanzibar ni wale ambao hawana *admission* na kama huna *admission* kwa mujibu wa sheria hii hustahiki kupewa mkopo, mimi nasema sheria

inavyosema hustahiki kupewa mkopo. Nasema kwamba serikali ina nia safi kabisa inataka kuwa-*train* watu wote lakini tufuate hii sheria, sheria hii tumeinda wenyewe, tumeipitisha wenyewe, tumeijadili, sheria hii tumechukua sisi wawakilishi kwenda katika majimbo yetu tukajadiliana na wananchi wetu ndio kwa maana tuna siku 21, tumerudi tumeikabidhi hii tumempa rais kaisaini.
Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ninachotaka kusema ni kwamba serikali ina nia safi kabisa ya kuwasomesha vijana wake, kinachokita hapa ni uwezo wake na kama huna uwezo Mhe. Spika, huwezi ukatukamua mpaka tukatoka damu mwisho wake tutakufa. Mimi nataka nimalizie kwa kusema kwamba, nia ya serikali ni nzuri hatuna sababu sisi kama serikali kubagua, lakini uwezo wetu ndio unaotufanya tuchukue wachache na kwa mujibu wa sheria hii.

Mimi nitawaomba sana ndugu zangu wa vyuo wanafunzi wote wakifika *Form VI* tu watafute sheria hii waisome halafu atajiona yeye mwenyewe kama yuko *eligible* au hayuko *eligible*, yeye mwenyewe atajiona kwenye sheria hii.

Nimalizie Mhe. Spika, nataka niseme la mwisho kaka yangu Mhe. Ali Mzee Ali pale aligusia, Mhe. Hamza ametoa mapendekezo tisa (9) mazuri, sitaki niyakatae mazuri. Lakini hii ni hoja binafsi, unapochukua mapendekezo ukayaweka kwenye hoja binafsi pendekezo ambalo sheria zenu halihusiani nalo, pendekezo ambalo linahusiana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hata mkilipitisha hapa halina mshiko, tutakuja kuonekana wawakilishi kama sote hatuelewi hizi taratibu. Nazungumza kwa faida yote sote kwa sababu nampongeza Mhe. Hamza kwa kuja na hii hoja na wengine watakuja nayo kesho na keshokutwa na mtondogoo, lakini tuangalie hilo tunalolipitisha tuna uwezonalo kisheria? Kama hatuna uwezo nalo kisheria hatuna mshiko, tutapitisha hapa tutakuwa tunatwanga maji katika kinu tu.

Naomba sana Mhe. Spika, mapendekezo mengine hatuna uwezo nayo hapa, hata ukisema wapige kura hatuna uwezo nayo. Cha msingi cha kufanya ni kukaa na wenzetu tukaongea nao, jengine linalofuata tukasubiri marekebisho ya katiba na tukabadilisha katiba. Hili ndilo ambalo Wazanzibari tuwaombe waangalie kwamba kila wanaloona wao halina maslahi na Zanzibar kwa mujibu wa katiba tuliyonayo, basi waombe tulirekebishe katika mchakato wa katiba. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nakushukuru sana. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Spika, naomba kuchangia hoja iliyoletwa mbele ya kikao chako kitukufu kuhusu mkopo wa elimu ya juu.

Kwanza Mhe. Spika, napenda kumpongeza sana mwasilishaji wa hoja hii kwa kutoa mapendekezo yake mbali mbali ya kutunisha mfuko na kuwapatia mikopo wanafunzi wetu wa Zanzibar wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu.

Mhe. Spika, naomba nikiri kwamba hivi sasa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi wetu ni chache na kwa utaratibu wa kutegemea fedha za serikali zinazopitishwa na Baraza lako tukufu hatutokuwa na utaratibu endelevu. Kwani idadi ya wananfunzi wanaojiunga na vyuo vikuu inazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka. Suala

hili wizara yangu imeliona na bodi ya mikopo ya elimu ya juu ilipoanza kazi zake tu basi lilianza na suala hili, na limeshaanza kuandaa mikakati ya kupata fedha kwa kupitia vianzio vyengine vya mapato.

Mhe. Spika, bodi inakusudia kufanya mazungumzo na taasisi ya fedha, mabenki pamoja na mfuko wa hifadhi ya jamii ya Zanzibar, ili kutafuta uwezekano wa taasisi hizi kuwakopesha wafanyakazi wanaoomba kwenda kusoma katika taasisi ya elimu ya juu. Pia suala la kufanya *fund razing*, limejadiliwa nalo ni jambo ambalo limewekewa mikakati katika bodi yetu, lakini pia jambo hili limo katika sheria ambayo tumeipitisha Mhe. Spika, katika Baraza lako hili.

Mhe. Spika, nasema ni jambo zuri na ni la kupongezwa na bila shaka jambo hili tukilifanya basi linaweza kutusaidia kutunisha mfuko wetu wa elimu ya juu. Mhe. Spika, pamoja na maneno mazuri ya muasilishaji hoja napenda kufanya marekebisho kidogo katika taarifa zilizotolewa katika hoja hii. Idadi ya wanafunzi walioomba mikopo kupitia bodi ya mikopo ya Zanzibar ni wanafunzi 1,603 na wala sio 1,630. Wanafunzi hao kama wote wangepatiwa mikopo basi tungehitaji zaidi ya bilioni 15.3 ili kuweza kukidhia haja. Fedha hizo ni nyingi na kwa sasa hatuna, kwani bajeti yetu ambayo ilipitishwa na Baraza lako hili tukufu Mhe. Spika, ni bilioni 4.

Vile vile wako wanafunzi 1,022 ambao wanaendelea na masomo katika nchi na sehemu mbali mbali duniani ambao wao wanahitaji bilioni 4.8. Hivyo ni dhahiri kuwa bajeti yetu ni ndogo kuweza kuwahudumia waombaji wote.

Mhe. Spika, wanafunzi waliochaguliwa kwa mwaka huu ni wanafunzi 191 na wala sio wanafunzi 300 kama mtoa hoja alivyoeleza. Kuna tofauti kubwa kati ya wanafunzi wale walioomba na wale ambao waliwasilisha barua na kukubaliwa kuingia katika vyuo, yaani *admission later*. Kati ya wanafunzi 1,603 walioomba mkopo ni wanafunzi 833 tu ndio ambao walipeleka *admission later* katika bodi ya mkopo, hivyo wanafunzi 768 hawakuwasilisha *admission later* na hawa ama wamepata mkopo kwa kupitia bodi ya mkopo ya Tanzania Bara au hawakukubaliwa kujiunga na vyuo husika ambavyo waliomba.

Mhe. Spika, vile vile tulipokea maombi 201 ya wanafunzi waliotaka mkopo wa kusoma nje ya nchi. Kati ya waombaji 71 ni kwa ajili ya kusoma shahada ya pili, hawa wote ni wafanyakazi wa serikali maombi yao hayakukubaliwa kwa sababu za msingi, kwa kuwa kuwasomesha wanafunzi nje ya nchi ni ghali sana katika uchache wa fedha tulionao na sio busara kutumia fedha nyingi za kufundishia wanafunzi wachache, hasa kwa mafunzo ambayo yanapatikana ndani ya nchi na gharama zake ni nafuu.

Mhe. Spika, pia tulipokea maombi 142 ya masomo ya shahada ya pili katika vyuo vya ndani ya Tanzania. Mhe. Spika, ni vizuri Baraza lako tukufu kuelewa kuwa bodi ya mikopo ya Tanzania haitowi waombaji wanaotaka kwenda kusoma shahada ya pili au kusoma nje ya nchi. Kutokana na uchambuzi huu idadi ya waombaji waliokosa mikopo ya elimu ya juu ni wanafunzi 400 na sio 1,300 kama mtoa hoja alivyoeleza.

Mhe. Spika, idadi hii ukizingatia kuondoshwa kwa wale ambao hawakuleta *admission later*, walioomba kusoma nje ya nchi na walioomba kusoma shahada ya pili ambapo kwa mwaka huu kutokana na uchache wa fedha hatukuweza kukubaliana na maombi yao.

Mhe. Spika, napenda kukiri kuwa hata idadi ya wanafunzi 400 kwa nchi yetu bado ni kubwa. Wengi waliokosa mikopo ni wanafunzi waliochagua fani ambazo mahitaji yake katika soko la ajira yamepungua. Hasa kwa fani ya sheria na utawala wa umme. Hivyo, bodi iliamua kutokuwakopesha waombaji wa fani hizo, isipokuwa kwa watu wenye ulemavu kwa wasi wasi wa kukosa ajira mara tu baada watakapomaliza mafunzo yao.

Mhe. Spika, ni kweli kuwa bodi ya mikopo ya Tanzania imetenga shilingi bilioni 300 kwa mwaka huu. Pamoja na kuwa fedha hizi ni nyingi sana, bodi hiyo ilipokea maombi ya 37,924 na waliopata mikopo ni waombaji 24,662. Waliokosa ni 13,296. hii inadhihirisha kwamba hata kama serikali zetu zitaongeza bajeti na mfuko wetu utaongezeka bado tutapambana na changamoto ya kuwa maombi mengi kuliko uwezo wetu.

Mhe. Spika, ni jana tu ofisini kwetu tulipata wageni kutoka Benki ya Dunia katika afisi ya Dar es Salaam na walitutahadharisha kwa kutuambia kwamba ni vyema bodi yetu ya mikopo ikajifunza kupitia katika bodi za mikopo ambazo zinaonekana kuwa ni endelevu kama vile bodi za mikopo ya elimu ya juu ya Kenya, ili kuepuka kutegemea bajeti ya serikali pekee.

Mhe. Spika, serikali yetu inajitahidi sana kuongeza fedha kwa mfuko wa elimu ya juu mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, katika mwaka 2009/2010 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitenga bilioni 2.3, kwa mwaka 2010/2011 ilitenga bilioni 2.5 na kwa mwaka 2011/2012 serikali imetenga bilioni 4, ikiwa ni ongezeko la asilimia 60 ya bajeti ya mwaka uliopita. Kwa hivyo, serikali imekuwa na nia dhabiti ya kuongeza fedha inazotenga kwa ajili ya kutoa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Mhe. Spika, wanafunzi waombaji wa mikopo wanateuliwa kwa mujibu wa fani zilizopewa kipaumbele, suala hili lipo ndani ya sheria tuliyoipitisha katika Baraza hili. Kwa hivyo, vipaumbele hivyo vinaweza kubadilika mwaka hadi mwaka kulingana na mahitaji na utaratibu utakao tumika.

Mwisho Mhe. Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kuwa wizara yangu itafanyia kazi mapendekezo yaliyowasilishwa na baadae kuwasilisha serikalini kwa mazingatio zaidi. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, na mimi naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nichangie hoja ya Mhe. Hamza Hassan. Mhe. Spika, hoja iliyotolewa ni nzuri na inaonesha vipi Mhe. Hamza Hassan anakereketwa sana na kuona kwamba watoto wetu hawa pamoja na ndugu zetu, ni lazima wapatiwe fedha kwa ajili ya masomo ya juu.

Mhe. Spika, mambo tisa ambayo Mhe. Mjumbe ameeleza katika maelezo yake ni mazuri sana. Mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya Jimbo la Mgogoni nayaunga mkono sana. Nayaunga mkono kwa sababu mbili kubwa. Mhe. Spika, katika kanuni zetu kifungu cha 48 cha kanuni, kinasema hivi naomba kunukuu;

Kifungu cha 48 cha Kanuni

> "bila ya kuathiri masharti ya katiba au kanuni mjumbe yeyote anaweza kupendekeza jambo lolote, lijadiliwe katika Baraza kwa kutoa hoja, yaani kwa kutoa pendekezo lililokamilika na liwe limewekwa katika hali inayoweza kueleza uamuzi wa Baraza".

Mhe. Spika, muhimu hapa ni kwamba lile pendekezo lake atowe ili Baraza liweze kutoa maamuzi yake, kutokana na pendekezo alilolitoa. Sasa Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan katika hoja yake hii kwenye ukurasa wa 3 chini kabisa amesema hivi;

Ukurasa wa 3 wa hoja, katika sehemu ya chini;

> "Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba ushauri kwa mambo yafuatayo".

Hii ndio simu yake, anaomba ashauri. Kwa hivyo, kwenye maelezo yake yote hayo mambo tisa ni ushauri ambao anautoa, sio jambo jengine ambalo anataka Baraza hili lichukuwe, isipokuwa anatoa ushauri ndio hoja. Lakini hoja hii pia iko katika ukurasa wa mwisho wa maelezo ya Mhe. Mwakilishi. Nanukuu, anasema;

> "Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naliomba Baraza lako tukufu kuijadili hoja yangu hiyo na kuichangia kwa kadiri ya uwezo wenu na tuishauri ipasavyo serikali".

Kwa hivyo, haya ndio maelezo ambayo ameyaeleza kwa mujibu wa kanuni ya 48, ambayo yeye mwenyewe aliinukuu katika ukurasa wake wa mwanzo. Kwa hivyo, ushauri huu Mhe. Spika, ni ushauri mzuri ambao na mimi naukubali kwamba ushauri huu ataishauri serikali. Kwa hivyo, serikali inaposhauriwa inaweza ikaamua kutokana na mashauri yale ambayo yametolewa.

Mhe. Spika, hapa sio kwamba tunatoa maelezo ili tutowe maamuzi, ni ushauri ambao wajumbe wote waliochangia wanasema wanaunga mkono ushauri huu alioutoa Mhe. Hamza Hassan. Hilo ni la kwanza Mhe. Spika.

La pili, naomba niseme kwamba katika maelezo yake haya kwenye vifungu vyake tisa ambavyo vimetoka vya ushauri, naomba niviweke katika sehemu 4. Sehemu ya kwanza ni sehemu ambayo inahusiana na sheria, sehemu ya pili ni sehemu inayohusiana na katiba, sehemu ya tatu ni sehemu inayohusiana na mambo ya Muungano na sehemu ya nne ni mambo ya usawa kwa wanafunzi.

Mhe. Spika, naomba nianze na sheria. Mhe. Spika, ushauri wake alioutoa katika kifungu cha kwanza, cha pili na cha sita hizi ni sheria. Kwa sababu anasema serikali iweke wazi *account* yake ya mfuko wa elimu ya juu, ili mtu au taasisi yoyote anayetaka kuchangia basi achangie hata kama yuko nje ya nchi. Halafu kifungu cha pili ni hivyo hivyo na kifungu cha sita ni hivyo hivyo.

Mhe. Spika, sheria hii ya mfuko wa bodi ya elimu ya juu ilitungwa na Baraza lako tukufu na ikapitishwa hapa na Mhe. Rais aliitia saini tarehe 01/07/2011. Katika sheria hii kifungu cha tatu kinaanzisha bodi hiyo na bodi hii imepewa uwezo kisheria kwamba inaweza ikafanya jambo lolote lile kwa faida ya kuongeza *funds* katika bodi hiyo.

Lakini katika kifungu cha tano Mhe. Spika, inaelezea *functions of the body*, yaani majukumu ya bodi. Majukumu ya bodi yameelezewa katika kifungu cha tano kuna (a) mpaka (n), lakini naomba ninukuu kifungu cha (f), (g), (h) na (i). Hii wanasema tu *solicits for funds and other assistance to promote functions of the body, to receive any gives donations, grands make to the body to organize funds raising activities to formulate some policies* na kadhalika. Sasa hizi ni miongoni mwa kazi za bodi ambazo zimewekwa kisheria. Sasa kama kuna sheria ambayo inasema hivi Mhe. Spika, hatuwezi tena ku-*raise* hoja ya kusema kwamba tunataka mambo haya yatendeke, kwa sababu tukifanya hivyo ni sawa sawa na kusema sheria hii tunaifuta na kama tunaifuta huo sio utaratibu wake wa kufutwa kwa sheria hii.

Mhe. Spika, mimi nilisema hapa kwamba nampongeza Mhe. Hamza Hassan kwa sababu yeye alisema kuwa anaishauri serikali na kuishauri serikali ni kwamba haya yatekelezwe kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo, lile suala la kusema kwamba mambo haya hayapo katika upeo wa serikali sio kweli.

Mhe. Spika, kifungu cha 17 ndicho kinachosema kwamba fedha za bodi hii zitafunguliwa katika *account* maalum na mtu yeyote, chombo chochote au fedha zinazopatikana kwa njia yoyote basi zitawekwa katika *account* ile ambayo itatumiwa kwa shughuli za elimu ya juu. Kwa hivyo, hii ndio sawa sawa na mambo ambayo ameyaeleza katika hoja yake hii au katika ushauri wake huo.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 20 cha sheria hii inaelezea namna gani mtu anaweza kupata mkopo. Kifungu cha 20(1)(b) kinasema lazima mtu awe amekubalika katika chuo ambacho anataka kusoma na lazima apeleke *admission later*, hii ndio sheria inavyotaka. Sasa kama mtu hajapeleka *admission later* ina maana kwamba ha-*qualify* kwa mujibu wa sheria hii na hivyo ndivyo alivyosema Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwamba kuna watu wengi wamepeleka na wengi hawakupeleka. Kwa hivyo, moja kwa moja wale waliokuwa hawakupeleka wanaji–*disqualify* wenyewe.

Mhe. Spika, katika sheria hii hii kifungu cha 28 kinatoa *funds* za bodi zitapatikana wapi. *Funds* hizo zitapatikana katika mambo yale yale ambayo ameyasema Mhe. Hamza Hassan, pamoja na mambo mengine ambayo yameelezwa humu, ni pamoja *funds raising.* Sasa *funds raising* hiyo kama bodi itamualika Mhe. Rais, itamualika Makamo wa Pili, itamualika Makamo wa Kwanza, itamualika Spika, itamualika Mhe. Hamza Hassan yote

ni sawa sawa. Lakini na hili limo, kwa hivyo kama hayo yamo katika sheria hakuna utaratibu Mhe. Spika, wala sio sheria kwamba itoke hoja ya kufanywa mambo yale ambayo tayari yapo katika sheria. Ingelikuwa haiko katika sheria mimi ningekubaliana na yeye sana, lakini haya yapo katika sheria ambayo imepitishwa na pia Mhe. Rais kaisaini tarehe 01/07/2011. kwa hivyo, hayo ni mambo ambayo yanatakiwa yafanywe chini ya sheria.
Mhe. Spika, kifungu cha 28(b),(c),(d) na (e) vinaonesha michango ile itapatikana wapi. Kwa hivyo, hii ni kusema kwamba hoja hizi ni hoja ambazo zote zimo katika sheria na kwa sababu zimo katika sheria, hapa hatuwezi kuchukua maamuzi tena, kwa sababu maamuzi tuliyoyachukua ni sisi wenyewe wawakilishi kwa kutunga sheria hii. La kufanya hapa ni kuharakisha, haya mambo yaharakishwe na ndio huo ushauri aliousema katika hoja yake, kwamba ataishauri serikali kufanywa mambo hayo. Mimi nakubali na ndio nikasema kwamba nakubaliana naye kwamba haya yaharakishwe.

Mwisho kuhusu sheria Mhe. Spika, kifungu cha 31 kinampa uwezo waziri ili kuharakisha haya mambo na ndio maana nafikiri katika hoja yake hasa angetumia kifungu cha 31 cha sheria ili kumtaka waziri anayehusika na mambo ya elimu aharakishe masuala haya. Sasa hii ni sehemu moja ya ushauri wake katika mambo tisa.

Sehemu ya pili ni katiba ambayo hii inaingia katika kifungu cha 3, ambacho anasema kwamba analiomba Baraza lako tukufu liitake Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipunguze shilingi 400 milioni kutoka katika mafungu ya safari ya viongozi. Mhe. Spika, hiyo haiwezekani kikatiba, kwa sababu kikatiba hizi fedha tumeshazipitisha kwenye bajeti iliyopita. Sasa kama fedha zimeshapitishwa katika bajeti iliyopita, katiba inasema na yeye Mhe. Hamza Hassan anajua, tukitaka kupunguza fedha katika fungu lolote tulilolipitisha ni lazima kwa mujibu wa katiba kifungu 106 na kifungu 107 cha katiba ya Zanzibar ni lazima tufanye *supplementary budget*. Sasa hatuwezi hapa kwa hoja tu au kwa ushauri tukachukua fedha katika fungu fulani tukalitumia katika fungu fulani, itakuwa tunakwenda kinyume na itakuwa Baraza lako Mhe. Spika, linakwenda kinyume na katiba na linakwenda kinyume na utaratibu ambao sisi wenyewe tumeutunga. Kwa hivyo, hiyo Mhe. Spika, kwa mujibu wa katiba haiwezekani.

Sehemu ya tatu ni mambo ya Muungano, mambo ya Muungano ni katika kifungu cha 7 na kifungu cha 8. Mambo haya kama alivyosema mwenzangu Mhe. Omar au Mhe. Ali Mzee nafikiri mambo haya yako katika *article* ya 4 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano. Sasa mambo haya sisi tukiyafanya hapa, kwa sababu ni mambo ya Muungano hatuna uwezo kisheria na hatuna uwezo kikatiba, kwa sababu mambo yote ya Muungano. Hata katika katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesemwa, kwamba jambo lolote la Muungano haliwezi kuzungumzwa katika Baraza la Wawakilishi au haliwezi kubadilishwa katika Baraza la Wawakilishi, ni Bunge ambalo lina mamlaka hayo.

Kwa hivyo, tukifanya kitu chochote kuhusu kifungu cha 7 na cha 8 mapendekezo yake, basi itakuwa tunakwenda kinyume, Mhe. Spika, hilo litakuwa ni kosa. Lakini kifungu cha 9 cha mwisho, ni kifungu ambacho mwisho kabisa kinasema kuiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuwaruhusu wanafunzi walioomba Chuo cha Chwaka kujiunga

na chuo, kwani hivi sasa kuna agizo baada ya wiki tatu kama hawajamaliza malipo, basi hawataruhusiwa kujiunga na kuondolewa chuoni.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Mjumbe ajuwe kwamba hapa tunazungumzia vijana wetu Wazanzibari, ikiwa yeye anataka kujiunga na Chuo cha Chwaka au anataka kujiunga na Chuo cha Tunguu au chuo chengine chochote, basi hawa ni watoto wetu wa Kizanzibari. Sasa tunaposema kwamba wanaotaka kujiunga na Chuo cha Chwaka tu ndio wapewe huduma hiyo, itakuwa sivyo. Hatukuja hapa kuwatetea wanafunzi wanaotaka kujiunga na Chuo cha Chwaka tu, lakini hapa tunazungumzia wanafunzi wote au Wazanzibari wote ambao wanataka kujiunga na Chuo Kikuu. Kwa hivyo, hoja hii Mhe. Spika, au ushauri huu, nafikiri ni ushauri uliokuwa hauna msingi kwa misingi ya ubaguzi, itakuwa tunabagua kwa vijana wa Chwaka, lakini vijana wengi itakuwa hatuwatakii mema.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kama ulivyosema kwamba nisichukuwe muda mkubwa. Hoja hii au ushauri huu ni ushauri kwa serikali, ushauri mzuri ambao naukubali na ni ushauri wa kuufanyia kazi katika suala hili lililoletwa. Zaidi ni kwamba sheria yetu hii kwa sababu inakidhi takriban mambo yote ambayo yameelezwa humu. Mhe. Spika, hapa hatuwezi kisheria kukaa na kuamua tena mambo ambayo sisi Baraza la Wawakilishi tumeshayatolea uamuzi wa kutunga sheria inayohusiana na hayo.

Kwa hivyo, madhali ni ushauri huu Mhe. Spika, na mimi naunga mkono ushauri wake na kwamba serikali ina wajibu wa kuyafanyia kazi hayo mashauri ambayo ametoa hapa. Baada ya hayo Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi).*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza na mimi natangulia kukupa shukrani kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja hii.

Pili na mimi niungane na wenzangu kwamba nadhani hakuna haja haikuletwa kwenye *House of Lords*, yaani si Baraza la Mamwinyi. Kwa hivyo, hii kwa Kiingereza tungesema *House of Commons*, yaani ni ya makabwela, sidhani humu ndani kama kuna mtu yeyote ni limbukeni wa umasikini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani wengine tunaweza kuwa malimbukeni wa utajiri, kwa sababu hatujawahi kuupata, lakini sio umasikini kwani tumetokea huko na sisi bado ni *first generation* ya umasikini wa kweli kweli. Kwa hivyo, hii *impression* inaweza kuja kwenye hii hoja, yaani mtu anaweza kufikiria labda ni hoja imeletwa kwa watu matajiri, kumbe ni hoja ya masikini wenzetu na imeletwa kwa masikini wenzao tuijadili na tuone ni namna gani tunaweza kusaidiana.

Nasema hivyo kwa sababu naamini kila mtu humu ndani anaguswa na tatizo hili. Kwa mfano, mimi mwenyewe binafsi yangu kama mtu anataka kuthibitisha basi tukitoka hapa tufuatane, wamo ndani mwangu watoto wangu, ambapo ni wajibu wangu wanataka kusoma na wala hawakupata huo mkopo. Kwa hivyo, ninahangaika na leo nimeamkia kwa Katibu na yeye ni shahidi kwa ajili ya kwenda kuchukua fomu ya mkopo *CRDB* nikope kwa lengo la kukopa, ili niwasaidie kusoma. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hoja aliyokuja nayo Mhe. Hamza Hassan Juma dhamira ni nzuri tena ni vizuri ikaonekana isije hii *impression* ya kwamba labda ya humu ndani au walioko huku mbele wao wanaipinga au serikali hawaitaki. Sasa tutaikataa vipi. *(Makofi)*

Jambo la pili Mhe. Spika, naomba kutoa indhari kwa sababu kila tunachokifanya kwenye chombo hiki kikubwa ni *precedent*, yaani tunaweka jambo la kuja kuigwa huko mbele tunakwenda. Lakini kila uamuzi tunaofanya humu ndani basi ni sheria.
Mhe. Spika, la tatu kila uamuzi tunaoufanya na tunalolisema humu ndani maana yake tunawaambia wananchi na wala hatusemi baina yetu sisi peke yetu. *(Makofi)*

Sasa nimeiangalia hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma ambayo ameileta, ambapo na mimi nimesema mwanzo kwamba dhamira yake ni nzuri, kwa sababu hizo ambazo zimenifanya na mimi leo niamkie kwa Katiba hapa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, mengi yaliyotolewa humu kama alivyosema mwenyewe hoja msingi wake ni ushauri. Lakini sisi wazee wetu Mhe. Spika, walitufunza na walituambia unaloweza kulipata kwa mkono, basi usilichukue kwa mguu. Maana ukija ukitaka tena kulichukua kwa mkono hulipati tena hilo, kwani umeshalidharau au umeshaliondolea muawala wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa mfano nikiusoma huu ushauri serikali ifungue *account* nadhani wenzangu tayari wameshalizungumzia. Lakini serikali ifanye *Fund Rising* na Mhe. Rais awe Mgeni Rasmi.

Sasa mimi najiuliza kwa ninavyomjua Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa sababu yeye mwenyewe ni shahidi wakati tulipokwenda China yeye ndiye alikuwa maarufu kuliko sote. Kwa kweli alikuwa maarufu kuliko sote kwa sababu ya cheo chake, yaani Mwenyekiti wa Wenyeviti kule kwa kifupi walikuwa wakimwita *Chair of the Chairs*, nadhani hata kwa Kichina ni rahisi kuita *Chair of the Chairs*. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, unaposema *Chair of the Chairs* suala la kumtaka Rais kuwa Mgeni Rasmi kwenye *Fund Rising* ya jambo zuri kama hili, linahitaji hoja ya kupitishwa ndani ya Baraza, kwa sababu ni *precedent* hiyo Mhe. Spika tunaiweka. Kwa mfano, Rais huyu amekuja na kufungua Vituo vyetu vya Afya Majimbo pamoja na mambo makubwa huko majimboni na wala haijawahi kupitishwa hoja hapa Barazani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ukilileta hapa linakuwa kama vile unawaambia wananchi hii serikali si sikivu, kwamba mpaka ilazimishwe pamoja na kutolewa Hoja Binafsi ndio Rais aje katika jambo zuri kama hili. Sasa mimi nadhani hiyo si *message* nzuri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ndio maana nasema kwamba nchi hii haitojengwa kwa ukereketwa wa mtu mmoja au Baraza hili peke yake ama Mawaziri au *backbenchers* na wala wananchi peke yao, isipokuwa ni hiki kitambaa ambacho kitafumwa na nyuzi zote hizi, basi ndipo kitaweza kuwa madhubuti. Mhe. Spika, ni vizuri tunayoyaamua na tunayoyafanya humu ndani yaoneshe kwamba sisi ni kitu kimoja. *(Makofi)*

Kwa kweli *Government National Union (GNU)* haikuja kufanya kwamba tuwe vipande vipande kwamba wengine wanataka maendeleo na wengine hawataki. Sasa kama vile tulikuwa tukigombea uhuru na walipopata uhuru wengine walipopata madaraka hawajui tena wengine ndio *impression* ambayo mtu unaweza kuipata. Lakini sote bado ni kitu kimoja na hili ni jambo letu pamoja na kila mtu limemgusa.

Mhe. Spika, ni vyema tukaonesha kwamba bado mtu maarufu kama Mhe. Hamza Hassan Juma anaweza kuwa na jambo zuri kama hili, amewapigia simu wenzake amewaambia na wamekwenda mpaka kwenye mkutano na wala sina hakika kama amemfuata kiongozi yeyote wa serikali na kumwambia na kumshauri kuhusu hili na kukataa mpaka likaja hapa kama Hoja Binafsi. Kutokana na hali hii, nasema tunajishtaki sisi wenyewe kwa wananchi wakati mwengine kwa kupitia chombo hiki chao.

Naamini suala hili lingehitaji *engagement* ambapo lingeweza kufanyika bila ya kuja hapa. Lakini nilivyokuja hapa mimi sikulichukia kwa sababu tumepata fursa sote kulionesha kwamba tatizo hili ni kubwa na nia yetu ni moja kuwa tushirikiane katika kuliondoa.

Kwa hivyo, naomba nikubaliane na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria aliposema kwamba ushauri huu uliotolewa ni vizuri serikali ukauchukua kwa ajili ya kuufanyiakazi. Mhe. Spika, msingi wa hoja ni ushauri na wala sio Hoja ya Baraza kumuamuru, hivi tutamuamuru Mhe. Rais kwenda kufanya *Fund Rising*.

Mhe. Spika, sipendi kurudia tena yale aliyosema Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kwamba kuna mambo mengine ni ya sheria na tukiyaamua hapa tunaweka *precedent* kwamba Baraza hili linaweza likaamuru serikali kuwa toa shilingi milioni 400/- hapa na peleka shilingi milioni 400/- pale, futa hizi shilingi milioni 600/- na wala usizitumie na badala yake tumia hizi, sasa hayo ni maamuzi ya ki-*executive* nadhani.

Mhe. Spika, je tujiulize tukifanya hivyo, kwa sababu haya matatizo yapo mengi na wakati mtu anapokuwa na shida Mhe. Spika, basi anaona lile la kwake *immediate* ndio muhimu. Kwa mfano, anapokuwa na njaa wewe ukahangaika ukapata muhogo, basi anakuona tajiri kweli tena anaweza kukuchukia kwa huo muhogo uliopata, kwa sababu anaweza kuona wewe pengine ndio sababu ya yeye kukosa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kama kuna watu wengine wamekosa mikopo, basi anaweza kuona kikwazo ni serikali labda haitaki. Lakini kumbe hajui serikali hiyo ndio inayosomesha watu, inayolipia watu matibabu, elimu tokea chekechea mpaka hatua nyengine, barabara, mishahara, *ICU* na fedha ndio hizi. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa si vizuri kufanya hivyo wakati mwengine kama njia si za busara, basi watu wengine wanaweza kutuona labda ni tatizo na mwengine anaweza kuona, kwa sababu wanasema kwamba mtu anapokuwa na shida kama hii pengine akajua mshahara wako, basi anaweza kusema mshahara wako upunguzwe. Maana yake anaweza kuona labda utasaidia, kumbe vile huo mshahara unaopata Mhe. Hamza Hassan Juma kila siku tunalalamika kwamba majimboni tumebanwa hautoshi. *(Makofi)*

Lakini huyo ambaye umemchukua aje ashuhudie hii hoja, ukenda kumwambia anaweza kukupopoa mawe na kuona kumbe wewe fedha ndio unayezizuia, kumbe hazitoshi na huo ndio ukweli. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, kwa sababu yeye anaweza kuziona nyingi sana na kusema kumbe umekuja kunihangaisha, lakini wewe mwenyewe ndiye unayejua kuwa fedha hizi hazitoshi kutokana na mahitaji yenyewe yalivyo. Kwa hiyo, nadhani huo ni mfano mdogo wa kuonesha kwamba pamoja na kuwa tunaweza kufikiria kama labda serikali haitaki, lakini huo ndio ukweli wenyewe.

Suala jengine la jumla kwamba kwenye hizi hoja nadhani baada ya uchambuzi wa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pale, basi ninachoomba kusisitiza ni kuwa tusijenge *precedent* ya kufanya maamuzi, ambao ama yanakwenda kinyume na sheria au ni maamuzi ya ki-*executive* ambayo serikali ilitakiwa iyafanye.

Mhe. Spika, kwa sababu leo hapa tukisema tunapiga kura kwa ajili ya kuilazimisha serikali ifanye hayo, kwanza ni maamuzi yatakuwa ni kinyume na sheria, pia inawezekana yakawa ni kinyume na Katiba, yaani ni maamuzi pengine tutayapitisha lakini hayatotekelezeka na haitokuwa na faida.

Kwa hivyo, kama ni ushauri basi nakubaliana sana na huu ushauri tuuchukue, lakini na ile indhari ya kwamba haya mambo mengine hayakuhitaji kuja hapa. Jambo la msingi ni *engagement* kwa sababu sote ni kitu kimoja na alisema vizuri Mhe. Ali Mzee Ali (*professor*) kwamba sote ni serikali kwa sababu tunatumikia wananchi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hii *engagement* nadhani tuitumie zaidi kuliko kuja hapa kuonesha wengine wanataka na wengine hawataki, lakini hakuna ambaye atalipinga hili hata mmoja. Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa kweli maelezo ya ufafanuzi waliozungumza Waheshimiwa Wajumbe walionitangulia nasema kwa upande wangu yamekidhi haja. Lakini naomba niseme machache kabisa Mhe. Spika.

Kwanza kabisa hapa alipomalizia Mhe. Mwanasheria Mkuu nafikiri suala la kuwasaidia vijana wetu kwa masomo ya juu hili halina mjadala Mhe. Spika, kwa sababu sote humu tunataka tuwasaidie vijana wetu. Kwa kweli serikali iko *very serious* na kama tunaambiwa hatuko *serious* basi si kweli Mhe. Spika. *(Makofi)*

Kwa mfano, nimekwenda kwenye vitabu vya bajeti miaka mitano iliyopita Mhe. Spika, nimeanza mwaka 2007/2008, mwaka huo serikali iliweka shilingi bilioni 1.45 kwa Mfuko wa Elimu ya Juu. Vile vile mwaka 2008/2009 tukaweka shilingi bilioni mbili 2, mwaka wa tatu 2009/2010 tuliweka shilingi bilioni 2.3 tunaangalie *trend* inavyokwenda juu tu, inakwenda juu kwa sababu ya kuweza ku-*cop* na ongezeko la wanafunzi. Mwaka jana 2010/2011 tumetenga shilingi bilioni 2.5 na mwaka huu kama alivyoeleza Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali shilingi bilioni 4. *(Makofi)*

Hali hii yote inaonesha Mhe. Spika, vipi serikali yetu inavyojali vijana wetu wasome. Kwa kweli hii Mhe. Spika, inasisitiza kwa ule wingi wanavyojitokeza. Kwa mfano, mwaka huu juzi tu kulikuwa na karamu Ikulu Mhe. Rais amekwenda kula chakula na wale vijana waliofanya vizuri, jumla walikuwa ni vijana 116 waliopata *Division I. (Makofi)*
Kwa upande wa *Form IV* ni vijana 92 na *Form VI* ni vijana 24, wakati zamani ilikuwa hatupati *figures* hizi tunahangaika, lakini leo *Alhamdulillah* vijana wetu wamefanya vizuri, hivyo tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hii ni *progress* nzuri niseme na leo nathubutu kusema tunapanga tusomeshe nani na vipi wenyewe, kwa sababu yale mapungufu ya wataalamu tulionao basi leo tunapanga, yaani tunao uwezo wa kupanga kwani vijana tunao.

Mhe. Spika, sijui kama Waheshimiwa Wajumbe wote walipata wasaa wa kulipitia Gazeti la Zanzibar Leo toleo la tarehe 12/10/2011. Kwa kweli toleo lile lilitoa orodha wa vijana wote wale waliopata udhamini wa Mfuko wa Elimu ya Juu, yaani walitumia kurasa kama nne.

Mhe Spika, nilipata bahati ya kulipitia, basi kupitia kwangu nimekuta mule hizo fani walizoomba hawa vijana na wale waliopata si chini ya fani 25 tena ninalo, hivyo hizi tunaziita kama *rare professions* maana sio kama kila mtu anakimbilia hizi.

Sasa hii nataka kusisitiza kuwa Mkopo wa Elimu ya Juu ni *privilege* kwamba yule anayefanya vizuri na anakwenda kwenye *rare professions* ndio anayetizamwa mwanzo na wala haina maana kwamba wengine wataachwa, isipokuwa wanatizamwa mwanzo kuwa hawa. Mhe. Spika, lengo letu ni kusomesha kule kwenye mapungufu na baadaye tutawajia hao wengine. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naipongeza sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na serikali kwa jumla kwanza kutulia na kufanya uchambuzi yakinifu. Kwa kweli hizi *professions* ukiangalia hizi gazeti na ninawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tukalipitie hili gazeti, yaani utaona hasa ule mtiririko wa vijana wenyewe pamoja na zile fani walizoomba, nikizisoma hapa nitachukua dakika zako na wala nisingependelea hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, wamezungumzia vile vigezo na hili ni suala la msingi nalo. Kwa kweli sio wote wame-*qualify* kupata huo mkopo, ni vyema haya mambo tuyazingatie.

Nafikiri Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ametueleza, ukipitia hapa utakuta ile *figure* aliyoizungumza Mhe. Hamza Hassan Juma haifikii, labda pengine ni vijana 400 tu ndio waliobakia. Kwa hivyo, hili ni suala la msingi kabisa la kuzingatia.

Lakini kubwa zaidi ambalo nataka kuzungumza Mhe. Spika, ni kwamba haya ni mashauri ambayo ni mazuri kabisa ameyaeleza Mhe. Hamza Hassan Juma, basi kama na mimi mzazi pia ninao watoto kama Waheshimiwa Wajumbe wengine. Kwa hiyo, mashauri haya tunayachukua serikali kwa ajili ya kuyachambua pamoja na kuyafanyiakazi, ili tuone mwakani tutakwenda vipi na tuongeze kiwango gani cha fedha.

Vile vile Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wamezungumza vizuri kabisa na wala sitaki kurejea wakati huu tena kwenda kuichokoza bajeti sirahisi kabisa.

Mhe. Spika, hii ni kawaida ushindani wa kupata ufadhili siku zote upo. Kwa mfano, hata *scholarship* zinatangazwa kwenye magazeti na watu wana-*apply*, lakini baadaye wanaambiwa wanaitwa watu fulani kwenye *interview* na ule ni ushindani. Kwa maana hiyo, ushindani kwenye kupata *sponsorship* na hata kupata kazi na hayo ni mambo ya kawaida kwenye maisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimalizie kwa kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu hasa Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Wenyeviti), ambaye amewasilisha hii Hoja Binafsi. Kwa kweli mimi kwa upande wangu niseme kwamba huu ushauri alioutoa unafaa kuzingatiwa, hivyo tutauchukua na kwenda kuuzingatia na tutafanya *very critical analysis*, yaani tutafanya uchambuzi wa ndani, ili tuone vipi tunaweza kufanikisha vijana wetu wakasome. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi kidogo kutoa mchango wangu juu ya ushauri wa swahibu wangu Mhe. Hamza Hassan Juma kuhusu kuwasaidia wanafunzi ambao hawajapata kusoma elimu ya juu.

Kwa kweli yanayohusu sheria yameshazungumzwa na wataalamu wa sheria na wala sina haja tena ya kwenda huko. Lakini kidogo nataka kukumbusha kwamba kuna wakati fulani nilikuwa nje ya serikali ikachaguliwa na Mhe. Haroun Ali Suleiman pamoja na Mhe. Ali Juma Shamhuna chini ya Mwenyekiti wetu Dkt. Mohammed Gharib Bilali kuandika Sera ya Elimu, ambayo mwisho wake nahakika wakati huo sipo ilikuja hapa na ikapitishwa.

Sasa sera ile katika mambo uliokuwa inashauri nikiwa mmoja katika walioshauri, kwamba tulisema elimu ya lazima iwe mpaka darasa la kumi na mbili, nadhani Mhe. Haroun Ali Suleiman anaweza kunisaidia kama hivyo.

Kwa hivyo, kuanzia *Form V, VI* na kwenda juu si elimu ya lazima kwamba kila mtu aipate. Lakini hii ya huku kila mtu lazima aipate.

Mhe. Spika, nakumbuka tulikuwa na mjadala mrefu sana wakati tunajadili sera ile, sasa tukasema lakini jamani tunajua maana yake, kwamba kila tukipanua elimu ya lazima kwenda juu, maana yake huko mbele tunajiwekea uzito kwamba watakuwa wengi waliotayari kusoma elimu ya juu na uwezo tutakuwa hatuna.

Sasa Mwenyezi Mungu amejaalia leo nimeyakuta yale tuliyoyaona kwa ku-*project*, basi leo yanatokea. Mhe. Spika, hivi sasa wanafunzi wamekuwa wengi zaidi wanaotaka kusoma, kwa sababu wengi zaidi wanapata fursa.

Lakini tusisahau kwamba kuna kundi linatoka darasa la saba wanakwenda mpaka *Form II* na hapo wanafanyiwa mtihani. Hivyo, kuna kundi linabaki mitaani na wala hatulizungumzi hili nalo ni tatizo tena ni wadogo na hata uwezo hawana, yaani hawana elimu ya kutosha, taaluma pamoja na maarifa ya kutosha, kundi hilo linatoka.

Sasa baada ya miaka miwili lile kundi lililopenya kwenye tundu linafika *Form IV*, pia kuna kundi linatoka linakwenda mtaani hawana maarifa wala elimu na halafu kinabaki hicho kiwango kidogo ndicho kinachoanza kwenda *Form V* na *VI*. Mhe. Spika, wanapofika *Form VI* pia kuna wengine wanatoka.

Kwa hivyo, kwa sababu ya watu kuachwa nje si hawa tu 1500, kuna hilo kundi tulililoliacha ambalo maarifa yake ni madogo sana na wala hatujaliandalia, yaani hao ndio wanaokula unga mitaani, wanaobaka, wanaochukua vitu na hawa ni kundi kubwa sana, hivyo nilitaka hilo lionekane.

Mhe. Spika, kwa utaratibu elimu yote duniani imekaa hivyo kwamba huku chini ni *base*, yaani wengi na kila ukenda juu inachuja mpaka inafika kwenye *pick*, kwa lugha ya kitaalamu wanasema *pyramid*. Kwa hivyo, kwanza nilitaka watu walijue. *(Makofi)*

Kwa kweli Sheria ya Mikopo imekuja kwa sababu gani, kwani kuna mmoja alikuja hapa na kusema nyote mumesomeshwa. Kweli, mimi ni mtoto wa kimasikini nisingefika hapa leo kama sikusomeshwa bure. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nilifika darasa la saba na ilikuwa zamani unalipia vile visenti vidogo, basi nataka kuingia *Form I* elimu ikatangazwa ni bure na baba yangu alisema *Alhamdulillah* kwamba ndio ikapata nafasi kuingia sekondari, kama ilikuwa ya kulipia basi hivi sasa pengine ni mchukuzi pale Malindi au baharia. Lakini fursa ile ilipotokea nimepata nafasi. Kwa hivyo, sote ambao tumo humu kweli tumesoma kwa *privilege* hiyo. *(Makofi)*

Sasa suala la kutunga na Sheria ya Mikopo limekuja kwa sababu ya *Scholarship*, yaani Misaada ya Elimu ya Juu imepungua sana. Mhe. Spika, atoke mmoja aseme kwamba mpaka amepata *PhD* amejilipia atoke hapa asimame, kama si misaada ya wazungu.

Kwa hivyo, hiyo haipo sasa na kwa sababu mahitaji ya wataalamu tukawa bado tunayataka, ndio tukalazimika sasa kwamba basi tufungue huu mfuko wa watu kukopeshwa, mfuku huu wa watu kukopeshwa umekuja baada ya Bara ndio walioanza na kwetu mwanzo ilikuwa hakuna, yaani sisi ilikuwa tunaendelea kujishika shika.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema kwamba fursa ya elimu kwa hawa ambao hawajapata nao wanastahiki kupata, lakini uwezo ndio kama vile ulivyoonekana hapa na ushauri wa Mhe. Hamza Hassan Juma kuwa na hawa wapate.

Kwa kweli na mimi ninao watatu nyumbani kwangu Mhe. Spika, natakiwa niwasomeshe kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu, lakini wamekwama kwa sababu uwezo mdogo. Kwa hivyo, ni sote tunaumia hivi, hivyo ni vyema wengine lazima waende na wengine wangojee.

Mhe. Spika, kuna Mhe. Mjumbe mmoja alieleza hapa, ambalo nalo ni suala la msingi alisema kwamba sawa fedha za Wawakilishi za Majimbo mwaka huu zipelekwe huko na wala sina hakika kwamba Sera imeshakwisha na wala Sheria imeshatungwa.

Kwa hivyo, sawa mwaka huu tuzipeleke huko na zikatumike, lakini mwakani ilizungumzwa hapa hao watakaoingia mwaka huu, mwakani watakuwa mwaka wa pili, sasa watakapoingia mwaka wa pili kuna wengine wanaokuja mwaka wa kwanza fedha za Wawakilishi ziende huko. Mhe. Spika, hao watakaokuwa mwaka wa pili baada ya mwaka wanakwenda mwaka wa tatu fedha za Wawakilishi ziende huko.

Kutokana na hali hiyo, tukubaliane kwamba miaka yote kuwe na fungu la wawakilishi ambalo linakwenda huko na hivyo si kweli. Sasa tunaweza kufanya maamuzi na tukaona leo laini, lakini mwakani yakatukaa na hilo nilitaka lieleweke hivyo.

Jambo la tatu kuna ushauri ambao ulitolewa na Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba wale wanaokwenda Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka waachiwe. Nadhani asisahau kama kuna Chuo cha Afya Mbweni na wao watasema hivyo waachiwe na kwa vile anavyonipenda, basi atasema na wao waachiwe kwa sababu wataongeza madaktari.

Lakini ninavyoamini na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora anacho Chuo cha Utumishi wa Umma na yeye tutasema aachiwe. Vile vile na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo naye anacho Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar.

Kwa hivyo, sasa tupitishe Sera nzima kuwa Elimu ni Bure kuanzia darasa la kwanza mpaka utakapofika kama zamani. Lakini tulipitisha sera kwamba mwisho *Form IV* na kama tunataka kufanya hivyo, basi turudi tena hapa Barazani na tuseme tunarudi kule mwaka 1964 kwamba Elimu Bure mpaka mwisho, je tunao uwezo huo. Mhe. Spika, naomba kukaa kitako. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi Makamo wa Kwanza wa Rais: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuchangia kidogo katika hoja hii binafsi ya Mhe. Hamza Hassan Juma ambae mimi kwa nafasi yake ni Mwenyekiti wangu katika Kamati ya kusimamia Ofisi za viongozi wakuu wa serikali na huwa anatusaidia sana katika kazi zetu za kamati, kwa kweli kwa uelewa na mashirikiano makubwa ambayo anatupa. Na mimi niseme kwamba nampongeza kwa jitihada yake hii ya kuona mambo kama alivyosema anayaona yeye historically ilikuwa najaribu kuisikiliza ile hoja binafsi jinsi alivyowaona wale vijana na kule ambako walikuwa wanataka kuelekea, lakini akaona awastopishe awaelekeze vizuri.

Kila mtu katika kufika sehemu fulani kuna njia nyingi za kupita Mhe. Hamza Hassan Juma na wenziwe waliona wakae na vijana hawa wawaelekeze kama ambavyo ilivyopaswa, mimi ushauri wangu nahisi bado kulikuwa na nafasi ya kwenda moja kwa moja katika vyombo vinavyohusika katika taasisi ya Wizara ya Elimu, pengine kwenye bodi ya mikopo wakaonana na vijana hawa isingekuwa pengine hata kuna sababu ya kuleta ushauri huu ambao Mhe. Hamza Hassan ameuleta kuufanyia kazi humu ndani ya baraza. Lakini ni haki yake na hivyo ndivyo alivyoona yeye mimi namshukuru kwamba ameona hivyo ndivyo alivyoona yeye.

Mhe. Spika, napenda niungane na wale wote waliosema kwamba wote tuliomo humu ndani nia yetu ni moja na ni kuwatumikia wananchi wetu, wenzetu pamoja na mimi ni wawakilishi wa wananchi tumebahatika tu sisi wachache ndio tuongoze katika kupanga mipango ya kuiendesha serikali na wao watusimamie kuona kwamba kule tunakokwenda ndio sawa, lakini wote nia yetu ni kujenga na kama kuumwa na hawa wanafunzi ambao wanakosa mikopo mimi ni mwalimu *by professional* nimefundisha na najua kiasi gani inauma mwanafunzi wako uliyemfundisha ukataka aendelee lakini ikabidi akwame. Ni ngumu sana na kwangu mimi tangu nilipokuwa muwakilshi mpaka leo matatizo haya ni mengi yananijia kwa kadri ya uwezo wangu pale ninapoweza kusaidia nasaidia na wanakwenda. Lakini uhalisia wa hali yenyewe ulivyo inabidi tukubali hali ilivyo huku tukijitahidi kuona kwamba hali itatengemaa.

Mhe. Spika, wakati mimi ninaingia kitado cha nne Lumumba Mhe. Omar alikuwa Form V, wakati ule skuli ambazo nazikumbuka mimi zikiwa na Form IV kama nazikumbuka ilikuwa ni Lumumba, ambayo ilikuwa na madara matano ya Form IV matatu ya Sayansi na mawili ya Art hili nalikumbuka kabisa, kulikuwa na Fidiel Castro sijui wao walikuwa na madasa mangapi, kulikuwa na Beit el Ras, kulikuwa na Mbweni na Mikunguni katika michepuo ile ya ufundi. Hizo ndizo zilizokuwa na Form IV kwa wakati huo pengine idadi ya wananchi pia ilikuwa ndogo lakini vile vile fursa ya wanafunzi kuweza kupata elimu ambayo itawafikisha pale haikuwa kubwa.

Mhe. Spika, lazima tuishukuru sana serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya kazi kubwa kwa kuona kwamba wanafunzi au watoto ambao inabidi wapate haki yao ya masomo wanapata haki hiyo, hivi sasa Zanzibar ni moja katika nchi ya kupigiwa mfano katika Afrika kwa kuandikisha kwa idadi kubwa karibu wote wanaopaswa kuandikishwa kuanza skuli wanaingia skuli. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nitoe takwimu ndogo tu hapa kwa mpaka mwezi wa Machi mwaka huu 2011, walioandikishwa katika skuli ya maandalizi *Nursery* katika skuli za Serikali ni (6,876) lakini katika skuli za binafsi ambazo nazo ni juhudi ya serikali katika kuzihamasisha kuwepo ili kutanua wigo wanafunzi waweze kusoma basi n (26,353) idadi hiyo kwa walioingia *Nursery School* kwa mwaka huu mpaka Machi basi ni (33,229). Mhe. Spika, tuanze kufikiria miaka kumi na mbili ijayo tutakuwa na *demand* kiasi gani ya wanafunzi ambao watataka kuendelea kwa masomo ya juu.

Lakini vile vile mpaka Machi tu mwaka huu walioko Form I mpaka Form II ni (49,934) sasa haya baada ya miaka minne hawa tayari, kwa sababu serikali inajitahidi sana

kuimarisha vifaa sasa hivi tayari, Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ametupa taarifa kwamba kila Wilaya inajengewa skuli moja ya mfano ambayo itakuwa ni ya kuimarisha masomo ya sayansi, tutegemee kwamba wanafunzi hao watakaohitaji elimu ya juu katika fani mbali mbali ambazo tutazihitajia kwa maendeleo yetu watazidi kuongezeka.

Mhe. Spika, lakini kupanga ni kuchagua bado serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunaiona elimu kama ni kipaumbele, lakini wenzangu wametangulia kusema kipaumbele si elimu peke yake. Mhe. Spika, katika mambo ambayo ni *basic miss* ya mwanadamu basi ni maji, maji ni muhimu sana tuna tatizo la maji kubwa ndani ya nchi hii. Mfuko wenyewe wa kupata pesa ili kuweza kuona wananchi wetu wanapata maji safi na salama ndio huo huo ambao tunautegemea pia utoe fedha kwa ajili ya kusomeshea wanafunzi.

Mhe. Spika, baraza lililopita sote hapa tulikuwa ni mashahidi jinsi gani wajumbe wote sisi tunamtaka Waziri wa Afya siku ya bajeti ahakikishe kwamba ICU ipo katika hali nzuri, haya mambo ni mengi lakini vile vile tukumbuke tunaposema tunataka kujenga matabaka, kuna tabaka la wananchi wa nchi hii karibu asilimia 75 wanategemea kilimo kwa maisha yao ya kila siku. Chakula ni kitu cha lazima kwa mwanadamu serikali hii ya Mapinduzi imejipanga kujikita katika kuhakikisha kwamba kutakuwa na usalama ndani ya nchi hii, kuweza kutumia fedha kuboresha kilimo wakati huo huo kutoa nafuu ya pembejeo kwa wakulima ili kuweza kupatikana chakula na usalama wa chakula uwe bora ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, hayo yote yanahitaji fedha hii hii ambayo inakusanywa, kwa hivyo nataka tu wenzangu tukumbushane najua haya wanayajua kwamba sio kwamba serikali inafanya ubaguzi, inachagua au ingependa kusomesha watu kidogo hiyo sio kweli na Mhe. Hamza Hassan Juma amenoti katika hoja yake kwamba kila maendeleo yanakuja na athari zake, tulipopanua wigo wa elimu kwa upanda sana mpaka sasa bado tuna matatizo mpaka kuweka kile kiwango chenyewe cha elimu kuwa bora. Kwa sababu tuna matatizo ya vikalio ndani ya skuli zetu, fedha hizo hizo ndio tunataka tuboreshe hiyo elimu yenyewe, tuna matatizo ya vifaa vya sayansi na mambo kama hayo, kwa hivyo haya ni matatizo ambayo ni kama cheni inaanza sehemu moja na inaendelea mpaka juu, lakini naamini kwamba ni nia ya serikali kuona kwamba itatafuta vianzio zaidi kama inavyoeleza sheira ili kuufanya mfuko huu kuweza kusomesha wanafunzi wengi zaidi, kwa sababu ili tuendelee tunawahitaji hao wanafunzi.

Niwaambie tu ndugu zangu tunaposema vipaumbele hatuna maana kwamba kuna masomo hatuyahitaji hakuna somo hata moja ambalo halina umuhimu katika maisha yetu ya kila siku, historia kama ni somo la *art* lina faida kubwa kwa binaadamu, masomo ya *culture* yana faida kubwa, somo la dini yana faida kubwa haya ndio yanayotujengea maadili ya watoto wetu. Lakini sasa kuna vitu ambavyo sisi wenyewe waheshimiwa wawakilishi ndio tunaolalamikia kila siku, Mhe. Rashid Seif ananyanyuka ndani ya baraza hili anasema hakuna walimu wa sayansi mmejipangaje. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Tuzingatia muda Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi Makamo wa Kwanza wa Rais: Tumeona tujikite basi ili tuweze kutatua matatizo hayo kwa hivyo mimi imani yangu kwamba serikali tunapokea huu ushauri kwa yale ambayo tutaweza kuyafanyia kazi, ni kitu kizuri tuko pamoja na Mheshimiwa sote ni wadau katika hili, kama yeye alavyoumia na kutokwa machozi Mhe. Spika, mimi tu naomba nisilie hapa, lakini nimeshalia mapema kwa kuona jinsi gani wanafunzi wetu wanakosa hii mitaji.
Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na kwa sababu muda wako umebana sana naomba tu niseme kwamba nashukuru kwa ushauri huu na tumeupokea. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe naona muda wetu unakwenda vizuri sana, tuna kazi mbili moja ya kumaliza jambo hili na nyengine kusikiliza hotuba ya kufunga mkutano huu. Kwa hivyo tunahitaji kuongeza muda.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwa vile shughuli zilizopangwa katika orodha ya shughuli za Baraza hazijamalizika na kwa vile muda ambao umebaki kumaliza shughuli za baraza umebakia mdogo, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likubali kutengua kanuni kwa muda ili tuweze kumaliza zile shughuli baraza hii leo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo ya Mwanasheria Mkuu wananyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nahisi kuna mambo mawili matatu naomba nisaidie kidogo , lakini niwashukuru sana wenzangu wote waliotangulia katika kusaidia hoja na kutoa maelezo. Lakini pia nimshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma mimi leo naona faraja kubwa kwamba Mhe. Hamza ameweza kutoa hoja kama hii wakati mwalimu wake nipo hapa, Mhe. Hamza anajua uchungu niliokuwa nao juu yake kwa sababu yeye alikuwa mwanafunzi mimi nilikuwa mwalimu kwa hivyo najua uchungu wa mwalimu kwa mwanafunzi.

Kama vile Mhe. Juma Duni alivyokuwa na Uchungu na mimi kwa sababu kanisimesha *Chemistry* nashukuru sana kwamba leo tumefika hatua hiyo, mwalimu Jume Duni kama umesahau ile *Chemistry* niliyokuwa nayo kidogo nimeipata kwako wewe chuo cha Ualimu.

Lakini pamezungumzwa kitu cha msingi hapa Mhe. Spika, nadhani ni vizuri tukalizungumza hili, lakini kabla ya hapo nizungumzie hii sera kidoto kwa sababu sisi ndio tulikuwa *master mind* wa ile sera, nashukuru mungu alinipa uwezo nikawateua wajumbe aliowataja Mhe. Ali Juma Shamhuna humu ndani wakati ule, Mhe. Juma Duni na Mwenyekiti DK. Gharib Bilali tukawapa ile kazi ya sera. Kwa sababu tokea mwaka

ule serikali ilikuwa imeshaona umuhimu wa kutoa nafasi za elimu kwa vijana wetu, na nchi nyingi duniani zinajaribu kufanya hivyo na zinashindwa na Zanzibar kama tajiri sana lakini kutokana na moyo na uzalendo wa viongozi wake wanahisi mtoto atakapomaliza Form II bado ni mdogo hawezi kujiajiri au kutafuta nyezo nyengine zozote zile, tukaona kuna haja ya kuwapeleka hadi darasa la kumi na mbili.

Mwaka 2010 nashukuru sana darasa la mwanzo la kutekeleza sera ile hivi sasa nadhani linaendelea darasa la pili, ikifika 2022 vijana wote wa Zanzibar nina uhakika watakuwa wamemaliza darasa la kumi na mbili, sasa hiyo ni hatua kubwa ambayo wenzetu wanashindwa hata wenzetu Tanzania bara wamejaribu bado hawajafanikiwa hilo.

Mhe. Spika, limezungumzwa suala la kuwaacha wanafunzi mimi nimekuwa waziri wa Elimu kipindi cha miaka kumi mfululizo, hili suala la kuacha wanafunzi limejitokeza mwaka huu kwa nguvu lakini hata hiyo miaka ya nyuma tulikuwa tunawaacha wanafunzi, mwaka 2004 nakumbuka tumewaacha wanafunzi. Dk. Mwinyi kazungumza mimi tokea nakamata Wizara ya Elimu bajeti yetu ya kusaidia vijana kusoma kwa elimu ya juu ilikuwa haifiki hata milioni mia tano (500,000,000) leo tumekwenda tumefika *four billion* (4,000,000,000) kwa sababu azma ya serikali ya awamu iliyopita na azma ya Dk. Ali Mohammed Shein suala la elimu wamelipa kipaumbele kabisa kabisa na wana uchungu nalo kweli kweli, sote tuna uchungu nalo, na sisi tuna vijana majimboni huko kila siku wanakuja kwa masuala haya haya ya elimu.

Sasa ninachoomba tukubaliane na ule msemo wa msanii maarufu na naomba uniruhusu nizungumze kwa Kimakunduchi, Msemo huu wa ndugu Idrissa Mudu unasema wakati alipokuwa kwenye suala la uzazi wa mpangilio watoto ni wengi nyumbani mama anapiga kelele.

Anawaambia:

(Navyaa tu vano wana nnga hunawatizama, nnga sabuni hunaleta)

Akasema : (Akasema sabuni naleta heya haba)

Kwa hivyo na sisi pesa kutoka Wizara ya Fedha tunapata bado hazijatosha kwa sababu vipaumbele viko vingi, na mimi naamini kweli sote tuliopo hapa sio kwamba tuna akili sana kuliko wenzetu wa *back bencher* yuko Mheshimiwa mmoja kasema na sisi tuna uwezo vile vile kuna siku tutakaa huko mbele, nawaambia kwamba kweli hata sisi huko majimboni kuna wazee wana akili kuliko sisi wawakilishi.

Kuna mzee mmoja mimi kwenye jimbo hiyo ni hadithi nyengine hiyo alinambia.

Alisema:

(Mheshimiwa Mwezi wa Ramadhani unakuja ukaja kuno unletee chochote).

Mhe. Spika, mwezi wa Ramadhani kufika nikakusanya tambi na tende nikapeleka akanambia wewe umeshakuwa waziri lakini maarifa yako madogo, mimi tende napata msikitini bure ukisikia chochote mapesa.

Sasa Mhe. Spika, nasema turidhike na hiki ambacho tumekipata lakini isichukuliwe kwamba sasa hivi ndio kwanza tumeanza mwaka huu kuwaacha wanafunzi, tulitoa *priority* kwa masomo kama ilivyotolewa sasa hivi sisi wakati ule tuko pale Wizara ya Elimu *public administration* tulipunguza kwa kiasi kikubwa tu labda kwa maeneo au vijana maalum ambao hawana njia nyengine ya kusoma masomo mengine. Lakini tulipunguza sana au tuliondosha *business administration* vile vile, sheria, dini na tatizo lilitokeza hata hao wanaosoma dini na kiarabu wakishamaliza huku Chukwani basi wakifika maskuli kuna walimu wengi wa kiarabu na dini basi wanasomesha masomo mengine, kutakuwa na haja gani ya kuendelea kutoa *sponsor sheep* katika masomo hayo kuyapa *priority* sio kama si muhimu ni muhimu, lakini tunaangalie pale ambapo serikali imeweka *demand* zake.

Kwa hivyo naomba sana waheshimiwa hili suala sisi wazo lililokuja hoja aliyoleta Mhe. Hamza ni nzuri na tumeiona kuna haja ya kukaa tukaitafakari na kuona njia gani katika bajeti inayokuja tukaona serikali itafanya vipi katika kui- *community* mambo haya ambayo yamezungumzwa hapa. Mimi nashauri tena kwamba hili jambo ni zuri tumetoka mbali tunakumbuka na waheshimiwa wapo hapa *Form V* ya mwaka 1974 wenye *credit* tatu hawakutimiza hata darasa moja ilibidi wenye *credit* mbili tuwakopeshe wakati huo na mimi nilikuwa mwanafunzi, wakakopeshwa *Form V* walipofika *Form* VI wameshaikomboa *credit* yao wakafanya mtihani wa Form VI kwa sababu huwezi kufanya mtihani ule kama huna *credit* tatu tulikuwa tunatoka huko.

Mimi leo nina furaha kusikia kwamba hapa tunaona na tunashuhudia wanafunzi karibu elfu moja na wanataka kuendelea na vyuo vikuu hii ni fahari kubwa ya kujipongeza, lakini kweli kila mwaka tutazidi, mwaka huu tumetoa bilioni nne na zingetolewa hata bilioni nane zisingetosha. Hapa sote waheshimiwa tujitahidi kuimarisha uchumi wetu ili mambo yetu yawe mazuri na Ishaalla Mungu atatujaalia tutafanikisha hilo. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, na mimi nisingependa nichukue muda wako mrefu kwa sababu nitakuwa na muda mrefu zaidi wa kusema, lakini na mimi nimshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma na nimpongeze kwa kutumia nafasi yake hii ya kuwatetea wananchi wa Zanzibar, kwa sababu hawa wanafunzi ambao tunatakiwa tuwasaidie kuendelea na elimu yao ya juu ni miongoni mwa wananachi wetu hapa Zanzibar.

Serikali inajua sana tatizo hili, tatizo la wanafunzi wetu na vijana wetu kukosa kupata mikopo ya kuendelea na masomo yao limezungumzwa hapa kwamba hili sio tatizo jipya, matatizo yamekuwepo mwaka hadi mwaka kwamba baadhi ya wanafunzi waliofaulu kuendelea na masomo ya juu kuwaacha wasiweze kuendelea. Sio kwa sababu serikali haipendi waendelee au haitaki vijana hao waendelee, isipokuwa tatizo ni uwezo serikali ina mambo mengi ya kufanya na mambo yote haya yanawagusa wananchi. Elimu

inawagusa wananchi, maji yanawagusa wananchi, afya inawagusa wananchi, mishahara inawagusa wananchi na yote haya lazima yafanywe na serikali.

Sasa hatuwezi kuwa na mfuko mkubwa sana wa kuweza kuyatekeleza mambo haya kwa ukamilifu wake, mpaka leo tunazungumzia habari ya matatizo ya maji mpaka leo hii, mpaka leo tunazungumzia habari ya matatizo ya afya. Sasa hakuna kitu ambacho tunaweza kukifanya tukakimalisha *hundred passent*, suala la elimu wanafunzi kuendelea na masomo ya juu hakuna nchi katika Afrika inayoweza kutoa mikopo kwa wanafunzi wao wote kuendelea na masomo yao ya juu hakuna labda ulaya, ambapo kule *system education* yao ni tofauti au China na kwengine lakini kwa Afrika hakuna.

Sasa hizi jitihada ambazo tunazifanya tunazifanya kwa nia safi na pale ambapo haiwezekani basi wananchi watuvumilie tuweze kujipanga vizuri kuhakikisha kwamba tunaandaa utaratibu mzuri kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu hawa, vijana wetu hawa wanaweza kuendelea na masomo yao, isije ikachukuliwa dhana kwamba ndani ya Baraza la Wawakilishi kuna watu fulani tu ndio wanaotaka wanafunzi hawa wapate mikopo na wengine hapana, hapana sote kwa umoja wetu humu ndani tunataka watoto wetu wasome. Hiyo ndio adhma ya serikali kwamba kila mwanafunzi ambae amepata mafanikio ya kuendelea katika vyuo vikuu basi aendelee na Chuo kikuu kwa sababu na sisi tunataka tuwe na jamii iliyosoma vizuri na ndio maana tukaambiwa hapa kila mwaka bajeti katika mfuko wa elimu inapanda.

Lakini hatuwezi kukamilisha mambo haya yote kwa wakati mmoja Wizara ya Elimu tumeambiwa imeomba bilioni kumi na tano (15,000,000,000) serikali haina tufanye nini, huku na huku wamepata bilioni nne (4,000,000,000) hazikutosha, san asana mwakani tunaweza kuongeza kidogo tukasema bilioni tano (5,000,000,000) hazitoshi kwa sababu mwamko wa vijana wetu kusoma umekuwa mkubwa, vijana wengi sasa wanasoma kwa bidii. Na sisi humu ndani Wawakilishi na wabunge kama mimi hivi tunawahamasisha vijana wetu wasome na sisi sote hapa tukiwa na majimbo tukenda majimboni huko tunayapata.

Mimi kama mbunge nakwenda jimboni kwangu nayakuta kwa hivyo matatizo haya yapo na nina hakika kabisa kwamba Mhe. Hamza Hassan Juma hakuleta hoja hii kuwatetea vijana wake wa Kwamtipura, amewatetea vijana wa Zanzibar yote, sisi serikali tunalielewa hili na tutajitahidi kadiri tunavyoweza kuhakikisha kwamba kila mwaka tunaongeza angalau vijana wale waliomo ndani ya sheria wanapata elimu ya juu.

Mhe. Spika, ushahidi wa kwamba mambo mengi sana yanayowagusa wananchi wetu ni muhimu ni wakati wa bajeti, tuliona hapa mtafaruku uliotokea wakati wa kujadili Wizara ya Afya kwa sababu gani kwa sababu wizara ile inawagusa wananchi. Tumeona mtafaruku hapa wakati wa kujadili bajeti ya Wizara ya Maji kwa sababu gani kwa sababu maji yanawagusa wananchi na mambo mengine, pamoja na mishahara nayo vile vile inawagusa wananchi. Kwa sababu serikali haiwezi kumuajiri mtu bila ya kumtafutia sheria, kwa sababu ile ni *contract* ukisha mpa barua ya kumuajiri ina maana umuwekee mshahara wake hukumpa mshahara wake ina maana unakwenda kinyume na taratibu za uajiri, kwa hivyo haya yote ni muhimu.

Sasa Mhe. Spika, sisi tumeyapokea huu ushauri wa Mhe. Hamza Hassan Juma mimi ningependa sana kwa niaba ya serikali tuwachiwe ushauri huu twende nao, tukaujadili na tuone utaratibu upi utatusaidia katika kuhakikisha wanafunzi wetu hapa wanaendelea na masomo yao. *(Makofi)*

Mengine haya yaliyotolewa ushauri humu ndani kama ilivyoelezwa na wenzangu Mhe. Abubakar Khamis Bakari amezungumza kwamba mambo mengini ni ya kisheria, mengine ya kikatiba hatuwezi kuyaamua na haya yote sisi tuachiwe twende tukayajadili serikalini tuone hatua za kuweza kuzichukua kwa manufaa ya Zanzibar na watu wake.

Labda nizungumzie hili suala la *OIC* Mhe. Spika, mimi nalifahamu sana hili na nilikuwa nalifuatilia ndio maana mara moja nilitoa taarifa hapa barazani kwamba sasa hivi Tanzania haiwezi kujiunga na *OIC* kwa sababu wanafanya *reform ya organization* yao mpaka hapo watakapomaliza nimejuaje kama sikufuatilia, kwa hivyo na haya nayo tunafuatilia watu wasione kwamba tumekaa sisi hatuitakii mema Zanzibar tunaitakia mema na maslahi yake lazima ipate, kwa hivyo na haya nayo mambo mengine haya tutayachukua serikalini tutakwenda kuyafanyia kazi na kuchukua hatua ambazo tunaona ni muafaka kwa nchi hii.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mimi nilikuwa sina haja ila nilitaka nihitimishe tu baada ya Mawaziri kuzungumza na kuliomba Baraza lako tukufu, kwamba mambo haya yote na ushauri uliotolewa basi serikali imesikia michango ya waheshimiwa wawakilishi tumeisikia, wameunga hoja mkono na sote tumeiunga mkono hoja hakuna mtu anayeikataa. Lakini lazima Serikali ikakae ili kuweza kuyatafakari na kuchukua hatua kwa utaratibu unaofaa.

Mhe. Spika, nakushukuru sana. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza na mimi nikushukuru kwa mara nyengine kunipa fursa hii kusimama tena mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kutoa ufafanuzi baadhi ya michango. Lakini nitaomba uniruhusu nisiwataje wajumbe wote waliochangia kwa kuokoa muda. Mhe. Spika, nashukuru sana hoja yangu imepokelewa na hakuna mjumbe yeyote aliyesimama hapa akaipinga. Kwa hilo Mhe. Spika, kwa kweli nakushukuru sana.

Lakini kabla ya hapo nataka niseme kwamba mimi ndiye Hamza Hassan Juma. Nasema hivyo kwa sababu kila mmoja ananitafsiri anavyotaka yeye au anavyoona yeye. Mimi natekeleza wajibu wangu kama Mwakilishi wa wananchi wa Kwamtipura, lakini vile vile kwa Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, sitaki kuwa maarufu, mimi nipo hapa Barazani huu sasa hivi mwaka wa 11 kama umaarufu basi ningelikuwa nimeshaupata huko nyuma. Lakini bado natekeleza majukumu yangu kama kiongozi niliyechaguliwa na wananchi.

Mhe. Spika, kuna mifano mingi nimenukuliwa hapa mara ICU, mara barabara, leo elimu. Mheshimiwa kila kitu nakichangia kwa wakati wake. Nilipokuwa nikichangia suala la ICU ililetwa hapa Barazani Bajeti ya Serikali. Bajeti ya Serikali inapokuja hapa sio kama *rubber stamp* kwamba ikishakuja hapa wameshapitisha wao ndio tuikubali hivyo hivyo. Sisi inaletwa hapa ili tutoe michango yetu. Sasa kama mnakasirika hoja yangu ilikuwa sio ya msingi, suala la ICU lilikuwa sio la msingi, kwa sababu hospitali zote tunazozijenga, dispensary, kuna hospitali ya rufaa, mtu anapozidiwa anapelekwa wapi? ICU. Sasa kama hoja hii kuna watu iliwaudhi mimi nilikuwa natakeleza wajibu wangu.

Mhe. Spika, sisi wengine tuna uwezo, mimi nikipiga chafya tu hapa Muhimbili, Regency, kwa sababu nina pesa. Lakini wanyonge kilimbilio Mnazimmoja. Ndio maana mimi sikutaka ijengwe ICU ya Regency wala Muhimbili nilitaka ijengwe ICU ya Hospitali ya Mnazimmoja.

Mhe. Spika, mfano mdogo hivi karibuni tulipata maafa makubwa, meli imezama, watu wamekwenda kuokolewa, haya kama mtu kazidiwa sana anapelekwa wapi? ICU. Kwa hivyo mimi naomba watu wajadili hoja zangu, watu wasimjadili Hamza.

Mhe. Spika, suala la barabara sina haja ya kulirejea kwa sababu nililitaja na limo ndani ya ilani ya uchaguzi, kuna ahadi za Rais. Namshukuru Mhe. Waziri ameniahidi kwamba hali ikiruhusu atashughulikia. Hili sina haja ya kulitolea ufafanuzi. Mheshimiwa narudi katika hoja.

Mhe. Spika, naomba ninukuu baadhi ya maneno tu katika hoja yangu ili nieleweke vizuri. Katika ukurasa wa pili wa hoja yangu ni lisema kwamba.

> "Mhe. Spika, tunaishukuru sana serikali yetu kuanzisha serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzisha ujenzi wa Skuli za Sekondari za kila Wilaya. Lakini isitoshe kuanzisha Vyuo Vikuu hapa Zanzibar. Na hivi sasa matunda yake tunayaona kula kukicha, idadi ya wasomi inaongezeka hapa Zanzibar. Lakini tunafahamu kila maendeleo yana athari zake. "

Nimeanza kunukuu kabisa kwamba kila maendeleo yana athari zake.

> " Kwani tumeanzisha mashule mengi kuanzia msingi, sekondari hadi vyuo, sasa changamoto yetu kubwa ni namna gani tutahakikisha kila Mzanzibari asome hadi ukomo wa uwezo wake."

Haya ndio maoni yangu, hii ndio hoja yangu, naendelea. Nimekuja katika kifungu cha 6 nilisema.

> "Naishauri serikali kushauriana na Mfuko wa ZSSF kuangalia kitaalamu kama itawezekana nao kusaidia kuendeleza mfuko huo. Haya ni mawazo yangu na ndio sehemu ya hoja zangu."

Mhe. Spika, mwisho kabisa katika kunukuu hoja yangu nilisema hivi.

"Mhe. Spika, kwa heshima kubwa, naliomba Baraza lako tukufu kuijadili hoja yangu hiyo, kuichangia kwa kadiri ya uwezo wenu na tuishauri ipasavyo serikali yetu na baadaye tuje na maamuzi ya pamoja kwa maslahi ya taifa letu. Naamini serikali yetu ni sikivu, wana uwezo mkubwa wa kufanya maamuzi mazito hasa linapotokezea jambo zito kama hili. Na sisi tunaahidi kushirikiana na serikali yetu kulifanikisha suala hili.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu naomba kutoa hoja."

Haya ndiyo yalikuwa ndio maoni yangu. Sasa kama nilikosea Mhe. Spika, basi naomba radhi.

Mhe. Spika, sasa nataka nije katika ufafanuzi mbali mbali. Katika hoja ya Mhe. Omar Yussuf, Mufti, rafiki yangu alieleza kwamba serikali haina ubaguzi. Katika hoja hii hakuna kipengele chochote nilichosema kwamba serikali ina ubaguzi.

Mhe. Spika, alieleza kwamba wanafunzi waliopatiwa lone ni wale waliotimiza sifa. Mimi kwa sababu hii hoja kama nilivyosema, sikuileta kwa utashi wangu. Nilikaa na wanafunzi wenyewe na wanafunzi wale tayari wanazo barua zao za *admission*, ndio maana wakawa wanasikitika. Hizo sifa zinazotakiwa vijana wanazo. Leo tunapoambiwa vijana hawa hawana sifa, sijui wamechukua masomo hawajui vipi.

Mhe. Spika, vijana hawa waliwa wameshafanya vikao mbali mbali na wamekwenda mpaka kwenye vyombo vya Habari, wakatoa tamko kwamba wanajiandaa kufanya maandamano. Mhe. Spika, sisi kama ni wawakilishi wako wa wananchi kuwazuia vijana wasifanye maandamano kwanza suala hili tulichukua sisi tuangalie serikali ita *react* vipi ni kosa?

Mhe. Spika, ndio maana vijana hawa tukawambia nyinyi ni vijana wadogo, wachanga, mngelikuwa mmeshakomaa kama Hamza basi ingelikuwa sio tatizo. Kwa sababu hata ukipeya Waswahili wanasema "Ukimuona nyani kapeya basi ameshakwepa mikuki mingi au mishale mingi". Vijana wale niliwashauri nyinyi bado wachanga, mkienda barabarani leo kweli tumekubali demokrasia lakini bado demokrasia tuliyokuwa nayo ndani ya vichwa vyetu, dhana zetu bedo wengine haijawakolea. Mtaanza kuambiwa wengine CUF, wengine CCM, wengine CCM B, wengine CHADEMA.

Mhe. Spika, niliwambia nyinyi ni vijana wadogo hamjaingia katika siasa. Humu katika hayo maandamano mtakayoyafanya niliwambia wataingia vibaka, wataingia wana siasa, wataingia wana harakati, kila mmoja ataingiza lake, wengine watabomoa magari ya watu watavunja viyoo, watachoma magari, faida itakuwa nini? Baada ya kuonekana kwamba mmefanya maandamano ya amani, mnataka kwenda kwa Makamo wa Pili wa Rais, kwenda kudai yaki yenu ya kimsingi ya elimu, matokezeo yake itakuja kuwa vurugu. Fedha ya serikali ikayolipa pengine katika Shirika la Bima kulipia magari pengine fedha hiyo hiyo ndio ingechangwa na serikali katika kusaidia kukwamua hayo maendeleo yenu ya elimu.

Mhe. Spika, huo ndio ulikuwa ushauri wangu na vijana wale walikubali. Ndio maana tukakuomba Mhe. Spika, siku ambayo tutakayosoma hoja hii na vijana wawepo wale pale. Wametusikia kwamba hoja yao imeletwa Barazani imejadiliwa na wao wenyewe wamesikia. Kama uwezo wa serikali ni mdogo wamesikia. Serikali hapa amesema kwamba hakuna aliyekataa hoja hii. Mimi nashukuru kwamba viongozi wote wa serikali waliozungumza wamesema kwamba hoja ni nzuri. Wameshauri vile vile kwamba hoja hii haina haja ya kutolewa maamuzi hapa, wamesema kwamba tutarudi serikalini tutakwenda kukaa na tutaliangalia suala hilo.

Mhe. Spika, nakubali vimenukuliwa vifungu mbali mbali humu vya Katiba, vya nini, wanasema kwamba tumeanzisha sheria na vitu vyengine. Kama sheria Zanzibar tumeshaanzisha nyingi. Mimi jana hapa nilizungumza kwamba Zanzibar katika watu ambao tuna shehena ya sheria na hodari wa kuanzisha mambo ni Zanzibar. Lakini tatizo letu ni katika kutekeleza na kusimamia sheria tunazozitunga hapa. Kama ingelikuwa tunafuata kila tulichokitunga hapa, watoto hawa wasingetaka kwenda barabarani.

Mhe. Hija kazungumza vizuri hapa kwamba kuna karibu bilioni 7 zipo mkononi, watu wanafanya kazi wameshaajiriwa ndani ya serikali, fedha hawalipi. Sasa sio kosa la watoto ni kosa la serikali kushindwa kwenda kuzikusanya zile fedha. Sisi tunapojenga hoja, mimi narejea tena mimi ndio Hamza Hassan Juma mkiniona nimejenga hoja nimeshafanya utafiti na mimi mwenyewe.

Mhe. Spika, kama hujachokozwa huchokozeki. Serikali tumeichokoza imechokozeka. Si wameshasema watakwenda kukaa kuyatafakari haya mambo. Mimi naamini katika watoto wale kama nilivyosema wanazo barua za *admission* lakini fedha wamekosa. Mimi naamini serikali itakwenda kukaa na naamini kuna busara nyingi zitafanywa ndani ya serikali wale vijana ambao wenye sifa, sijasema mpaka yule mtoto aliyekaa barabarani maskani aende akapatiwe mkopo. Tumesema vijana wenye sifa na wao wanajua kwamba sifa wanazo. Ndio maana wakataka kwenda kuandamana.

Mhe. Spika, bado mimi nasema hoja zangu nilizozileta hapa ni za msingi na bado nashukuru kuwa serikali imezikubali na itakwenda kuzifanyia kazi.

Mhe. Spika, nakuja hoja nyengine. Mimi nilinukuu yale mambo niliyoyasema. Nilisema kwamba tupewe *ratio* yetu katika fungu la Mfuko wa Elimu ya Juu wa Serikali ya Muungano. Mimi hakuna mtu kitu anachonikera na anachoniudhi kila tunapozungumza kero za muungano au suala la Muungano akanitajia katiba mpya. Tuna uhakika Katiba mpya ya mwaka 2014 itakuwepo. Kwa sababu hoja hii ndio kwanza inaandaliwa Bungeni, itakuja kwa wananchi, wananchi watatoa mapendekezo yao mbali mbali, mwaka wa 2014 kuna uchaguzi unakuja, yanaweza yakaingia mambo mengi. Katiba mpya mpaka tunakwenda kwenye uchaguzi ikawa isiwe tayari, sasa kwa nini katiba tunayo.

Mimi ndio maana siku zote nasema sisi tumeapa hapa Zanzbiar kwa katiba mbili, Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wenzetu wa Jamhuri ya

Muungano wameapa kwa katiba moja. Kwa nini hii katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania haitekelezwi. Sisi tumekula kiapo cha uongo?

Mhe. Spika, mimi ninapoambiwa tusubiri katiba mpya nakataa. Kuna mambo ambayo yamo ndani ya Katiba ya Muungano hayatekelezwi kimuungano. Walikaa tu watu serikalini wakafanya maamuzi, wakashauriana na yametekelezwa. Mimi siku zote natoa mfano suala la Bandari, hili ni suala la muungano je, tunalitekeleza kimuungano. Suala la TRA, mapato yote ya TRA yanakushanywa na Jamhuri ya Muungano, lakini mimi nasikia tu sijui kama ni kweli, Mheshimiwa alikuwa Maukula Majogo au sijui nani. Walikaa, wakasema Zanzibar ilisema sisi pesa zetu sisi hatutoi. Maukula Majogo akasema basi sawa nyie zenu kushanyeni kwenu na sisi zetu tunakusanya kwetu. Ndio katiba inavyosema hivyo?

Mhe. Spika, kama tuliapa kwa kutekeleza Katiba tuifate kivitendo yote, isiwe tunayatekeleza rebo, mengine tukasema tusubiri katiba mpya. Kama tusubiri katiba mpya basi mimi nadhani ilikuwa tusiape kwa Katiba ya Muungano, kwa sababu inaonekana kwamba sisi wenyewe hatuiamini, ina maana kama ina makosa ina makosa mengi. Mimi nadhani Mhe. Spika, bado kuna mambo mengi ya ambayo ya kushauriana juu ya serikali mbili hizi, kama zikiona kuna athari tunaweza tukashauriana na hayo masuala mengine yatakuja baadaye. Lakini tukisema kila kitu tusubiri katiba mpya, tunakwenda wapi? Mhe. Spika, mimi nimeona haja hiyo siyo ya msingi kwa kweli siikubali hata kidogo.

Mhe. Spika, mimi nilipendekeza katika yale maeneo ambayo nimeyaona kwamba tunaweza tukapunguza mafungu. Bajeti tumepitisha sisi na bado Waziri ana uwezo wa kuleta *supplementary budget* hapa, tutakubali sisi kufanya marekebisho ya mafungu, sisi kwetu sio tatizo na ndio maana moja katika mapendekezo tuliyopendekeza mimi katika hoja yangu nilisema hapa tunasubiri fedha zetu za mfuko wa jimbo. Wengine wanasema sera bado, sheria bado. Lakini fedha hizi Mhe. Spika, sio mpya, fedha hizi zilikuwepo Wizara ya Fedha katika fungu la miradi midogo midogo ya wananchi, sio fedha mpya.

Mhe. Spika, mimi nina akili timamu, ninafahamu ninachokifanya, na ninajua ninachokifanya. Fedha zipo zimeondoka tu Wizira ya Fedha zimekuja Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, sheria kila siku kesho, halafu, kesho, halafu, halafu lugha nzito, lugha nini, tunasubiri, sheria itakuja. Kwa hivyo fedha bado zipo, ndio maana sisi tuka *sacrifice*, tunajua katika majimbo tunavipa umbele vingi, tunadaiwa maji, tunadaiwa barabara, yaani kila kitu, tunasubiri fedha hizo hizo.

Mimi nilipendekeza hapa basi katika hilo fungu la milioni 10 basi japo milioni 2 sisi tuuchangie huo mfuko. Wajumbe wengine wamechangia wakasema milioni 2 kidogo, bora zote milioni 600 za mfuko wa majimbo, zingeliweza kusomesha vijana wengi. Vijana kiu yao kusoma.

wa hivyo bado mimi nilikuwa kama nilivyosema sitaki nijibu hoja mmoja baada ya nyengine, lakini namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Elimu. Namshukuru sana kwa sababu amekubali hoja zangu. Lakini vile vile amesema kuna wenzetu wahisani gani sijui wamekaa nao, wakasema kwamba wajaribu kujifunza kwenye bodi za wenzetu

wanazoendeleza mifuko yao. Haya ndio maneno tuliyokuwa tunayataka. Kwa sababu tunataka huu mfuko sio kwamba tukishakuokoa mwaka huu ndio iwe basi, tunajua kuwa wengine wanakuja.

Mhe. Spika, mimi nadhani mengi nimejaribu kuyazungumza kijumla jumla lakini bado Mhe. Spika, mimi nashukuru sana naibu ta serikali zaidi nashukuru maoni au ushauri aliokuja nao Mhe. Balozi kwamba watakwenda kukaa tena serikalini, wataliangalie tena suala hili. Nawaomba sana vijana wengu maandamano yasiwepo. Mimi naamini ndani ya kipindi hichi kifupi mtaweza kupata maelezo mazuri ya serikali. Nategemea kwa kuwa hoja hii tumeileta hapa Barazani nadhani basi pengine katika kikao kinachokuja hapa tunaweza tukapata maelezo ya serikali kwamba walikaa wakaliangalia vipi hili suala na wamelitatua katika staili gani.

Mhe. Spika, lakini ulitoka ushauri ilikuwa sisi twende kwenye bodi ya mfuko wa elimu, hatuna haja ya kutaka hapa labda tuanzishe *fund raising* aje Mhe. Rais. Tunaanzisha *fund raising* kwa mambo mengi tu, madogo madogo, lakini hili kubwa. Mheshimiwa kama tutaitisha *fund raising* na kwa kuwa sheria ipo mimi nafikiri huo ndio ushauri tuliyoutoa, sawa sawa na mtu kumkumbusha tu. Kwani Mheshimiwa sala kila mmoja si anajua kuwa ni wajibu kwa nini kila baada ya kipindi muadhini anaadhini, inatukumbusha. Na sisi tumeadhini, tumeikumbusha bodi ya mfuko wa elimu ya juu wafanye hii sheria ambayo tumeipitisha. Tunapiga kelele kwamba tunapitisha sheria zinakuwa wakati mwengine zinachukua muda mrefu kutekelezwa au zinakuwa hazitekelezwi.

Kwa hivyo suala la kuanzishwa fund raising, mimi natoa mfano mdogo wa mwisho. Wenzangu wamenitolea mifano mingi. ZFA walikwisha kutaka kutangaza au sijui kama waliwahi kutangaza kwamba ligi ya Zanzibar mwaka huu haitokuwepo. Kutokana na uchungu wa watu kuona kwamba michezo itaanguka Zanzibar. Kuna kampuni nafikiri kama sikosei Kampuni ya SIGAL wamekubali kufadhili ligi ya Zanzibar. Sasa hizo ndio changamoto, jambo linapokuwa zito watu wakaanza kulitamka mimi naamini kuna wafanyabiashara wengi wa Zanzibar Wazalendo, wenye uchungu wanaoweza kutusaidi kulitatua tatizo hili.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache kama nilivyosema kwamba hoja yangu hii sikutaka iamuliwe. Nilikuja kwa ushauri na naamini serikali imakubali ushauri wangu. Mhe. Spika, nawapongeza sana kwa kuweza kuichangia. Ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe mimi nichukue nafasi hii kuwashukuru sana. Kwanza nimshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma, lakini niwashukuru na waheshimiwa wajumbe wote kwa michango. Pia niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri mbali mbali ambao wamechangia jambo hili muhimu. Suala hili lilipokuja katika mikono yangu ili niamue liingia katika orodha ya shughuli zetu au laa. Kwa uzito na umuhimu wa jambo hili nikasema hili acha tukalizungumze.

Waheshimiwa Wajumbe peke yake kuwa na jambo zito ndani ya nchi yetu na tukapata nafasi ya kulizungumza wapa. Waheshimiwa Mawaziri katika michango iliyotoka

tumeeleza kwamba haya tunayozungumza hapa hatujiambii sisi wenyewe tu lakini pia tunawaambia na wananchi wetu. Kama tusingelilizungumza hili maana yake wananchi wetu wasipata kujua haya tuliyoyazungumza humu ndani kiasi cha kujua hali halisi ya serikali, hali halisi ya sheria inasemaje, sheria ya bodi ya elimu ya juu. Kumbe mambo mengi yaliyokuwemo humu yatakiwa yatekelezwe na bodi ambayo imeteuliwa hivi karibuni. Maana yake hoja hii tumekumbuka kazi za bodi watekeleze kama vile sheria inavyosema.

Mambo mengine yaliyoombwa ndani humu ni mambo yanayogusa muungano. Serikali imekubali, nashukuru sana kwamba serikali imekubali kuchukua mambo haya na kwenda kuyazingatia. Pia yale ambayo yanaweza yakapelekwa kwa wenzetu kuyazingatia, mbali ya kuyapeleka hii taarifa ikizungumzwa hapa maana yake ujumbe umekwenda. Nashukuru vile vile kwamba tumefikia hatua nzuri.

Pale kipindi cha asubuhi nilieleza utaratibu tutautumia juu ya kupitisha jambo hili. Kwa *consensus* iliyopita hapa inaonekana hakuna haja. ya kwenda *item* kwa *item* juu ya jambo hili. Kwa sababu jambo limeeleweka, wajumbe tumelikubali sote kwamba kuna umuhimu jambo hili kulizingatia, serikali imekubali kuchukua jambo hili kwenda kulizingatia. Mtoa hoja pia ameshukuru kuwa serikali imeyakubali hayo. Hiyo maana yake tumepitisha jambo hili kwa makubaliano kwamba serikali inakwenda kukaa na kuzingatia mambo haya kama tulivyoyashauri au ilivyoshauriwa katika hoja hii ya Mhe. Hamza.

Basi baada ya hapo mimi niseme tu kwamba jambo hili tunalikabidhi serikali wakakae kuzingatia na yale ambayo yanaweza kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu basi chombo hichi kipo mnaweza mkaleta ili tukaweza tukafikia pahala pazuri zaidi. Vijana wetu pia wameelewa nini tunachokifanya katika chombo hichi kwa ajili yao ambao wao ndio viongozi wetu wa kesho na keshokutwa.

Nichukue nafasi hii kuwashukuru wajumbe wote kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya kwa siku ya leo, kwa bahati imekuwa ni siku ndefu kidogo. Sasa serikali imepokea jambo hili na hakuna maagizo mengine zaidi ya kupokea. Niseme tu na nitoe taarifa rasmin kwamba jambo hili serikali imelipokea na linafanyiwa kazi na serikali kama ilivyoahidi hapa mbele yetu.

Kwa kuwa tunakaribia mwisho ya shughuli zetu nimepata msaada mkubwa sana wa kuendesha Mkutano huu basi nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru wasaidizi wangu, Naibu Spika, na wenye viti kwa kazi nzuri ya kuendesha mkutano huu. Pia nimshukuru sana Katibu na timu yake yote ambao nao wamekuwa tayari wakati wote kuona kwamba shughuli za mkutano huu unakwenda vizuri. Nirudie kushukuru sana serikali kwa sababu kuna mambo yaliombwa na waheshimiwa wajumbe sisi wenyewe kufanya semina mbali mbali kwa ajili ya kurahisisha kazi iliyokuwepo mbele yetu ya kupitisha miswada mbali mbali. Serikali imefanya hivyo, nawashukuru sana serikali kwa kutupa taaluma ili kazi yetu ya kupitisha miswada mbali mbali iwe rahisi.

Ndugu zetu waandishi wa habari, watu wa televisheni, tumekuwa pamoja katika shughuli hizi na yote ilikuwa ni kwa ajili ya kufanikisha kazi ya Mkutano huu wa Tano, wao ndio wanaotusaidia kupeleka taarifa kwa wananchi juu ya kazi zinazofanywa na wawakilishi wa wananchi tuliyokuwemo humu ndani.

Basi nisichukue muda mkubwa niishie hapo kwa ajili ya jambo ambalo lipo mbele yetu.

Katibu wa Baraza: Mhe. Spika, nitoe taarifa tu kwamba shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano huu wa Tano zimekamilika.

Mhe. Spika: Sasa kwa heshima na taadhima naomba sasa nimkaribishe Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

HOTUBA YA KUAKHIRISHA MKUTANO WA TANO WA BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehma, kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana na kufanikisha Mkutano wetu wa Tano wa Baraza la Nane la Wawakilishi.

Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia amani, mshikamano na utulivu katika nchi yetu. Aidha napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kama ilivyokawaida wako kwa umahiri wako mkubwa wa kuliendesha Baraza letu kwa busara, hekima na umakini mkubwa.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Rais wetu mpendwa wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake wa busara, hekima na unaozingatia maslahi ya wananchi. Ni dhahiri uongozi wa Mhe. Dk. Shein unaendelea kutupatia mafanikio makubwa katika nchi yetu katika nyanja zote za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Wahisani mbali mbali wanafurahishwa na juhudi zetu na wanaendelea kutuunga mkono katika hatua zetu mbali mbali za maendeleo.

Mhe. Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa umakini wao wa kuhoji, kuuliza na kutoa maoni yao wakati wa kujadili Miswada na hoja mbali mbali zilizowasilishwa hapa Barazani kwa lengo la kuimarisha utendaji wa shughuli za Serikali na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi. Vile vile, nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri kwa kuyajibu vizuri na kwa ufasaha maswali yaliyoulizwa pamoja na kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali. Ni matumaini yangu kwamba wananchi wamefuatilia kwa karibu na kwa umakini mkubwa, na wamefaidika na majibu yote yaliyotolewa.

Mhe. Spika, katika Mkutano huu wa Tano wa Baraza la Nane la Wawakilishi jumla ya maswali ya msingi 96 yalipaswa kuulizwa lakini ni maswali 92 ndio yaliyoulizwa na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri pamoja na maswali mengine ya nyongeza. Aidha, Baraza lilipokea na kujadili Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Zanzibar kwa mwaka 2009/2010. Pia Baraza lilipokea Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu

wa Udhibiti na Uhifadhi wa Mali za Kudumu za Serikali, pamoja na Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu wa Miradi ya Maendeleo ya Wananchi na Miradi ya *TASAF*.

Katika mkutano huu, Wajumbe kutoka Chama cha Mapinduzi (CCM) nao walipata nafasi ya kumchagua mjumbe mmoja, kwa ajili ya kuwakilisha Baraza hilo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nafasi ambayo iliachwa wazi kutokana na kifo cha aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini na Mbunge wa kuchaguliwa kutoka Baraza la Wawakilishi, Marehemu Mussa Khamis Silima. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahala pema peponi – Amin.

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu lilijadili kwa kina na umakini mkubwa na hatimae kupitisha Miswada mitatu (3) ya Serikali kama ifuatavyo:-

1) Mswada wa Sheria ya kuweka masharti ya kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

2) Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa Shirika la Taifa la Biashara (*ZSTC*), na kuweka Masharti Bora kwa ajili ya Usarifu, Uendeshaji, Uzalishaji Biashara na Ukuzaji Karafuu na Mazao mengine ya kilimo pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

3) Mswada wa Sheria ya kurekebisha baadhi ya sheria na kuweka masharti bora ndani yake.

Mhe. Spika, Mswada wa Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo una madhumuni ya kutunga Sheria ya kuanzishwa na kufanyakazi kwa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kazi zake na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali itafanyakazi ya kuchunguza na kupima vyakula, dawa za kulevya, dawa za kawaida, kemikali na aina nyengine ya bidhaaa za kemikali na kutoa ushauri kuhusiana na uchunguzi uliofanywa na matokeo yake.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Mswada wa sheria hii, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali itakuwa ni wakala wa Serikali na itakuwa ni chombo kinachojitegemea katika kudhibiti viwango vya dawa, kemikali na bidhaa nyengine zinazolingana na hizo. Jukumu hili ni kubwa na muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu pamoja na wananchi wake. Natoa wito kwa uongozi na wafanyakazi wa Maabara hii kufanya kazi kwa uadilifu na bila ya upendeleo ili kutimiza majukumu waliyopewa kwa ufanisi. Aidha, tunaiomba jamii na wadau wote kutoa mashirikiano mazuri kwa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ili irahisishe utekelezaji wa majukumu waliyopewa na Serikali, hasa suala la kupima dawa za kulevya na vyakula vilivyopita muda wake wa matumizi.

Mhe. Spika, Mswada wa pili uliopitishwa ni ule wa kuanzishwa Shirika la Taifa la Biashara (*ZSTC*), na kuweka Masharti Bora kwa ajili ya Usarifu, Uendeshaji, Uzalishaji Biashara na Ukuzaji Karafuu na Mazao Mengine ya Kilimo. Mswada huu una

madhumuni ya kutekeleza maelekezo ya Serikali ya kuliendeleza Shirika la *ZSTC* pamoja na zao la karafuu na mazao mengine ya kilimo. Mswada huu ni matokeo ya utafiti uliofanywa na Wataalamu wa tafiti za kilimo uliozingatia utaalamu wa kisasa katika biashara ya zao la karafuu na changamoto zake. Hivyo, Mswada unakusudia kuanzisha Shirika jipya ambalo litakuwa na malengo mapya na kazi za kibiashara.

Katika kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake, Shirika la Biashara litakuwa na Mkurugenzi Mwendeshaji ambaye atateuliwa na Rais, na pia kutakuwepo Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika ambayo itakuwa na uwezo wa jumla wa kusimamia utendaji kazi wa Shirika. Nia ya Serikali ni kujipanga upya kwa Shirika la Biashara na kuhakikisha linatekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa na kuongeza mapato ya Serikali kwa maendeleo ya nchi yetu kiuchumi na kijamii. Natoa wito kwa Shirika lijifunze kutokana na mapungufu na kasoro mbali mbali zilizopita ili shirika hili liweze kujiendesha kibiashara na kwa mafanikio.

Mhe. Spika, Mswada wa tatu uliowasilishwa na kujadiliwa katika Baraza lako tukufu ulihusu Sheria ya kurekebisha baadhi ya sheria na kuweka masharti bora ndani yake. Madhumuni ya Mswada huu ni kufanya marekebisho katika Sheria mbili ambazo ni (i) Sheria ya Kuzuia Madawa ya Kulevya, Nam. 9 ya 2009; na (ii) Sheria ya Kudhibiti Usafishaji Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu, Nam. 10 ya 2009. Mswada umependekeza kuweka muundo mpya wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti na Kuratibu Dawa za Kulevya ambayo itamjumuisha Makamu wa Kwanza wa Rais kama Mwenyekiti. Ni imani yangu kwamba Mswada huu umekuja kwa wakati, hasa tukizingatia kuwa tatizo la madawa ya kulevya bado lipo Zanzibar na linawaathiri sana vijana wetu, na hivyo Serikali inajipanga upya katika kukabiliana nalo kwa lengo la kuleta ustawi mzuri wa vijana hao, ambapo baadhi wamejitumbukiza katika vitendo hivi haramu vya matumizi ya madawa ya kulevya bila ya kujijua. Ushirikiano mkubwa unahitajika katika mapambano dhidi ya madawa ya kulevya na Serikali itaongoza mapambano hayo.

Mhe. Spika, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar ya 2009/2010 iliwasilishwa na kujadiliwa katika Baraza lako tukufu. Hii ni hatua inayoonyesha nchi yetu inafuata misingi ya utawala bora katika utunzaji wa fedha na rasilimali nyengine. Ripoti imeweka wazi juu ya hali halisi ya uwekaji wa mahesabu ya Serikali pamoja na utunzaji wa mali za umma kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Nachukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais), Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuiwasilisha Ripoti hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar.

Mhe. Spika, nimesikitishwa sana kusikia kwamba watendaji wa Serikali kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wanatumia fedha nyingi kutekeleza miradi ya wananchi, lakini ripoti ya ukaguzi imebaini kwamba taratibu na miongozo kwa mujibu wa Sheria za fedha na Sheria ya manunuzi hazifuatwi ipasavyo wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo. Vile vile, ukaguzi umebaini kuwa mali nyingi za Serikali ziko katika hali mbaya na baadhi yake zinahitaji matengenezo madogo ili ziweze kutumika tena na hivyo kusababisha hasara kubwa kwa Serikali.

Pia, imebainika kwamba Taasisi nyingi za Serikali hazina mpango wa manunuzi wa mwaka kwa mahitaji ya vifaa na huduma mbali mbali zinazohitajika. Aidha, Wizara na Taasisi nyingi haziweki Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu (*Fixed Asset Register*) kwa mujibu wa kifungu namba 264 cha kanuni za mwaka 2005. Kutokana na mapungufu hayo, Serikali kwa mara nyingine tena inatoa agizo kwa Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na wale wote wanaosimamia fedha za Serikali wawajibike ipasavyo kwa kurekebisha kasoro hizo katika Taasisi zao. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakaekwenda kinyume na sheria za fedha na manunuzi hapa nchini.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ulipaji Mafao ya Viongozi wa Kitaifa Nam. 4 ya 1988 na Sheria ya Viongozi wa Kisiasa Nam. 6 ya 1999 na Kutunga Sheria Mpya ya Maslahi na Mafao ya Viongozi wa Kisiasa baada ya kustaafu pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo ulipangwa kujadiliwa Barazani katika Mkutano huu. Hata hivyo, kutokana na haja ya kufanyiwa marekebisho haukuweza kuwasilishwa tena katika Baraza lako kama ilivyoahidiwa hapo awali na badala yake utawasilishwa katika kikao kijacho. Hii ilikuwa ni bahati mbaya sana Mswada huu kutojadiliwa katika Baraza lako tukufu. Sababu iliyopelekea Mswada huu kutokujadiliwa ni kwamba umeandikwa upya na hivyo kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wawakilishi kupata muda zaidi wa kuutafakari na kuvielewa zaidi vifungu vya Mswada huu.

Katika mswada huu hakuna mambo mapya kwani sheria hii ilikuwepo, kitu kilichoongezwa ni kuwaingiza viongozi wengine ambao hawakuwemo katika sheria ya awali ambao ni Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais. Ningependa kuwasihi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuendelea kujenga mahusiano mema na ya kuaminiana baina ya Mihilimi hii ambayo inategemeana. Mhe. Spika, ningependa pia kuvisihi vyombo vyetu vya habari visipotoshe Mswada huu kwa kutoa dhana potofu bali kuelezea malengo halisi ya Mswada wenyewe.

Mhe. Spika, kama sote tunavyoelewa tarehe 10 Septemba, 2011 majira ya saa 9 usiku Taifa letu lilikumbwa na msiba mkubwa na mzito wa kuzama kwa meli ya M.V. Spice Islander 1 katika eneo la Nungwi iliyokuwa ikitokea Unguja kuelekea Kisiwani Pemba.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena na kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nachukua fursa hii kuwataka wale wote walioondokewa na ndugu na jamaa zao kuendelea kuwa na subra. Msiba huu ni wa taifa; ni wetu sote. Wenzetu wametangulia mbele ya haki na kila mmoja wetu ataonja mauti kwa muda, mahala na siku ambayo Allah amemwandikia. Serikali inawashukuru kwa dhati wale wote waliojitolea kwa hali na mali katika kusaidia uokozi. Tunawashukuru wananchi wa Nungwi kwa ushirikiano wao katika kuwaokoa wananchi wenzetu. Tunavishukuru vyombo vya ulinzi, vyombo vya habari na wananchi wote kwa ushirikiano mkubwa waliotoa katika tukio hilo. Vile vile, nachukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wote wa ndani ya Zanzibar na nje ya Zanzibar na nje ya Tanzania zikiwemo Taasisi mbali mbali kwa kutoa michango yao ya hali mali kuhusiana na ajali hii, Mwenyezi Mungu atawalipa kwa mema *Inshallah*.

Mhe. Spika, kama tulivyokwisha eleza mara nyingi Serikali tayari imeunda Tume maalum ya watu 10 ili kuchunguza sababu na chanzo cha ajali ya meli ya M.V. Spice

Islander I. Nawaomba wananchi waendeleze kuwa watulivu huku tukisubiri matokeo ya uchunguzi wa Tume hiyo. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wote kwamba iwapo itabainika kuwepo na uzembe uliosababisha ajali hiyo Serikali itawachukulia hatua kali wale wote waliohusika. Kwa hivi sasa tusitafutane uchawi. Aidha, Serikali inaendelea na juhudi yake ya kufanya mazungumzo na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kutafuta uwezekano wa kupata meli mpya ya uhakika kwa ajili ya kuhudumia safari za Unguja na Pemba kwa njia ya mkopo au ubia.

Mhe. Spika, Serikali, kupitia Mamlaka husika, inaendelea na jitihada za usimamizi wa usalama wa vyombo vya usafiri wa baharini kwa kuimarisha shughuli za ukaguzi wa vyombo na kusimamia ipasavyo upakiaji wa abiria na mizigo. Aidha, Serikali pia inachukua juhudi ya kuimarisha sekta ya usafiri kwa ujumla kwa kujenga miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na bandari. Hivi sasa barabara 4 kati ya 6 za vijijini Pemba zimekamilika kujengwa. Barabara hizo ni Mtambile – Muambe, Mtambile – Kangani, Mizingani – Wambaa, na Kenya – Chambani. Nachukua fursa hii kuwapongeza Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa juhudi zao hizo na kuwataka waendelee na juhudi za kusimamia usalama wa vyombo vya usafiri wa baharini na nchi kavu.

Mhe. Spika, tarehe 03 Julai, 2011 Serikali ilitangaza rasmi bei mpya ya kununulia karafuu kutoka kwa mkulima na hivi sasa Serikali kupitia Shirika la Biashara la Taifa *ZSTC* inanununa karafuu kutoka kwa mkulima kwa wastani wa Tshs. 15,000 kwa kilo ambapo ni sawa na wastani wa Tshs. 21,000 kwa pishi.

Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wananchi, na hasa wakulima kwa kushirikiana na Serikali kwa nguvu zote katika uchumaji wa karafuu kwa msimu huu wa mwaka 2011/2012 ambao hadi sasa unaendelea vizuri sana. Kadhalika naomba kutoa shukrani za pekee kwa wananchi kwa kuuza karafuu zao *ZSTC*. Serikali imepata mafanikio makubwa kutokana na uvunaji na uuzaji wa karafuu katika msimu huu.

Hadi kufikia tarehe 20 Oktoba, 2011 Serikali kupitia Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) imekwisha nunua kutoka kwa wakulima kiasi cha kilo 1,595,620 sawa na tani 1,595.6, ambapo gharama za ununuzi huo ni Tshs. 23,727 milioni (23.73 bilioni) kiasi hicho chote cha fedha kimekwenda kwa wakulima wa karafuu.

Aidha, katika kipindi hicho Serikali iliuza karafuu nje ya nchi tani 1,000 kati ya idadi ya karafuu zilizonunuliwa za *ZSTC*. Kwa sasa Serikali inatathmini mwenendo wa soko la dunia ili kuuza tani nyengine 1,000 hivi karibuni.

Mhe. Spika, kama tunavyoelewa kuwa kwa miaka mingi zao la karafuu nchini mwetu lilikumbwa na biashara ya magendo ambayo kwa kiasi kikubwa zao hilo lilitoroshwa na kupelekwa nchi ya jirani, hivyo kuifanya nchi hiyo kuwa maarufu kwa usafirishaji wa zao la karafuu ingawaje haizalishi zao hilo. Malalamiko makubwa ya wakulima katika kipindi cha nyuma ni bei ndogo ya karafuu wanayolipwa kupitia *ZSTC*. Serikali yetu ilikisikia kilio cha wakulima na kuchukua hatua ya kufanya marekebisho kwa kuiongeza

bei hiyo kutoka Tshs. 3,500 hadi Tshs. 15,000 kwa kilo. Hili ni ongezeko la zaidi ya mara tatu na lilitokana na mwenendo wa bei ulivyo katika soko la dunia.

Mhe. Spika, Serikali inapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza sana wananchi kwa ushirikiano wao wa kuendelea kupambana na vitendo vya usafirishaji wa zao la karafuu kwa njia ya magendo. Zipo dalili nzuri sana za kufanikiwa kwa vita hivi hasa kutokana na mwenendo mzuri wa ununuzi wa karafuu kutoka katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu.

Mhe. Spika, Serikali inazo taarifa kwamba kuna watu wanaojishughulisha na kutorosha karafuu kwa magendo ambao huwahadaa wakulima wa karafuu kuwa *ZSTC* imeishiwa fedha za kununulia karafuu, na wataanza kukopa karafuu zao. Uvumi huu una dhamira ya kutaka karafuu wauziwe wao ili wazisafirishe kimagendo. Serikali inawatanabahisha wananchi na hasa wakulima wa karafuu kuwa watu wanaosambaza uvumi huo ni maadui wa maendeleo yetu na yeyote atakayejitokeza kusambaza uvumi huo, taarifa zake zipelekwe kwenye vyombo vya dola ili adhibitiwe.

Shirika la Biashara la Taifa lina uwezo wa kununua karafuu za msimu wote kwa bei ambayo itaendana na soko la dunia bila ya kuwakopa wakulima. Serikali inawaomba wananchi kuudharau uvumi huo na kuendelea kuuza karafuu zao *ZSTC* na pale itakapotokea kupanda kwa bei ya zao hilo katika soko la dunia, Serikali nayo itawapandishia bei wakulima kadri hali itakavyoruhusu. Aidha, inawaomba wananchi waendelee kushirikiana na Serikali katika kupiga vita magendo ya karafuu.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutoa kipaumbele katika sekta ya elimu kwa kuzifanyia ukarabati skuli mbali mbali za sekondari pamoja na vyuo kama vile utanuzi wa Chuo Kikuu cha Taifa Tunguu, Skuli za Sekondari Tumekuja, Forodhani, Utaani na Fidel Castro. Aidha, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inaendelea kutoa mikopo ya masomo ya elimu ya juu. Kwa mwaka huu Bodi hiyo imepanga kutoa mikopo kwa wanafunzi 191, kati ya waombaji 1,603. Hali hii inatokana na uhaba wa fedha za mikopo. Hata hivyo, Bodi inaendelea kutafuta vyanzo vyengine vya kupata fedha kupitia Mabenki, na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ili kuongeza idadi ya wanafunzi watakaopatiwa mikopo.

Napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa uchaguaji wa wanafunzi waliokubaliwa kupata mikopo umefanywa kwa uangalifu na uadilifu mkubwa kwa kuzingatia vigezo. Aidha, Bodi itaendelea kuwahudumia wanafunzi 1,022 ambao wanaendelea na masomo yao katika vyuo mbali mbali vya elimu ya juu, ndani na nje ya nchi. Serikali inaendelea kutoa wito kwa wazazi kuwekeza katika elimu ya watoto wao na Serikali itaendelea kuchukua hatua kuhakikisha vijana wetu wenye sifa wanapata fursa za kupata elimu bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

Mhe. Spika, madawa ya kulevya bado ni tatizo kubwa linalosumbua nchi yetu na dunia kwa ujumla. Ili kufanikisha mapambano dhidi ya madawa ya kulevya katika nchi yetu, Serikali imeifanyia mapitio Sheria namba 9 ya mwaka 2009 ya udhibiti wa Dawa za Kulevya ambayo siku chache zilizopita ilipitishwa na Baraza lako tukufu. Kilichobaki

sasa ni kuhakikisha kila mmoja wetu anawajibika katika utekelezaji wa Sheria hiyo mara baada ya kutiwa saini na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, tuna wajibu wa kuhakikisha kuwa vijana wanaotumia dawa za kulevya wanaachana na tabia hiyo.

Natoa wito kwa wananchi, tusiwanyanyapae vijana hawa, tuwe nao karibu, na tuwathamini. Hii itakuwa ni changamoto kwao kuacha kutumia madawa hayo. Aidha, natumia nafasi hii kuviomba vyombo vyote husika kutekeleza wajibu wao wa kudhibiti uingizaji, utumiaji na usambazaji wa dawa za kulevya. Serikali inatoa onyo kali kwa wale wote watakaokwenda kinyume na wito huu kwa kuwachukulia hatua kali za kisheria ili kuangamiza kabisa madawa ya kulevya hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Ugonjwa wa Ukimwi bado ni tishio kwa Taifa letu na dunia kwa ujumla. Serikali inatoa wito kwa Taasisi zote za Serikali na binafsi na Asasi za kiraia kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Pili wa Ukimwi kila mmoja kwa nafasi na mamlaka yake. Hivi sasa tumo katika mchakato wa kujiandaa na maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani tarehe 01 Disemba, 2011, ambapo Umoja wa Mataifa umeweka shabaha ya kuwa na "zero tatu" yaani:-

1. Pasiwepo na maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi;

2. Pasiwepo na unyanyapaa na ubaguzi wa watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi;

3. Pasiwepo na vifo vinavyotokana na Ukimwi;

Katika kutekeleza shabaha hiyo, nguvu za pamoja zinahitajika na hivyo kupelekea kuwa na Zanzibar isiyo na Virusi vya Ukimwi. Hii inawezekana. Sote tutimize wajibu wetu.

Mhe. Spika, suala la uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja wetu na limekuwa likisisitizwa kila mara. Serikali inasikitishwa na hali isiyoridhisha ya mazingira machafu ya mji wetu na maeneo mengine tunayoishi. Tumekuwa tukitupa taka ovyo, kuchimba mchanga sehemu zisizohusika, kuendelea kuingiza na kutumia mifuko ya plastik. Kufanya hivyo, ni kwenda kinyume na kauli mbiu ya kutunza mazingira na hali hii inahatarisha afya za wananchi wetu.

Serikali inaendelea kuwashajihisha wananchi katika juhudi za kuhifadhi maliasili kwa kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa misitu ya asili ili kuepusha nchi yetu dhidi ya majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabia ya nchi. Aidha, Serikali inawaomba viongozi na wananchi kusaidia juhudi za kulinda rasilimali zilizomo ndani ya misitu ikiwemo wanyama adimu, maliasili zisizorejesheka, pamoja na uhifadhi na matumizi bora ya ardhi. Serikali inawakumbusha Viongozi na wananchi kwa jumla kupanda miti mingi zaidi na kuitunza, kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji na kulinda mazingira kwa ujumla wake. Hali ya uharibifu wa mazingira ni mbaya sana katika Kisiwa cha Pemba ambapo maji ya chumvi yameanza kuingia ndani ya nchi kavu kuharibu maeneo ya kilimo. Hali hii kama hatua za kuidhibiti haikuchukuliwa inaweza kuleta madhara makubwa.

Nachukua fursa hii kuziagiza Taasisi zote kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika kushughulikia suala la uhifadhi na utunzaji wa mazingira. Aidha, wafanyabiashara wa bidhaa za mitumba, hasa vifaa vya umeme na eletroniki waweke utaratibu mzuri ili kuiepusha nchi yetu kuwa ni jaa la takataka za aina hiyo.

Mhe. Spika, watu wenye ulemavu ni sehemu ya jamii, wanahitaji kupata haki na fursa sawa na wengine. Inasikitisha kuona kwamba ndani ya jamii yetu bado kuna watu wanaowadhalilisha watu wenye ulemavu kwa kuwatumikisha, kuwatenga, na hata kuwalazimisha kufanya vitendo vya ngono, hali ambayo inaweza kuwasababishia kupata mimba zisizohitajika na hata virusi vya Ukimwi.

Napenda kutoa wito kwa familia za watu wenye ulemavu wa aina yoyote, wachukue hatua za makusudi kujisajili kupitia kwa masheha wao. Aidha, nachukua nafasi hii kuikumbusha jamii kwamba tarehe 03 Disemba, 2011 ni siku ya watu wenye ulemavu duniani, ambapo ujumbe wa mwaka huu ni “Jenga maisha bora kwa wote pamoja na watu wenye ulemavu”. Serikali itaendelea kuhamasisha wananchi na wadau mbali mbali kuchangia Mfuko wa Watu wenye Ulemavu ili waweze kuondokana na hali ya utegemezi.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo imechukua uamuzi wa makusudi wa kuuhamisha mnara wa matangazo ulikuwepo Chumbuni na kuuhamishia Bungi, kwani sehemu uliyokuwepo ni njia ya kuanza kutua kwa ndege zinazoingia Zanzibar. Hatua hii imechukuliwa baada ya kupokea malalamiko kutoka kwenye Mashirika ya Ndege kuwa mnara huo kwa mahala ulipo ulikuwa unahatarisha usalama wa safari za anga.

Aidha, serikali imekamilisha utandikaji wa nyasi za bandia katika uwanja wa Gombani, Pemba na hivyo kupelekea uwezekano mkubwa wa kuchezwa kwa mechi za kitaifa na kimataifa katika uwanja huo.

Mhe. Spika, serikali ina mpango wa kuwaendeleza wazalishaji wadogo wadogo wa mazao ya baharini. Aidha, serikali imeanza kutayarisha ziara za mafunzo kwa wafugaji wa mazao ya baharini kwenda nje ya nchi kwa lengo la kujifunza mbinu bora za ufugaji. Jumla ya wazalishaji 18 (wanawake na wanaume) walipelekwa China kwa siku 32 wakifuatana na maafisa 12 na huko walijifunza kwa vitendo uzalishaji wa mazao ya baharini. Kutokana na kushajihika kwa wananchi katika ufugaji, jumla ya vikundi vya uzalishaji wa mazao ya baharini (pweza, chaza, samaki, kaa na mwani) vimeongezeka na kufikia vikundi 85. Hatua hii itasaidia sana azma ya serikali ya kuwapunguzia wananchi umasikini.

Mhe. Spika, kumekuwa na mabadiliko ya mara kwa mara kwa bei za chakula hapa nchini hasa kwa bidhaa za mchele, sukari na unga wa ngano. Mabadiliko haya ya bei yanaathiri maisha ya wananchi wetu. Mabadiliko haya yanatokana na kubadilika kwa thamani ya shilingi yetu (*exchange rate*). Serikali imezingatia hali za maisha za wananchi wake na mnamo tarehe 13 Oktoba, 2011 imefanya mkutano na wafanyabiashara wa ngazi zote

wakiwemo waingizaji, wauzaji wa jumla na wauzaji wa rejereja kwa lengo la kuzungumzia mwenendo wa bei za bidhaa za vyakula hapa nchini. Aidha, baada ya makubaliano yaliyofikiwa na wafanyabiashara, serikali itatafakari na si muda mrefu itatangaza bei mpya ya bidhaa katika soko la Zanzibar.

Mhe. Spika, katika hatua za kuongeza uhakika wa chakula nchini serikali imeandaa mpango wa kutoa ruzuku kwa pembejeo za kilimo na huduma za utayarishaji wa mashamba hasa kwa zao la mpunga. Aidha, serikali inaendelea na juhudi za kuimarisha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji maji ili wakulima waweze kuzalisha kwa tija zaidi bila ya kutegemea mvua. Serikali inawaomba wananchi kuzitumia vyema fursa hizo ili waongeze uzalishaji.

Mhe. Spika, bado tatizo la ardhi hapa nchini ni kubwa ingawa juhudi zinaendelea kuchukuliwa kuondokana na tatizo hilo. Miongoni mwa hatua zinazoendelea kuchukuliwa na serikali ni:-

- Mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi Zanzibar.
- Mapitio ya Muundo wa Sekta ya Ardhi.
- Kuandaa mipango madhubuti ya matumizi ya Ardhi *'National Land UsePlan'*.
- Kuweka usimamizi endelevu wa sekta ya ardhi ikijumuisha usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa sheria zinazohusiana na masuala ya ardhi.

Naendelea kutoa wito kwa Viongozi na watendaji wote katika ngazi zote kuacha kujishirikisha katika migogoro ya ardhi kwa kufuata sheria zilizopo. Wananchi nao hawana budi kutoa ushirikiano wao katika kuondoa matatizo ya ardhi katika nchi yetu. Bado wapo wananchi wanaovunja sheria kwa makusudi kwa kuvamia maeneo yasiyoruhusiwa na hasa sehemu za Maruhubi ambako baadhi yao wameshaanza kujenga majengo. Serikali itayatembelea maeneo hayo na hatua za kuvunja majengo hayo zitachukuliwa bila ya kulipa fidia.

Kwa upande wa sekta ya maji serikali iliahidi upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama mijini na vijijini kwa umbali wa wastani wa mita 250 vijijini na mita 150 mijini. Jitihada zinaendelea kuchukuliwa kwa kuchimba visima, kulaza mabomba na kujenga matangi maeneo mbali mbali ya vijijini kama vile Kizimkazi, Micheweni na Ziwani, sambamba na juhudi za uchimbaji wa visima na ulazaji wa mabomba katika Mkoa wa Mjini/Magharibi ili kupunguza ukubwa wa tatizo la maji unaokabili Mkoa huo.

Mhe. Spika, kabla ya kumalizia hotuba yangu, naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Mohammed Said Mohammed kutoka Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kuchaguliwa kuliwakilisha Baraza letu tukufu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Mohammed Said ana uwezo mkubwa wa kutetea maslahi ya Zanzibar wakati wa Vikao vya Bunge vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongera sana Mhe.

Mohammed Said kuchaguliwa kwako kunaonyesha imani ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wenzako waliyonayo juu yako. Nawapongeza pia Waheshimiwa Mbarouk Wadi Mussa Mtando na Mussa Ali Hassan, ingawa kura zao hazikutosha. Bado nafasi wanayo ya kuomba tena baada ya miaka minne kuanzia sasa au wakati wowote fursa ikitokea.

Mhe. Spika, kwa kumalizia napenda kukushukuru tena wewe Mhe. Spika kwa kusimamia na kuliongoza Baraza letu kwa umahiri mkubwa, kwani busara, hekima zako na miongozo yako inasalisaidia Baraza hili kuwa na taswira nzuri kwa wananchi. Aidha, kwa mara nyengine tena napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonyesha katika kipindi chote cha majadiliano. Nawatakia kila la kheri na safari njema ya kurejea Majimboni mwao kushirikiana na wananchi katika kuendeleza kazi za kuiletea nchi yetu maendeleo.

Mhe. Spika, pia napenda kutoa shukurani na pongezi zetu za dhati kwa Vyombo vyetu vya Habari ambavyo vimekuwa vikifanya kazi nzuri ya kutuunganisha na wananchi huko nje, jambo ambalo limesaidia sana wananchi kufuatilia mambo yote yanayotokea hapa Barazani.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, kwa vile hatutokutana katika hali hii kabla ya mkutano ujao, nachukua fursa hii kuwatakia Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu Sikukuu ya *Eid el Hajj* njema na ya baraka pamoja na heri ya mwaka mpya wa 2012.
Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja ya kuliahirisha Baraza lako tukufu hadi tarehe 18 Januari, 2012.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba hiyo ambayo imeeleza maneno mengi, mambo mengi ambayo tumeyafanyia kazi katika Baraza hili na hatimaye kutoa hiyo hoja. Basi Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Narudia kuwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe wote kwa mashirikiano makubwa ya kuendesha mkutano wa huu wa tano. Sasa napenda kuahirisha Mkutano hadi tarehe 18 Januari, 2012 saa tatu za asubuhi.

(Saa 3:10 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 18/01/2012 saa 3:00 asubuhi)